# UINJILISTI WA KIBIBLIA NA UANAFUNZI

Dr. Stephen Gibson

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki © 2019 Shepherds Global Classroom
Imetafsiriwa kutoka Toleo la Tatu Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa. Isipokuwa kwa kurasa za majaribio, hakuna sehemu yeyote katika kitabu hiki itakayotengenezwa au kutawanywa kwa njia yeyote ile ya – elektroniki, mbinu za utunzi mfupi, kunakili, kurekodi au vinginevyo- bila kibali kutoka Shepherds Global Classroom (SGC). Kila linaponunuliwa toleo la mtalaa wetu wa SGC Kiswahili au Kiingereza kunatusaidia kufanya tafsiri kwa lugha nyingi ili kuvigawa kwa Viongozi wa Kikristo duniani kote. Kwa kuwasiliana na SGC au kuchangia katika maono haya ya kuvutia sana, ingia kwenye tovuti yetu: www.shepherdsglobal.org.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB)."

Usanifu wa jalada: Shane Muir

Tafsiri ya chapisho la Kiingereza kwenda katika Kiswahili imefanywa na:
Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,
Arusha, Tanzania, East Africa.
E-mail: revwangowi@gmail.com

# Yaliyomo


Mtazamo wa Somo....................5
(1) Kukubaliana na Agizo Kuu la Yesu....................7
(2) Theolojia ya Kuzaliwa mara ya Pili....................13
(3) Dharura ya Uinjilisti....................23
(4) Vipengele Muhimu vya Injili....................29
(5) Dhana ya kiuinjilisti (evangelicalism) na Kipaumbele cha Injili....................33
(6) Kazi ya Roho Mtakatifu....................41
(7) Maombi na Kufunga....................47
(8) Mbinu za Yesu....................55
(9) Uwasilishaji wa injili "Daraja"....................65
(10) Barabara ya Kirumi....................71
(11) Kuhubiri Kiuinjilisti....................79
(12) Milango iliyofunguka....................87
(13) Uboreshaji Mbinu za Uinjilisti....................95
(14) Huduma kwa Watoto....................103
(15) Mpango wa Kanisa....................115
(16) Wafuasi wa Kweli....................121
(17) Kuelekea Kukua Kiroho....................131
(18) Kitabu cha Mwongozo kwa Kikundi Kidogo. ....................139
(19) Kuwaombea Wafuasi....................151
Viambatisho Vilivyopendekezwa....................154
Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa....................155

# Mtazamo wa Somo

### Maelezo Kuhusiana na somo

Kozi hili ni nyenzo ya kusaidia kanisa katika kutimiza utume wake.

Kozi hii inatilia mkazo kitovu cha kanisa la mahali, kioneshacho kwamba injili ndiyo utume wa kanisa, na kwamba asili ya injili inapaswa kuonesha sura ya kanisa.

Kwa kuelezea misingi ya injili, kunasahihisha baadhi ya makosa yanayotokana na mfumo wa kisasa ambao haumwelekezi mtenda dhambi kuokoka kiukweli na kuishi maisha ya Kikristo.

Mwanafunzi ataandaliwa kuikuza huduma yake.

mada nyingi katika somo hili zinaweza kufundishwa kama somo kamili kwa ajili ya vikundi mbalimbali. Kwa mfano, somo linaweza kutumika katika kufundisha njia ya kuwasilisha injili.

Katika kozi hii, wanafunzi watajifunza jinsi ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu. Shepherds Global Classroom imetengeneza **nyenzo ya kutumika kuwafanya watu kuwa wafuasi** hususani kwa ajili ya waumini wapya. Kitabu hiki cha masomo cha jinsi ya kuwafanya watu kuwa wafuasi, kinachoitwa, *Masomo ya Kukuza Uanafunzi,* kinapatikana kwa kupakua kutoka shepherdsglobal.com*.* Kila somo katika masomo 26 ya *Masomo ya Kukuza Uanafunzi*, kumewekwa na kitabu cha mwongozo cha mwalimu pamoja na kurasa za wanafunzi.

### Malengo ya somo

(1) Kufafanua maana ya injili kwa ajili ya taswira na muundo wa kanisa.

(2) Kufanya tafakuri ya imani za msingi za injili.

(3) Kuwafundisha waumini njia za vitendo zinazohusiana na uinjilisti.

(4) Kufahamu wajibu wa kanisa katika ufuasi.

(5) Kufafanua maana na kuelezea kazi ya ufuasi.

(6) Kujifunza njia kwa vitendo kuongoza kikundi kidogo kwa ajili ya ufuasi.

(7) Kutoa mfululizo wa masomo mbalimbali kwa ajili ya kutumika kwenye ufuasi wa waumini wapya.

**Ufafanuzi na Maelekezo kwa Viongozi wa Madarasa**

*Mambo ya kukumbuka kwa ajili ya viongozi wa madarasa* yamewekwa katika somo nzima ikiwa ni pamoja na maelekezo kwa ajili ya sehemu maalumu za masomo. *Mambo hayo yameoneshwa kwa herufi mlazo*.

**Maswali ya kujadiliana** na **kazi za ndani za darasa** zimeoneshwa kwa alama ►. Kwa ajili ya maswali ya kujadiliana, kiongozi wa darasa atapaswa kuuliza swali na aruhusu wanafunzi kujibu. Siyo lazima swali lijibiwe kwa usahihi sana wakati wa majadiliano. Mafundisho yaliyoko kwenye somo yatajibu swali hilo. Kama mwanafunzi yule yule huwa wa kwanza kujibu na wanafunzi wengine huwa kimya, kiongozi anaweza akaelekeza swali kwa mmoja wao: ”Emanueli, ni kwa jinsi gani utaweza kujibu swali hili?”

Kila somo linamalizikia na **kazi za kufanya.** Kazi za kufanya zinapaswa zimalizike na kuwakilishwa kabla ya muda wa kuanza somo linalofuata. Kama mwanafunzi hatakamilisha kazi ya kufanya, anaweza akaifanya kwa wakati mwingine. Hata hivyo, kiongozi atapaswa kuwahamasisha wanafunzi kutunza na kuendana na wakati ili waweze kujifunza zaidi kutoka darasani.

Wanafunzi wanatakiwa kukamisha **kazi za kuandika** za aina zote. Kwa kawaida kiongozi wa darasa atapaswa kukusanya kazi zote za kufanya zilizoandikwa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. (Kazi mbili za kufanya Somo la 6, Kazi ya kufanya ya 1, na Somo la 14, Kazi ya kufanya ya 1) hazitahitajika kukusanywa bali zitatolewa taarifa tu.)

Wanafunzi pia watapaswa **watawasilisha Injili** kwa watu wengi kwa kutumia vigezo walivyojifunza darasani. Kila baada ya kuwasilisha, wataandika mambo yanayohusu uzoefu wao na kushirikishana darasani ni kwa jinsi gani uwasilishwaji huo ulivyofanyika. Wataandaa mahubiri ya uinjilisti kwa ajili ya watu wazima na somo kwa ajili ya watoto wadogo. Kuna mitihani miwili katika kozi hii, baada ya somo la 5 na la 10. Wanafunzi watapaswa kuuandika mtihani huu kwa kutumia akili zao tu bila kunukuu kutoka katika maandiko yoyote au kwa kusemezana. Hakuna mwongozo wa majibu unaotolewa kwa mwalimu kwa sababu majibu yanapatikana kwa urahisi kutoka katika masomo ya kitabu hiki.

Somo la 13 linajumuisha pamoja na maelekezo ya jinsi ya kugawa vipeperushi vya injili. Wanafunzi watapaswa kujua ni mahali gani watapata vipeperushi kwa ajili ya kuvigawa. Ikiwezekana, vinaweza vikaletwa wakati wa kipindi cha darasani.

Kama mwanafunzi atahitaji kupata **cheti cha kufuzu mafunzo kutoka Shepherd’s Global Classroom**, atapaswa ahudhurie vipindi vyote vya darasa na amalize kufanya kazi zote zilizotolewa. Fomu imetolewa mwishoni mwa kozi hii kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi za kufanya zilizokamika.

# Somo la 1
# Kukubaliana na Agizo Kuu la Yesu

## Utangulizi

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Mathayo 28:18-20 kwa ajili ya kikundi.

Baadhi ya watu wanaamini kwamba Agizo hili lilikuwa ni kwa ajili ya mitume tu.

► Je, Agizo hili lilikuwa ni kwa ajili tu ya watu waliolisikia siku ile? Elezea jibu lako.

William Carey aliishi mwaka 1761-1834. Alikuwa mzawa wa Uingereza. Alikuwa mshona viatu aliyekuwa na matamanio makubwa ya kuieneza injili. Kanisa lake halikuwa na shauku kubwa ya huduma ya umisheni wa nje. Waliamini kwamba Mungu tayari alishaamua ni nani atakayemwokoa, na kwamba hakutegemea msaada wa mwanadamu.

Kwenye kongamano la wachungaji, Carey alipendekeza mada ya kujadiliwa: aliuliza kama Agizo Kuu la Yesu ni jukumu la Kanisa hadi mwisho wa dunia, kwa kuwa ahadi aliyoitoa Yesu kwenye Agizo Kuu ni kwamba atakuwa pamoja nao hadi ukamilifu wa dahari. Kiongozi wa lile kongamano akasema, "Kaa chini, kijana mdogo. Wewe ni mtu mwenye shauku sana (msimamo mkali). Wakati itakapompendeza Mungu kuwabadilisha wapagani au makafiri, atafanya hivyo bila ya msaada wako au wangu."

Tunajua kwamba Agizo hili lilitolewa kwa kanisa hadi mwisho wa dunia. Yesu aliahidi kuwa pamoja nasi tutakaoipeleka injili, hadi mwisho wa dahari, jambo linaloonesha kwamba jukumu la uwajibikaji liko kwa kanisa kwa vizazi vyote. Wanafunzi wa Yesu hawangeweza kulikamilisha jukumu hili katika maisha yao, lakini Yesu alisema kwamba injili itahubiriwa kwa kila taifa.[1]

Kwa hiyo jukumu la kuhubiri injili linarithiwa na kila kizazi cha kanisa.

► Angalia tena kwa umakini maelezo yaliyoko kwenye Mathayo 28:18-20. Je, ni nini mahususi kinachoagizwa?

Agizo maalumu la Yesu lilikuwa kwamba kanisa liende kila mahali na kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi wake.

Agizo hili ni pamoja na uinjilisti kwa sababu mtu hawezi akawa mwanafunzi wa Yesu hadi pale atakapokuwa ameokoka.

[1] Mathayo 24:14

Agizo hili linamaanisha kwamba kanisa ni lazima lifanye uinjilisti na ufuasi kama kipaumbele chake cha kwanza na kuchukua hatua zenye ari kubwa; vinginevyo, halitatimizi sababu za kuwepo kwake.

Fungu la maneno “ulimwenguni mwote” (kila taifa inamaanisha kila kundi la kabila) inaonyesha kwamba kazi ya umisheni wa nje ni agizo, kwa kuwa makundi ya kikabila hayana injili hadi itakapokuwa imepelekwa kwao. Hakuna aina fulani ya watu wanaopaswa kutengwa.

Agizo lenyewe sio kuhubiri injli tu. Mchakato wa kufundisha ni muhimu kwa sababu tunapaswa tufundishe watu wapya waliookoka kila kitu ambacho Yesu aliagiza.

> “Ninajiridhisha zaidi kabisa kwamba kama tungechukua mwelekeo wa Bwana wetu na ahadi za uhakika alizowapa wanafunzi wake wa kwanza kama mwongozo wetu kamili, tungewakuta nao wanastahili kama ilivyo kwa nyakati zetu kama vile walivyokuwa wamepewa awali..”
> - J. Hudson Taylor,
> “The Call to Service”

Mwalimu ni lazima adhamirie katika kumtii Kristo kwa sababu ni lazima awe mfano mzuri wa kuigwa, akiwaelezea watu waliookoka jinsi ya kuishi maisha yenye kumtii Kristo.

Mtu aliyeokoka ni lazima adhamirie katika kumtii Kristo kwa sababu kujifunza maagizo ya Kristo tu hakutoshi bila ya kutii anayojifunza. Kama siyo mtiifu kwa yale anayojifunza, anapingana na kazi ya ufuasi. Mchakato wa ufuasi siyo tu wa kielimu, bali kubadilika kitabia.

## Uinjilisti ni Kipaumbele cha Maandiko

Mbali na Agizo Kuu la Yesu, kuna taarifa nyingi ndani ya Biblia zinazoonyesha kwamba uinjilisti ni kipaumbele cha Mungu kwa ajili ya kanisa.

*Ukumbusho kwa kiongozi wa darasa: Wanafunzi watapaswa waangalie kumbukumbu za rejea zilizopo hapa chini na waweze kuelezea ni kwa jinsi gani uinjilisti ni kipaumbele cha Maandiko. Wasaidiwe kwa kutumia mapendekezo yaliyotolewa.*

**Mathayo 9:36-38**. Yesu alitaka wanafunzi wake washirikishe huruma zake kwa wenye dhambi na waombe kwamba Mungu atume watendakazi katika mavuno ya kiroho.

**Matendo 4:29**. Wakati kanisa lilipokabiliana na mateso, wasi wasi wao wa kwanza kuhusika hakukuwa juu ya hatari za kimwili, bali kwamba injili ingeweza ikazuiliwa. Waliomba kwamba mbali na mateso yaliyokuwepo Neno la Mungu lisambae maeneo yote.

**Matendo 11:18**. Kanisa la Kiyahudi lilimtukuza Mungu kwamba wokovu umepatikana kwa Mataifa.

**Wafilipi 1:18**. Paulo alifurahia kwamba Kristo alikuwa anahubiriwa hata wakati ambapo alikuwa anateseka kifungoni.

**Waefeso 6:19**. Paulo aliomba maombi ya kina yafanyike kwa ajili ya uinjilisti wenye matokeo.

**Warumi 10:13-15**. Paulo alisisitiza umuhimu wa haraka wa wajumbe wa kupeleka injili kwa sababu wokovu ni kwa ajili ya wale wanaosikia na kuamini.

► Je, kuna sababu gani kadhaa za mwamini kuwa na shauku ya kuona watu wakiokolewa?

**Sababu za Mwamini kuwa na Shauku ya kuona mwenye Dhambi Akiokoka.**

- Anapaswa awe na shauku ya kufuata mfano wa Yesu ambaye aliacha mbingu kwa minajili ya kuja kuishi na kufa kwa ajili ya wokovu wa mwenye dhambi.
- Anapaswa awe na shauku kwamba Mungu aweze kutukuzwa kutokana na kuokoka kwa mwasi hadi kuwa mtu wa kumwabudu Mungu.
- Anapaswa aone injili ikisambaa kila mahali kama ushindi kwa Kristo na upatanisho wake.
- Atapenda kushiriki katika kazi ambayo ni kipaumbele cha Mungu.
- Atapaswa kuwa na huruma kwa ajili ya wanaopotea ambao wanaingojea hukumu ya mwisho kwa sababu ya dhambi zao.

► Je, inawezekana mtu akawa na nia mbaya za kutaka kufanya uinjilisti? Ni sababu gani hizo?

Siyo jambo baya kutamani mafanikio katika huduma na kukua kwa kanisa la mahali pamoja.

Ni muhimu kwamba hatushawishiki katika kiburi cha mafanikio, mashindano na makanisa mengine, au kupenda kubishana.

Baadhi ya waumini wameitwa maalumu na kuwa na karama ya Mungu kwa ajili ya kufanya uinjilisti.[2] Viongozi ni lazima wakumbuke kwamba siyo waumini wote wenye karama za kufanya uinjilisti kwa njia inayofanana. Hata hivyo, kila muumini anapaswa kujitoa kulisaidia kanisa katika kutimiza wito wake wa umisheni wa uinjilisti na anapaswa kujiandaa katika kushirikisha injili.

**Sababu za baadhi ya Wakristo kutofanya Uinjilisti**

► Je, kwa nini siyo Wakristo wote wanaofanya Uinjisti?

*Ukumbusho kwa kiongozi wa darasa: Wanafunzi watapaswa kuandika oradha sababu wanazofikiria kabla ya kuangalia orodha ifautayo hapa chini.*

- Ukosefu wa jumla wa bidii ya kiroho
- Kujisikia binafsi kutowajibika kwa ajili ya uinjilisti

[2] Waefeso 4:11

- Kutojua jinsi ya kuanzisha mahojiano ya kiroho
- Kutojua jinsi ya kuwakilisha Injili
- Hofu ya kushindwa kujibu hoja za ushindani
- Kujisikia aibu kwa kuwa tofauti na dunia
- Kuwa na hofu kwamba juhudi zake zinaweza zisiwe na matokeo mazuri
- Mateso

► Je, sababu hizi zina uzuri wowote wa kuridhisha?

## Jinsi ya Kuanza

► Je, kama mtu hafanyi lolote kwa ajili ya wokovu kwa watu waliopotea dhambini, ni nini kinachohitajika ili kumfanya aweze kuanza?

Kama amekosa bidii ya kiroho, anahitaji uamsho wa kiroho.

Kama mtu yuko hai kiroho, ni mwenye bidii, na anayetambua wajibu wake binafsi wa kushiriki katika kutekeleza Agizo Kuu la Yesu, inawezekana vipengele viwili vifuatavyo ndivyo anavyohitaji ili kumfanya aweze kuanza:

1. **Imani** – Anahitajika kutambua kile ambacho Mungu anafanya katika kuifanya injili iwe na nguvu.

2. **Maandalizi** – Anahitajika atayarishwe katika kupata mafunzo ya jinsi ya kuwasilisha injili.

► Mwanafunzi atapaswa asome Yohana 4:28-30, 39 kwa ajili ya kikundi. Je, ni nini kilichomfanikisha mwanamke Msamaria kuwaleta watu kwa Yesu?

> "Hii ilikuwa ndiyo njia ambayo kanisa lake lilikuwa lishinde – kupitia maisha ya watu waliojikabidhi kabisa katika kumjua Mkombozi kiasi kwamba Roho wake na njia yake iliwalazimisha wao kuwaeleza wengine."
> - Robert Coleman, *The Master's Plan*

Alikuwa hana mafunzo. Kilichokuwa kwake ni ile neema aliyojionea mwenyewe na kipaumbele cha kuwaeleza watu wengine kuhusu habari za Yesu.

Endapo mtu atakuwa na mambo haya mawili, uzoefu wa neema na kipaumbele cha kuwaeleza watu wengine, atakuwa anazo sifa muhimu sana za mwinjilisti. Mafunzo ni mazuri, lakini kama mtu atakosa sifa hizi mbili, hakuna mafunzo yeyote yanayoweza kumfanya mtu kuwa mwinjilisti mzuri.

### Jambo la muhimu: Unahitaji kitu gani ili uweze kuanza?

► Je, Unafanya nini sasa kwa utayari wa kuipeleka injili? Je, unaridhika na kile unachokifanya?

► Je, ni nini kitakachokusaidia wewe kushirikisha injili kwa watu wengine kwa bidii zaidi na kwa mafanikio makubwa?

## Tabia ya Mwinjilisti

Tuzungumzie kuhusu aina ya mtu ambaye amekubaliana na Agizo Kuu la Yesu.

Hata kwa muumini mpya aliyeokoka anaweza kuushirikisha ushuhuda wake na akaelezea kuhusu ukweli uliomleta hata akaokoka.

Hata hivyo, mtu anayeweza kutumiwa na Mungu kwa mafanikio ya muda mrefu kama mwinjilisti anahitaji sifa maalumu.

### (1) Kuokoka

Mwinjilisti ni lazima awe mtu ambaye ameokoka kwa sababu:

1. Anahitajika awe na ushuhuda wa kushirikisha.
2. Hawezi akaelewa kuokoka ni kitu gani kama mwenyewe hajaokoka.
3. Ni lazima awe na mabadiliko ya tabia ambayo yanaanza mara tu mtu anapookoka.

> "Tunaamimni kwamba ufunguo mkuu kwa ajili ya ushuhudiaji wa Kikristo unapatikana kwa washuhudiaji wenyewe na aina ya watu walivyo. Bila kusahau kuwa wanahitajika kuwa watu wenye imani ya Kikristo, watu wa upendo na watakatifu. Ndiyo kusema kwamba, ni lazima wawe na uzoefu binafsi unaokuwa wa nguvu ya kubadilisha ya Roho Mtakatifu, ili kwamba sura ya Yesu Kristo iweze kuonekana kwa uwazi katika mienendo na tabia zao."
> - The Laussanne Committee for World Evangelization, *The Willowbank Report*

Endapo mtu ambaye hajaongoka anafanya kazi ya kidini, haelewi anachofanya na ana nia mbaya.

### (2) Mwenye Msimamo wa Kuishi maisha ya Kikristo

Ingawaje hatupaswi kukosa nafasi ya kushirikisha injili, uinjilisti una matokeo makubwa sana wakati mtu anaposikia injili kutoka kwa mtu anayemwamini. Watu wanaokuamini sana wewe wanapaswa wawe watu wanaokufahamu vizuri zaidi. Mwinjilisti anapaswa adhihirishe maisha ya kujitolea kwa Mungu pamoja na msimamo wa utii kwa Mungu

### (3) Mwenye Kushikamana na Kanisa

Mwinjilisti anahitajika awe mfuasi aliyejikabidhi kabisa kwa kanisa kwa sababu:

1. Atahitajika aweze kuwakaribisha watu kwenye familia ya watu wa imani.
2. Atahitajika kupata msaada wa kanisa katika kuwafanya wanafunzi wale wanaookoka.
3. Atahitajika kuwajibika kiroho.
4. Atahitajika kupata msaada na kutiwa moyo na kanisa.

Ni lazima awe na uhakika na ndugu zake wa kiroho wa kiume na wa kike. Ni lazima aheshimu uongozi wa kanisa na jikumu la kanisa.

Kama atafikiri kwamba anaweza kuwa Mkristo na kufanya huduma yake bila ya kanisa, huyu haelewi kanisa ni kitu gani na haelewi maana ya mwaliko wa injili.

**(4) Mwaminifu kwenye kweli.**

Mwinjilisti ni lazima aamini kwamba Neno la Mungu ndio hazina ya ukweli inayopaswa kushirikishana. Biblia inatoa masharti ya wokovu na uhusiano na Mungu. Kamwe hatuwezi kuubadilisha ukweli ili kuufanya ujumbe wetu uwe wa kukubalika zaidi.[3]

Kutokana na Biblia, tunajua kwamba kila mtu mwisho wake aidha ataingia kwenye uzima wa milele au moto wa milele. Mwinjilisti anahamasishwa na imani hiyo.

**(5) Mwenye Kujazwa Roho Mtakatifu**

Roho Mtakatifu huutia nguvu ujumbe wa injili. Anahukumu dhambi, analeta mwamko wa kiroho, na anamfanya mwenye dhambi aweze kuwa na jibu katika imani.

Mwinjilisti anakuwa na matokeo mazuri tu pale anapokuwa anatumiwa na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, ni lazima awe mnyenyekevu kwa Mungu. Ni lazima awe mwombaji. Ni lazima aombe mwongozo kutoka kwa Mungu.

Mwinjilisti ni lazima atafute kujazwa Roho Mtakatifu. Kuna ujazo wa Roho Mtakatifu ambao unatakasa moyo na kuipa huduma nguvu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuingojea kazi hii ya Roho Mtakatifu.[4] Wanafunzi waliupokea ujazo huu wa Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste. [5]

Kuna nyakati zingine pia ambazo Mungu hutoa upako maalumu wa Roho Mtakatifu ili kumuwezesha mwinjilisti kukabiliana na chanagamoto maalumu.[6]

## Kazi za Kufanya

(1) Andika aya chache zinazoelezea jinsi ambavyo wewe umehusika binafsi katika uinjilisti na kuwafanya watu kuwa wafuasi wa Yesu kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Je, ni nini malengo yako ya baadaye? Je, ni kitu gani unachotegemea kukipata kutoka kwenye somo hili?

(2) Je, ni nini kinachofanywa na makanisa yaliyoko kwenye eneo lako katika kueneza injili? Chunguza na uliza maswali, kisha andika kurasa 2-3 za maelezo hayo.

---

[3] 1 Wakorintho 4:1-2
[4] Matendo 1:4-5
[5] Matendo 1:8, 2:4, 15:8-9
[6] Matendo 13:9-12

# Somo la 2
# Theolojia ya Kuzaliwa mara ya Pili

## Ukumbusho kwa kiongozi wa darasa

*Pamoja na nyongeza ya aya za Maandiko zitakazojadiliwa katika somo hili, Kuna aya nyingine nyingi zilizoonyeshwa kwenye tanbihi. Inawezekana kusiwepo na muda wa kutosha kwa darasa kupitia na kuzisoma aya zote wakati wa kipindi cha darasani. Kiongozi wa darasa anaweza kuchagua baadhi kwa ajili ya kusomwa.*

Neno *kuokoka* linahusika na mabadiliko yanayotokea wakati mtu anapookoka. Kusudi la uinjilisti ni kumwongoza mwenye dhambi aweze kufikia kuokoka.

► Soma 1 Wathesalonike 1. Je, kuna mabadiliko gani ya ndani kwa Wathesalonike wakati walipookoka

Ili kuelewa ni kwa nini mtu anahitajika kuokoka, na kuelewa ni nini kinachotokea wakati mtu anapookoka, ni lazima tuelewe hali ya mtenda dhambi kabla ya kuokoka.

## Hali ya Mwanadamu kabla ya kuokoka.

► Je, ni kwa jinsi gani unaweza kuielezea hali ya mwanadamu kabla hajaokoka?

Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, kila mtu ametengwa na Mungu anapokuwa amezaliwa.[7] Hii inamaanisha kwamba kila mtu ni mbinafsi na anayeenda katika njia zake kwa jinsi anavyotaka.

### Tabia Nne za Mwenye Dhambi

Mara tu mtu anapofikia umri wa kufanya maamuzi, anaanza kuteda dhambi. **Kila mwenye dhambi ana hatia kwa matendo yake mengi ya uovu.[8]**

Dhambi ni kukiuka sheria ya Mungu.[9] Kwa kuwa Mungu ni mwenye haki yote, haipuuzi dhambi, na kila mtu atahukumiwa kwa yale yote aliyoyatenda.[10] Hakuna maswali kuhusu hatia ya mtu au adhabu anayostahili. Kila mtenda dhambi tayari ni mhukumiwa.[11]

**Mtenda dhambi ni adui wa Mungu.**[12] Mwenye dhambi hawezi kuwa kwenye uhusiano na Mungu hadi hapo makosa yake yaliyo kinyume na Mungu yatakapoondolewa.

---

[7] Warumi 5:12
[8] Warumi 3:23
[9] 1 Yohana 3:4, Yakobo 2:10-11
[10] 2 Wakorintho 5:10, Ufunuo 20:12-13
[11] Yohana 3:18-19
[12] Warumi 5:10

Mtenda dhambi pia yuko katika hali inayomfanya asiwe mtu wa kufaa kwenye uhusiano na Mungu kwa sababu **ni mtenda mabaya kwa ajili ya tamaa zake**.[13] Kwa kuwa yeye ni mtumwa wa dhambi, **mwenye dhambi hana uwezo wa kuibadili hali yake**.[14]

Kwa hiyo ni nini anachohitaji mtenda dhambi? Kwa kuwa mtenda dhambi ni mwenye hatia, wokovu kwake unamaanisha ni kusamehewa. Kwa kuwa ni adui wa Mungu, wokovu kwake unamaanisha ni kupatanishwa. Kwa kuwa ni mtenda mabaya, wokovu kwake unamaanisha ni kutakaswa. Kwa kuwa hana uwezo, wokovu kwake unamaanisha ni kuwekwa huru. Hivi ni vipengele vichache tu vya wokovu ambavyo mwenye dhambi anavihitaji.

Wakati wa kuokoka, mwenye dhambi husamehewa, hupatanishwa na Mungu, hutakaswa, na huondolewa kutoka katika nguvu ya dhambi. Paulo anaelezea hali ya awali au ya nyuma ya dhambi ya waamini wa Korintho zikiwemo dhambi za kutisha. Kisha akasema, "Lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki…"[15]

## Umuhimu wa Msalaba

Hakuna mtu anayeweza kutoa malipo kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe. Dhambi ni kwenda kinyume cha Mungu wa milele. Na ubinadamu hauna chochote chenye thamani ya umilele cha kulipia.

Hakuna chochote ambacho mwanadamu angeweza akafanya kwa ajili ya hitaji lake mwenyewe; kwa hiyo, hakuna chochote ambacho mwanadamu angetakiwa kutoa kwa ajili ya wokovu.[16] Kama kungekuwa na uwezekano wa mwanadamu kufanikisha wokovu wake mwenyewe, hakungekuwepo na haja yeyote ya Yesu kufa kifo cha msalaba.[17]

► Je, kama Yesu angetaka kusamehe dhambi, kwa nini asingefanya hivyo bila ya msalaba?

Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu, ni lazima atafanya hukumu kwa mujibu wa kweli na haki.[18]

Jaribu kufikiria kama dhabihu ya Kristo haingefanyika. Je, ingekuwaje kama Mungu kirahisi tu angeamua kusamehe dhambe bila ya kuwepo kwa upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu?

Kama Mungu angesamehe dhambi bila ya kuwepo kwa upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu, ingeonekana kwamba dhambi siyo kitu hatari. Ingeonekana kwamba Mungu siyo mwenye haki na vile vile siyo mtakatifu. Ingeonekana

[13] Waefeso 2:3
[14] Warumi 5:20, 7:23
[15] 1 Wakorintho 6:11
[16] Wagalatia 3:21
[17] Wagalatia 2:21
[18] Warumi 2:5-6

kwamba mbele ya macho ya Mungu kuna tofauti ndogo sana kati ya mtu anayetenda mema na mtu anayetenda maovu.

Kama msamaha ungekuwa bila ya kuwepo kwa upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu, Mungu hangeweza kuwa anaabudiwa kama mwenye haki na mtakatifu. Msamaha bila ya kuwepo kwa upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu mwisho wake ungekuwa ni kutomheshimu Mungu badala ya kumheshimu.

Mungu ni wa upendo na anataka kusamehe. Hakutaka kuwaacha wanadamu kwenye hali ya dhambi ambayo ingekuwa ni kupotea milele, ingawaje ndio halali yao waliyokuwa wanastahili.

Dhabihu ya Yesu juu ya msalaba ilitoa dhabihu yenye thamani ya milele iliyokuwa inahitajika. Yesu alistahili **(1) kwa kutokuwa mtenda dhambi** [19] (mkamilifu na asiyehitaji wokovu wake mwenyewe), na **(2) kufanyika kwake kuwa ni Mungu na Mwanadamu kwa wakati moja.**

Upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu ulitoa kilichokuwa kinahitajika kama msingi wa msamaha. Kwa sasa, Mungu anaweza kumsamehe mtu ambaye anatubu na kuamini ahadi yake. Hakuna mtu yeyote anayeelewa kuhusu dhabihu ya msalaba anayeweza kufikiri kwamba dhambi siyo kosa kubwa mbele ya Mungu.

Upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu ulitoa njia ambayo Mungu anaweza kuichukulia kwamba ni ya haki kwa mwenye dhambi anayeamini katika ahadi yake na bado akawa mwenye haki. Warumi 3:20-26 inatoa ufafanuzi wenye mantiki wa jinsi upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu unavyofanya kazi.

Biblia inatueleza kwamba njia ya ukombozi ambayo Mungu aliitoa ndiyo njia peke yake. Kama mtu ataukataa wokovu kwa njia ya neema, hawezi akaokolewa.[20]

Hii ndiyo sababu ni muhimu kuelewa kuhusu imani ya wokovu kwa njia ya neema peke yake, inayopokelewa kwa imani peke yake. Wokovu ni kwa njia ya neema peke yake kwa sababu hakuna lolote tunaloweza kulifanya ili kupata wokovu au kustahili wokovu. Ni kwa njia ya imani tu tunayoweza kufanya katika kuufanikisha wokovu. Tunawza tu kuamini ahadi ya Mungu.

## Neema ya Kwanza

► Je, ni kitu gani kinachotangulia kwanza: Mwitikio wa mwanadamu kwa Mungu au kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu?

[19] 2 Wakorintho 5:21
[20] Marko 16:15-16, Matendo 4:12, Waebrania 2:3

Nema ya Mungu hufika hadi kwenye moyo wa mwenye dhambi, inamhukumu kuhusiana na dhambi zake na inamsababishia awe mwenye kuhitaji msamaha.[21] Mwenye dhambi hana nguvu za kuachana na dhambi zake bila ya msaada wa Mungu.[22] Mungu humpa mwenye dhambi uwezo wa kuipokea injili. Kama mtu akiwa hajaokoka, siyo kwa sababu hakuwa na hiyo neema, ila ni kwa sababu hakutaka kuipokea neema ambayo Mungu ameitoa kwake.

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu, na Mungu anamtaka kila mtu aokoke.[23] Neema ya Mungu inampa kila mwanadamu uwezo wa kukubali kupokea, lakini hamlazimishi mtu yeyote. Hiyo ndiyo sababu Mungu anamwita kila mwenye dhambi kuchagua kutubu na kuamini.[24]

## Kuelezea maana ya Toba

► Je. Toba ni nini?

Toba maana yake ni kwamba mwenye dhambi anajisikia mwenyewe ni mwenye hatia na anayestahili adhabu na kwamba yuko tayari kuachana na dhambi zake.

Aya hii kutoka katika Isaya inafafanua kuhusu toba:

> Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa.[25]

Toba haimaanishi kwamba mwenye dhambi ni lazima ayarekebishe maisha yake na ajihesabie mwenye haki mwenyewe kabla Mungu hajamsamehe. Kwa jinsi hiyo haiwezekani kwa sababu mtu kama huyo yuko kifungoni na hawezi akajifungua mwenyewe; badala yake mwenye dhambi anapaswa awe na hiari kwa ajili ya Mungu kumtoa katika dhambi zake.

► Wokovu unapokelewa kwa imani; sasa ni kwa nini toba iwe ni muhimu kwa ajili ya wokovu?

Imani ndiyo peke yake hitaji la msamaha, laini imani iliyo ya kweli ndani ya Kristo siku zote itasababisha watu kutubu dhambi zao. Kumgeukia Kristo (kuamini) na kugeuka kutoka katika dhambi (kutubu) kutatokea kwa wakati mmoja, lakini ni imani inayofanya kugeuka kutoka katika dhambi kuwe jambo linalowezekana. Hii imani yenye kuokoa ni

[21] Tito 2:11, Yohana 1:9, Warumi 1:20
[22] Yohana 6:44
[23] 2 Petro 3:9, 1 Yohana 2:2, 1 Timotheo 4:10
[24] Marko 1:15
[25] Isaya 55:7

kipawa kutoka kwa Mungu.[26] Kama mtu hayuko tayari kutubu, ni kwamba hayuko tayari kuokolewa kutoka katika dhambi.

Kama mtu hatatubu, ni kwamba hataki kukiri uovu wa dhambi. Kama hawezi kujiona ni kwa nini aachane na kutenda dhambi, basi mtu huyo hazioni dhambi zake kama kweli ni uovu. Kama hawezi kuona kwamba dhambi zake ni uovu, kwa uhakika haelewi ni kwa nini anahitaji msamaha

Kama mtu hawezi kujiona mwenyewe kwamba ni mwenye hatia, bila ya kujitafutia sababu, na anayeitaji adhabu, bado anakuwa hajatubu. Kama atakiri kwamba yeye ni mwenye dhambi lakini anahitaji kukaa na dini ambayo itamwachia mwanya wa kuendelea kutenda dhambi, bado anakuwa hajatubu kwa sababu bado anataka aendelee kufanya kile kilichomfanya awe mwenye hatia.

## Kuelezea maana ya Imani Iokoayo

► Kama mtu anayo imani iokoayo, je, inamaanisha nini kwamba ameamini?

**(1) Anajiona kwamba hawezi kufanya lolote la kuweza kujihesabia haki yeye mwenyewe**.

> Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.[27]

Anajitambua kwamba hawezi akafanya lolote (matendo) litakalomfanya astahili kuokolewa, hata kwa sehemu kidogo tu.

**(2) Anaamini kwamba dhabihu ya Kristo inatosha kwa ajili ya msamaha wake.**

> Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.[28] Kituliza hasira, kiombea msamaha

*Kipatanisho maana yake ni* kwamba dhabihu ndiyo inayofanya msamaha wetu kuwa jambo linalowezekana.

**(3) Anaamini kwamba Mungu atamsamehe yeye kwa sharti la imani peke yake.**

> Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.[29]

Ikiwa atafikiria kwamba kuna masharti mengine, maana yake kwa sehemu, anategemea kusamehewa kwa matendo yake badala ya kusamehewa kikamilifu kwa neema.

---

[26] Waefeso 2:8-9
[27] Waefeso 2:8-9
[28] 1 Yohana 2:2
[29] 1 Yohana 1:9

## Kubadilika na au Kuokoka

► Mwanafunzi atahitajika kusoma Matendo 26:16-18 kwa ajili ya kikundi. Je, aya hizi zinasema nini kuhusu huduma ya Paulo itakavyokuwa?

Huduma ya Paulo itakuwa ni kuongoza watu wafikie kuokoka. Aya ya 18 inaelezea kuhusu kuokoka. Inahususha pamoja na kugeuka kutoka katika giza na kurejea nuruni, na kutoka katika nguvu za shetani na kumrejea Mungu, kupokea msamaha, na kupokea urithi kwa wale wote ambao watatakaswa. Hayo yote yanapatikana kwa imani katika Kristo.

> "Mchungaji mwenye uadilifu hataweza kuridhika na 'maamuzi' bali na waamini ambao wanaendelea mbele kwa bidii kwenye uhusiano wao na Kristo; waamini ambao wana njaa ya Neno la Mungu, wanaotembea kwenye upendo wa Kikristo, ambao daima hushiriki kwa imani katika kifo cha Kristo na kufufuka, na wanaomba bila ya kukoma,"
> - Timothy Keep,
> "The Integrity of Biblical Evangelism and Conversion"

Kubadilika na au uokoka kutoka kuwa mwenye dhambi hadi kufanyika Mkristo kamili ni mabadiliko makubwa sana. Biblia inataja kama ni uzao mpya.[30] Mambo ya kale yamepita, na kila kitu kimekuwa kipya.

Mtu aliyeokoka huachana na masanamu na taratibu zote za kidini ambazo zina mgogoro na uaminifu kamili kwa Mungu.[31]

Mabadiliko kwa kawaida huwashangaza watu wengine.[32] Hawaelewi ni kwa jinsi gani mtu anaweza akawa na mabadiliko makubwa hivyo. Marafiki zake wa karibu na jamii yake wanaweza wakamtesa.[33]

Mtu aliyeokoka hashiriki tena na tamaa na vitu ambavyo ni vipaumbele vya kidunia. Tofauti hii ndiyo inayoonyesha shuhuda za kwamba mtu huyu ameokoka.[34] Mtu aliyeokoka anawapenda watu wengine walioamini na anatamani kuwa katika ushirika pamoja nao.[35]

Matamanio ya mtu hubadilika anapokuwa ameokoka. Bado ataendelea kuwa na majaribu, lakini anakuwa na uwezo wa kuhimili matendo ya kutenda dhambi kwa sababu hatawaliwi tena na tamaa za dhambi. Ana matamanio ya Neno la Mungu kwa sababu anakuwa ameshajionea neema ya Mungu.[36]

---

[30] 2 Wakorintho 5:17
[31] 1 Wathesalonike 1:9
[32] 1 Petro 4:3-4
[33] Mathayo 10:34-36
[34] 1 Yohana 2:15
[35] 1 Yohana 3:14
[36] 1 Petro 2:2-3

Mtu aliyeokoka anampenda Mungu na atataka ampendeze yeye. Hatazichukulia amri za Mungu kama ni ngumu na zisizopendeza.[37]

Mtu aliyeokoka huuimarisha uhusiano endelevu na Mungu, na zaidi sana katika maombi.[38]

► Kwa maneno yako mwenyewe, elezea jinsi mabadiliko yanavyotokea wakati mtu anapookoka.

## Tabia za Uzao Mpya

Biblia inasema kwamba wakati mtu anapozaliwa mara ya pili, mambo yote hufanywa kuwa mapya. Mambo mapya ni pamoja na yafuatyo:

- Asili mpya—asili ya kiroho[39]
- Bwana mpya—Kristo kupitia Roho Mtakatifu[40]
- Hamu mpya ya Neno la Mungu[41]
- Tabia mpya ya upendo[42]
- Uhusiano mpya na Mungu kama mwana au binti[43]
- Msaidizi mpya katika Roho Mtakatifu[44]
- Wakili mpya katika Yesu Kristo kama tutaangukia kwenye dhambi[45]
- Matumaini mapya ya kuishi maisha ya milele[46]

## Uhakika Binafsi wa Wokovu

► Je, sababu gani potofu ambazo zinamfanya mtu ajifiirie kwamba yeye ni Mkristo?

Mtu anaweza kujifikiria kwamba yeye ni Mkristo wa sababu zifuatazo:

- Kwamba yeye alibatizwa.
- Kwamba ni mshirika wa kanisa.
- Kwamba anaamini baadhi ya imani za Kikristo (doctrine).
- Kwamba anashika mapokeo kadhaa ya kidini.
- Kwamba anafuata msingi fulani wa matendo ya haki.
- Kwamba ana uzoefu na mambo kadhaa ya kiroho.
- Kwamba alishafanya maamuzi na ukiri wa imani.

[37] 1 Yohana 5:2-4
[38] 1 Wakorintho 1:2
[39] 2 Petro 1:4
[40] Mathayo 23:10, Warumi 8:14
[41] 1 Petro 2:2
[42] Warumi 5:5, 1 Yohana 4:7-8
[43] Yohana 1:12
[44] Yohana 14:16, Warumi 8:26-27
[45] 1 Yohana 2:1
[46] Warumi 8:12, 1 Yohana 3:2

Kwa mujibu wa Biblia, hakuna hata kipengele kimoja katika hivi vyenye uhakika wa kutosha wa kumhakikishia mtu kwamba ni Mkristo.

Biblia inatueleza kwamba tunaweza kujua kwa uhakika kwamba tumeokoka. Tunaweza kuwa na uhakika na Mungu kwamba ametukubali. Hatuna sababu ya kuishi katika hofu, kwa sababu Roho wa Mungu anatuhakikishia kwamba ametuasili kuwa wana wa Mungu.[47]

Uhakika huu umekamilika kabisa kiasi kwamba hatupaswi kuwa na hofu ya Siku ya Hukumu.[48] Baadhi ya watu wanasema kwamba wanategemea wanaweza kupokelewa mbinguni, lakini sisi tunakuwa na uhakika zaidi ya huo. Haitoshi tu kuamini kwamba wokovu unatolewa kwa mwanadamu yeyote kwa ujumla; mtu ni lazima ajijue kama yeye binafsi ameokoka.

► Je, mtu anawezaje kujua kwa uhakika kwamba ameokoka?

Baadhi ya watu wanategemea hisia zao, lakini hisia hubadilika na zinaweza zikapotosha.

Maisha yaliyobadilishwa yanatoa ushahidi kwamba mtu ameokoka, lakini ushahidi huo haupo kwa wakati huo huo wa mwanzo. Matokeo ya wokovu hayana muda wa kutokea. Kwa hiyo, maisha yaliyobadilishwa siyo msingi wa uhakika.

Mwamini anaweza akawa na uhakika wa wokovu wake kwa kujua kwamba amefuata njia za wokovu za kimaandiko. Kama mtu kweli ametubu kama Biblia inavyoelekeza, ana haki ya kuamini kwamba Mungu amemsamehe. Wakati mtu anapotubu na kuamini, Mungu humpa ushuhuda wa Roho wake kwamba sasa amefanyika kuwa mtoto wa Mungu.

Kama mtu atajaribu kujihisi kwamba yeye ameokoka wakati kiuhalisia hajawahi kutubu, atajichanganya na atakuwa anajidanganya yeye mwenyewe.

Kama mtu (1) atatubu kwa ukweli, (2) ataamini ahadi ya Mungu katika Maandiko, na (3) atapokea ushuhuda wa Roho Mtakatifu, hataweza kudanganyika. Uhakika huu uko katika msingi wa Neno la Mungu, ambalo kwa uhakika linaaminika kabisa. Mungu siku zote hutimiza ahadi zake.

### Maneno 10 yanayohusiana na Vipengele vya Wokovu.

**Upatanisho**: Neno hili linamaanisha kwamba waliokuwa maadui hapo mwanzo wamerejea kwenye amani tena. Katika wokovu, tunafanya aman na Mungu.[49]

**Kufidia kosa**: Neno hili linamaanisha kwamba kumbukumbu zimefutwa. Katika wokovu, kumbukumbu za makosa yetu zimefutwa.[50]

---

[47] Warumi 8:15-16
[48] 1 Yohana 4:17
[49] 2 Wakorintho 5:19, Warumi 5:1. (Aya hizi kwa pamoja zinaelezea kuhusu kuhesabiwa haki na upatanisho.)
[50] Waebrania 8:12

**Kipatanisho**: Neno hili linamaanisha kwamba kuna kitu kilichofanyika ili kutuliza ghadhabu ya mtu mwingine. Katika wokovu, dhabihu ya Yesu ilibadilisha kabisa ghadhabu ya Mungu iliyokuwa juu yetu.[51]

**Kuokolewa**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anaokolewa kutoka katika mikono ya mtu mwingine mwenye nguvu. Katika wokovu, tumeokolewa kuwa chini ya nguvu za Shetani na dhambi.[52]

**Kukombolewa**: Neno hili linamaanisha kwamba fidia inalipwa ili mtu aweze kuwekwa huru. Katika wokovu, kifo cha Yesu ni fidia kwa wengi ili tuweze kuwekwa huru kutoka katika kifungo na adhabu ya dhambi[53]

**Kuhesabiwa haki**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anahesabiwa kuwa mwenye haki, na asiyekuwa na hatia. Katika wokovu, mwenye dhambi ambaye ana hatia anahesabiwa kuwa mwenye haki tena kwa sababu Yesu aliteseka badala yake.[54]

**Utakaso**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anafanywa kuwa mtakatifu. Katika wokovu, mwenye dhambi anatakaswa na kufanywa mtoto mtakatifu wa Mungu.[55]

**Kuasiliwa**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anafanywa kuwa mtoto halali kisheria wa mtu mwingine. Katika wokovu, tunafanyika kuwa watoto wa Mungu.[56]

**Urejesho/Uzao Mpya**: Neno hili linamaanisha kwamba mtu anaanza tena maisha kwa upya. Katika wokovu, mwamini anaanza tena maisha mapya.[57]

**Kutiwa muhuri**: Neno hili linamaanisha kwamba kitu fulani kimefungwa kwa lakiri ili kuonyesha ni nani anayehusika nacho. Katika wokovu, Roho Mtakatifu ndani yetu anakuwa lakiri ya kututambulisha kwamba sisi ni mali ya Mungu.[58]

## Kosa la Kuepuka: Kuwa na Dini bila Toba

Kuna aina ya mtu ambaye kwa urahisi tu huwa anafikiria kwamba ameokoka anapokuwa akisikia kwamba wokovu ni kwa neema kupitia imani. Hajawahi kufanya toba ya kweli kwa sababu hakuona kama alihitaji hilo. Hakuwahi kujiona mwenyewe kwamba ni mwenye dhambi anayestahili adhabu ya Mungu. Anafikiria kwamba neema maana yake ni kufanya kwa jinsi yake anavyoona yeye mwenyewe. Kwa vile anakubali ukweli wa Ukristo, anajifikiria kwamba yeye ni Mkristo ingawaje hajawahi kufanya mabadiliko au mageuzi ya maisha yake. Kamwe hajawahi kusalimisha nia na dhamira ya mapenzi ya nafsi yake;

[51] 1 Yohana 2:2
[52] Luka 1:74; Warumi 6:6, 12-18
[53] Waefeso 1:7, Tito 2:14
[54] 2 Wakorintho 5:19, Warumi 5:1. (Aya hizi kwa pamoja zinaelezea kuhusu kuhesabiwa haki na upatanisho.)
[55] Nyaraka nyingi zimerejea kuhusu waamini kama "watu waliotakaswa" (Waefeso 1:1, Wakolosai 1:1, Wafilipi 1:1).
[56] Yohana 1:12, Warumi 8:15
[57] Waefeso 2:1, Yohana 7:38-39, Wagalatia 4:29, Yohana 3:5
[58] Waefeso 1:13

badala yake, alimkubali Mungu tu kama sehemu ya maisha yake ya kawaida na bado kwa sehemu kubwa anaishi kufuatana na mapenzi yake mwenyewe. Huu siyo mwanzo wa uhusiano na Mungu unaookoa, kutokana na maelezo ya kimaandiko.

### Kazi za Kufanya

(1) Katika somo hili tumejifunza maneno 10 yanayohusiana na vipengele vya wokovu. Elezea kwa kuandika aya chache ni vipengele gani vinavyoonekana kuwa muhimu sana kwako katika uhusiano wako na Mungu. Je, viko vingine unavyohitaji kuvifikiria zaidi?

(2) Kutokana na aina za Ukristo zinazoonekana katika nchi yako, na hususani katika mkoa wako, watu wanafikiri inamaanisha nini kuwa Mkristo? Kwenye kurasa 2-3, elezea aina mbalimbali za watu na jinsi wanavyoelezea Ukristo kwamba ni nini. Fafanua ni kitu gani kilichopotoka katika mtazamo wao kuhusu toba, imani inayofanya kazi, au imani nyingine yeyote.

# Somo la 3
# Dharura ya Uinjilisti

## Utangulizi

► Je, inawezekana mtu kuokoka bila ya kusikia injili? Je, kazi ya uinjilisti ina ulazima wowote?

Katika Maandiko tunapata huko mifano ya watu waliofikiwa na injili kwa neema ya Mungu bila ya mawasiliano yeyote kutoka Israeli au kanisa. Ayubu alikuwa mtu mwenye haki na alikataa mambo ya uovu hata kabla Musa hajatokea kuishi na kabla Maandiko hayajaandikwa. Baalam alikuwa mwenye uhusiano na Mungu, na alijulikana kama mwonaji aliyekuwa akipokea ujumbe kutoka kwa Mungu bila ya kuwa katika hali ya kupagawa. Abimeleki alifanya mambo mazuri zaidi ya haki kuliko Abrahamu, baada Abrahamu kufikiri, "yakini hapana hofu ya Mungu mahali hapa." Warumi 1:21-32 inaelezea kuhusu wapagani au makafiri waliokuwa kwenye hali ya mkengeuko wa tabia; siyo kwa sababu walikuwa hawamjui Mungu, bali kwa sababu walikataa kile ambacho walikuwa wanakijua.[59]

"Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake."[60] Agano ni sharti la uhusiano wa Mungu na mwanadamu, ambalo linahitaji upatikanaji wa neema kwa sababu watu wote wametenda dhambi. Kama mtu akimheshimu Mungu kwa ukamilifu wote, Mungu atamwonyesha njia ya kuwa kwenye uhusiano na yeye.

Biblia inasema kwamba wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, isipokuwa Yesu.[61] Hata hivyo, watu waliokuwa wameokolewa wakati wa Agano la Kale hawalijui jina la Yesu. Waliiweka imani yao kwenye ahadi ya Mungu ili kupata wokovu na msamaha, na aliwapatia kupitia kwa Yesu. Kwa hali hiyo hiyo, watu ambao hawajawahi kulisikia jina la Yesu wanaweza wakamwamini Mungu kwa ajili ya wokovu wao, anaokuwa anautoa kupitia kwa Yesu.

Kwa hiyo, inamaanisha nini kwa kusema kwamba wokovu hauwezi kupatikana kupitia kwa mtu mwingine yeyote? Inamaanisha kwamba mtu hawezi akaokolewa kupitia mpango mwingine wa ukombozi. Inamaanisha pia kwamba mtu asiyejua habari za Yesu hapaswi kumkataa yeye kwa sababu kumkataa Yesu itakuwa ni kuukataa wokovu au kutazamia njia nyingine ya ukombozi.

---

[59] Ona pia Zaburi 19 na Warumi 10:18.
[60] Zaburi 25:14
[61] Matendo 4:12

Yesu alisema, “Mtu yeyote akiyafanya mapenzi yake, ataijua kweli.” Hii ni ahadi kwamba kama mtu atamtafuta Mungu kwa uaminifu, Mungu atamjulisha analopaswa kulijua. “Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu.”[62] Roho Mtakatifu huleta nuru ya Yesu hata kwa wale watu ambao hawajawahi kusikia habari zake.

Watu wengi wamepokea maono au ufunuo mwingine ambao uliwaleta kwa Mungu hata kabla hawajasikia habari njema za injili kutoka kwa mjumbe mwanadamu. Kwa mfano, kwa wakati wa sasa Waislamu wengi wanakubali kubadilika baada ya kupokea ujumbe kutoka kwa Mungu

► Je, ulishawahi kusikia habari za mtu yeyote ambaye alipokea ujumbe maalumu kutoka kwa Mungu kabla ya kuielewa injili sawasawa?

Kwa hiyo, tunaona kwamba inawezekana kwa mtu kumpata Mungu na hata kuweza kuokoka bila ya kusikia injili kutoka kwa wajumbe wa kibinadanu. Lakini bado, Biblia inaelezea injili kama ni ujumbe ambao kila mtu kwa umuhimu wake anatakiwa kuisikia.

Kitabu cha Warumi kinaelezea umuhimu wa injili. Mtume alisema kwamba injili “ni uweza wa Mungu uletao wokovu.”[63] Alisema kwamba anawiwa na deni kwa kila mtu, ambalo ni kupeleka injili kwao.[64] Anajenga ukweli kwamba sisi tunahesabiwa haki na Mungu kwa kuamini tu ahadi yake ya kusamehe.[65]

> “Kwenye eneo kubwa la wazi la Kaskazini, nimekuwa mara nyingine nikiona wakati wa asubuhi moshi wa maelfu ya vijiji ambayo watu wake wako bila Kristo, bila Mungu, na bila ya mategemeo katika dunia.”
> - Robert Moffat

Kisha linajitokeza wazo la udharura. Anasema, “Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri?”[66] Akasema,”Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.”[67] Mungu huitumia injili kutengeneza imani iokoayo kwa wasikiaji wake. Mahubiri ya injili ni njia ya kawaida ya Mungu anayoitumia katika kuwaokoa wenye dhambi.

Kama wanaweza kuokolewa pasipokuwa na mjumbe wa kuwapelekea ujumbe wa injili, ni kwa nini uwepo wa mjumbe ni muhimu sana?

## Kwa nini Wamisionari Wanahitajika? (Sehemu ya 1)

Mmishenari Steve Hight alilijibu swali hili la *(Kwa nini Wamisionari Wanahitajika?)* kama ifuatavyo:

> Jibu rahisi ni kwamba, wakati wanadamu walipopata kuiona nuru, waliikataa. Yohana 1:9 anatupa taarifa kwamba Yesu ndiye amtiaye nuru kila mtu. Paulo

[62] Yohana 1:9
[63] Warumi 1:16
[64] Warumi 1:14
[65] Warumi 3:26, Warumi 5:1
[66] Warumi 10:14
[67] Warumi 10:17

anakiri kwamba uumbaji ulimfanya Mungu akajulikana[68] na kwamba, hata wakati ambapo wanadamu "walimjua Mungu, hawakumtukuza kama ndiye Mungu."[69] Yohana anaifanyia uchambuzi hali hiyo kama ifuatavyo: "Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru."[70] Moyo wa mwanadamu wa kupotea unapendelea giza. Kwa sababu ya moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, na una ugonjwa wa kufisha;[71] moyo wa dhambi ulikengeuka ukatoka kwa Mungu.

Kwa hiyo, wamisionari ni lazima waichukue hiyo nuru tena! Mungu atoaye fursa nyingine huwatuma wawakilishi au mabalozi wake wakiwa na mwenge wa injili uwakao "kwa ajili ya kuwarejesha kutoka gizani na kuwapeleka tena kwenye nuru."[72]

Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi wake kuhubiri injili, alisema kwamba, kama jiji lolote halitakubaliana na ujumbe wao, wayakung'ute mavumbi ya miguu yao katika eneo hilo kama ushahidi dhidi yao wakati wa hukumu. Mavumbi kutoka katika miguu yao yalikuwa ni ushahidi kwamba ujumbe wa injili uliwahi kufika katika jiji lao. Kwa wale watakaokuwa wameikataa injili, watapokea adhabu mbaya zaidi kuliko wale ambao hawajawahi kamwe kuisikia. Yesu anasema kwamba watahukumiwa adhabu kubwa na kali sana kuliko ile iliyokuwa kwa watu wa Sodoma. Hali hii inatufunulia kwamba injili inaleta faida kubwa sana kwa wale wote wanaoisikia.[73]

## Kwa nini Wamisionari Wanahitajika? (Sehemu ya 2)

Pasta Eric Himelick alilijibu swali hili la *(Kwa nini Wamisionari Wanahitajika?)* kwa ufafanuzi ufuatao:

Huwa tunatuma wamisionari kwa sababu ujumbe wa injili unawasilishwa vizuri zaidi kimahusiano. Ukweli wa injili siyo mambo ya kibinadamu yanayohusiana na Mungu, au masanduku ya imani za kidini yanayohitaji kukaguliwa; bali ukweli huo upo katika jumla ya ubinadamu wa Yesu Kristo. Wamisionari ni mabalozi kwa ajili ya Kristo, ujumbe wake, na huduma yake ya upatanisho.[74]

Wamishenari wanahitajika kwa sababu bila ya uwasilishwaji wa uhusiano wa moja kwa moja wa ujumbe wa injili, watu wengi wataangamia. Hatutaki kuamini kwamba watu wengi wanaangamia kwa ajili ya kutowajibika kwetu, lakini katika Warumi 10:13-15 ni wazi: "Tena wamsikieje pasipo mhubiri?" Ukweli wa kusikitisha ni kwamba hawataweza. Kuwapeleka na kuwapa msaada wamisionari ni jambo la

[68] Warumi 1:19-20
[69] Warumi 1:21
[70] Yohana 3:19
[71] Yeremia 17:9
[72] Matendo 26:18
[73] Marko 6:11
[74] 2 Wakorintho 5:20

lazima. Tukitegemea kwamba Mungu atatufanyia kazi ambayo alituitia tuifanye haitakuwa suluhisho. Mungu ametupa sisi Agizo Kuu; na kwa yule aliyepewa zaidi, mengi yanahitajika kutoka kwake. Tunatuma wamisionari kuitikia wito wa neema ya Mungu na kwa imani kwamba Mungu yuko kazini katika ulimwengu wake akiwaleta watu na kuwaweka kwenye moyo wake mkuu.

## Ufanisi wa Kivitendo wa Injili

Idadi ya watu duniani imekuwa zaidi ya watu bilioni saba tangu mwaka wa 2011. Zaidi ya watu 153,000 hufariki dunia kila siku, lakini idadi ya watu wa dunia bado inaongezeka kwa 220,000 kila siku. Zaidi ya watu 100 hufariki dunia kila baada ya dakika moja. Zaidi ya watu 1,000 wameshafariki dunia tangu ulipoanza kusoma somo hili. Ni watu wangapi miongoni mwa hao ambao waliwahi kuisikia injili? kabla hawajafariki?

Injili ndiyo njia nzuri ya mafanikio ambayo Mungu ameiratibu kwa ajili ya kuwaokoa watu waliopotea. Ni "nguvu ya Mungu iletayo wokovu." Tujaribu kufikiria swali hili tena: Kama mtu anaweza kuokolewa bila ya kuisikia injili, kwa nini tuwatume wamisionari? Tuyafikirie maswali mengine yanayofanana na hili. Kama mtu anaweza kuokolewa bila ya maombi yangu, kwa nini nimwombee? Kama mtu anaweza akaokolewa bila ya kuisikia injili zaidi ya mara moja, kwa nini tumwelezee tena mara nyingine? Kama mtu anaweza akaokolewa bila ya kanisa, kwa nini tuwe na makanisa? Jibu dhahiri ni "ndiyo, anaweza akaokolewa, lakini uwezekano ni mdogo sana." Hizi ndizo njia alizoratibu Mungu za kuwaokoa watu.

Neno la Mungu ni chombo kinachotumiwa na Roho Mtakatifu katika kuwaleta watenda dhambi kwa Mungu. Hata Biblia inasema kwamba watu wanazaliwa upya kutokana na Neno la Mungu.[75]

Ni kama hakuna mtu ambaye wamishenari humkuta ameokoka kabla ya kusikia injili. Ukweli kwamba Mungu ataweza kumwokoa mtu mkweli bila ya injili kunaonesha alivyo mwenye haki, lakini jambo hili haliwezi kuwa ni uthibitisho wa sisi kuzembea katika njia za kawaida alizoratibu Mungu. Kwa ujumla, wale ambao hawataweza kuisikia injili wataangamia. "Ole wangu nisipoihubiri Injili."[76]

► Soma Mathayo 9:35-38.

Yesu alikuwa na huruma sana kwa ajili ya mahitaji ya watu. Alikuwa na kazi kubwa ya kuhubiri na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina.

Yesu alihusika sana na mahitaji ya kiroho ya watu. Aliwataka watu waokoke na wamjue Mungu. Katika kifungu hiki, tunasoma kwamba Yesu alipowaona makutano, aliwahurumia kwa ajili ya mahitaji yao ya kiroho. Aliwaona kwamba walikuwa kama kondoo wasio na

[75] 1 Petro 1:23, 25
[76] 1 Wakorintho 9:16

mchungaji. Pia aliilinganisha huduma na mavuno, na alihuzunika kwamba watendakazi walikuwa wachache.

Yesu aliwapa wanafunzi wake hitaji la kuombea. Aliwaambia kwamba wamwombe Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake.

► Je, kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake waombe sala hii? Ni hakika kuwa Mungu anataka apeleke watenda kazi ikiwa tunaomba au hatuombi, si ni kweli?

Tunapokuwa tumeomba kwamba Mungu apeleke watenda kazi katika mavuno yake, tunaomba kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu. Kwa sababu ya hilo, tunajua kwamba Mungu atakwenda kujibu maombi yetu.

Kuna sababu nyingine ambayo inawalazimu waamini kuomba maombi haya. Yesu aliwataka wanafunzi wake kushirikisha huruma yake na kushiriki katika umisheni wake wa kufanya uinjilisti. Kama watakuwa wanaomba maombi haya mara kwa mara, wataanza kuwa watu wa kujali sana kuhusu mavuno. Watapendelea kushiriki katika kazi hii na kuwashawishi watu wengine kufanya hivyo pia.

Tunapaswa tuwe watu wa kupenda kujali mambo yale ambayo Yesu naye alikuwa anayajali. Tunapaswa tuombe maombi aliyowapa wanafunzi wake, ili kwamba yaweze kuleta mafanikio yale yale kwa ajili yetu.

### Hadithi Kuhusiana na Umisheni

Kundi la wamishenari lilikwenda kuhubiri katika kambi moja ya gereza. Humo gerezani mlikuwa na maelfu ya wafungwa, na wengi wao walikuwa ni wauaji na magaidi. Wamishenari walikuwa wakihubiri kwenye jukwaa la nje ndani ya gereza. Kuzunguka eneo la jukwaa, walinzi waliokuwa na silaha waliwekwa ili kuwalinda. Mwishoni mwa mahubiri ya injili, mhubiri aliuliza kama kuna mfungwa yeyote anayetaka kusogea mbele kwenye jukwaa kwa ajili ya kupokea kitabu cha Agano Jipya. Wafungwa thelathini walijitokeza mbele ili kupokea kitabu.

Wiki chache baadaye, wamisheari walilitembelea tena gereza hilo. Kabla ya huduma, askari wa magereza aliwaeleza kwamba watu wote thelathini waliochukua Agano Jipya walikuwa wameuawa na wafungwa wengine. Wamishenari walihubiri tena ujumbe wa injili, na pale mwishoni tena, wakatangaza kutoa Agano Jipya kwa yeyote atakayejitokeza mbele. Wafungwa mia tatu walijitokeza. Walikuwa wakitambua kwamba wafungwa wenzao thelathini wlikufa kwa ajili ya kuipokea injli, lakini kwa kuwa injili ilionekana kuwa na umuhimu kwao, walikuwa tayari kuhatarisha maisha yao, Walitambua thamani ya ujumbe wa injli waliokuwa wameusikia.

**Kazi za Kufanya**

(1) Andika sentensi chache katika kujibu mojawapo ya maswali haya mawili: Je, kuna fursa yeyote ya wokovu kwa mtu ambaye kamwe hajawahi kusikia ujumbe wa injili? Kwa nini tuwatume wamishenari na wainjilisti?

(2) Soma kitabu cha Yona. Jaribu kutambua udharura wa mjumbe wa injili. Mungu alikuwa anahusika na nini katika taarifa hii? Yona alikuwa anahusika na nini? Andika kurasa 1-2 za uchunguzi wako.

# Somo la 4
# Vipengele Muhimu vya Injili

## Utangulizi

*Ukumbusho kwa kiongozi wa darasa: Kwa kila kipengele cha Maandiko kilichorejelewa, ruhusu mtu mmoja asome, kisha mchukue mtu mwingine asome ufafanuzi wa kipengele. Acha nafasi kwa darasa lijadili kwa kifupi kila swali la majadiliano.*

## Vipengele Muhimu vya Injili

Vipengele vinavyofuata ni muhimu kwa injili. Inawezekana mtu kuokoka bila ya kuwa amevielewa kikamilifu. Hata hivyo, kupinga mojawapo ya kipengele chochote katika hivi kunaondoa msingi wa injili. Mtu au shirika ambalo linakataa au linapinga kipengele chochote katika hivi itasababisha kutengeneza injili nyingine, ikiwa ni pamoja na kuamini maana iliyo potofu ya wokovu.

Unaposhirikisha injili pamoja na mtu mwingine, vipengele kadhaa vitakuwa ni muhimu hasa kwa sababu ya makosa ambayo tayari anayaamini. Kwa mfano, kama anaamini kwamba wokovu unapatikana tu kupitia shirika au dini fulani, atakuwa ameamini kwamba mahitaji ya kuwa mwanachama wa shirika hilo au dini hiyo ni muhimu kwa ajili ya wokovu. Mtu huyu anahitajika ajue kwamba mtu binafsi hupokea msamaha na mwenyewe kuingia moja kwa moja kwenye uhusiano na Mungu.

**(1) Mungu alimwumba mwanadamu kwa sura yake ili Mungu aweze kuwa na uhusiano na yeye (Mwanzo 1:27, Matendo 17:24-28).**

Ukwli huu unaonyesha kusudi la maisha yetu na lengo la wokovu. Ukweli huu unapingana na dini ambazo haziamini katika Mungu mwenye sifa za kibinadamu. Ukweli huu unaonyesha tatizo halisi lililopo katika dunia; watu hawako kwenye uhusiano na Mungu.

► Je, itakuwaje kama mtu haamini kwamba Mungu anampenda?

**(2) Wanadamu wa mwanzo walitenda dhambi na kutenganishwa na Mungu (Mwanzo 3:3-6).**

Hii inaonesha asili ya dhambi na sababu kamili ya hali ya dunia ilivyo. Duniani ni mahali pa mateso na masikitiko kwa sababu ya dhambi. Bado kuna furaha na kusudi kwa sababu ya mpangilio wa Mungu, lakini dunia haiko kama vile Mungu alivyokuwa ameipangilia iwe.

► Je inakuwaje kama mtu hakuamini kwamba dhambi ndiyo tatizo halisi la ulimwengu wote?

**(3) Kila mtu anazaliwa akiwa ametengwa na Mungu na kutomtii (Warumi 3:10, 23).**

Kila mtu ni mwenye hatia kwa dhambi za kujitakia dhidi ya Mungu. Hakuna hata mtu mmoja ambaye siku zote amefanya yaliyo mema.

► Je, itakuwaje kama mtu atafikiria kwamba anaweza kujihesabia haki kwa mambo aliyoyafanya?

**(4) Kila mtenda dhambi ambaye hataki kutafuta rehema atahukumiwa na Mungu na hukumu yake itakuwa ni adhabu ya milele (Waebrania 9:27, Warumi 14:12, Ufunuo 20:12).**

Jambo hili linaonesha unyeti na umuhimu wa mtenda dhambi kwa ajili ya wokovu.

► Je, itakuwaje kama mtu hataamini kwamba kuna Mungu mwenye haki ambaye ana hasira kwa ajili ya dhambi zake?

**(5) Mtu hawezi kufanya lolote kwa ajili ya kulipia dhambi zake alizozifanya dhidi ya Mungu. (Warumi 3:20, Waefeso 2:4-9).**

Matendo mema na karama haviwezi kutumika kama ni malipo kwa ajili ya dhambi kwa sababu dhambi ni dhidi ya Mungu wa milele ambaye kila kitu tayari ni mali yake.

► Je, itakuwaje kama mtu ataamini kwamba ana uwezo wa kujifanyia msamaha mwenyewe?

**(6) Ni lazima kuwepo na msingi wa msamaha, kwa sababu dhambi ni jambo nyeti na Mungu ni mwenye haki (Warumi 3:25-26).**

Mungu huwa anapenda kusamehe; lakini, kama atasamehe pasipokuwepo na msingi, dambi itaonekana ni jambo la kawaida na Mungu ataonekana kwamba siyo mwenye haki.

► Je, kwa nini kifo cha Yesu kilikuwa ni muhimu?

**(7) Yesu, Mwana wa Mungu, aliishi maisha yasiyokuwa na dhambi na akafa kama dhabihu ili dhambi zetu ziweze kusamahewa (Yohana 3:16, Waumi 5:8-9).**

Kwa kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, dhabihu yake ina thamani ya milele na inatoa msingi wa msamaha kwa mtu yeyote katika ulimwengu huu. Kama angekuwa ni mwanadamu wa kawaida tu, dhabihu yake ingekuwa na thamani ndogo sana yenye mwisho. Damu ya Yesu inawakilisha maisha yake yaliyotolewa kwa ajili yetu. Bila ya damu yake hakungekuwepo na wokovu.[77] Kama hangekuwa ni Mungu, hangeweza kutuokoa kabisa; na, tungekuwa tunatafuta bila mafanikio, njia nyingine ya kupata wokovu.

► Je, ni kwa nini baadhi ya dini zinafikiri kwamba watu ni lazima waokolewe kwa njia ya matendo?

**(8) Yesu alifufuka kimwili kutoka katika wafu, akithibitisha utambulisho wake kama Mwana wa Mungu na akidhihirisha uwezo wake wa kutoa uzima wa milele. (Yohana 20:24-28, Ufunuo 1:18).**

Madhehebu yanayokataa kwamba Yesu hakufufuka, kwa kawaida pia yanakataa uungu wake na utoshelevu wa dhabihu yake kwa ajili ya wokovu. Kisha, wanaanzisha njia nyingine ya wokovu.

► Je, Ni mambo gani tunayoyajua kwa sababu ya Yesu kafufuka kutoka kwa wafu?

**(9) Dhabihu ya Yesu inatosha kwa ajili ya msamaha wa dhambi zote (1 Yohana 1:9, 1 Yohana 2:2).**

Kama mtu ataukataa ukweli huu, ataamini injili ya matendo. Dini nyingi zinaamini ujumbe wa jinsi ambavyo mtu anaweza kuupata wokovu kiasi fulani. Hali hii inawaweka watu kuwa chini ya utawala wa shirika la kidini linalowaambia kitu cha kufanya ili waweze kuokoka.

► Je, kwa nini watu wengine wanafikiri kwamba hawawezi kuokoka bila ya shirika lao la kidini?

**(10) Mungu husamehe kila mtu ambaye anakiri kwamba ni mwenye dhambi, anayetubu dhambi zake,na anayeamini katika ahadi ya Baba ya kusamehe. (Marko 1:15, 1 Yohana 1:9).**

Hakuna shirika lolote la kibinadamu lenye haki ya kuongeza chochote kwenye mahitaji ya wokovu au kutoa njia nyingine mbadala ya wokovu.

►Je, ni aina gani ya mtu ana haki ya kuamini kwamba ameokoka?

[77] Waebrania 9:22

**(11) Toba maana yake ni mtu kujutia dhambi zake na kutaka kwa hiari kuachana na dhambi zake. (Isaya 55:7; Ezekieli 18:30; Ezekieli 33:9-16; Mathayo 3:8).**

Toba haimaanishi kwamba ni lazima mtu ayafanye maisha yake yawe makamilifu kabla Mungu hajaweza kumkubali; ni Mungu peke yake mwenye uwezo wa kumtoa mwenye dhambi kutoka katika nguvu ya dhambi zake. Toba inamaanisha kwamba mwenye dhambi amejutia dhambi zake na kutaka kwa hiari kuachana na dhambi zake. Kama mtu hataki kuachana na dhambi zake kwa hiari yake, haiwezekani kuokoka. Kama mtu bado anaishi kwenye dhambi kwa makusudi, bado hajaokoka.

► Je, kwa nini toba ni muhimu?

**(12) Mwenye dhambi aliyetubu na kuamini hupokea msamaha wakati anapokuwa anaomba kwa Mungu na kumsihi Mungu amsamehe (Warumi 10:13, Matendo 2:21).**

Kila mtu anacho kibali cha kupokea moja kwa moja huruma ya Mungu kwa sababu ya Yesu. Hakuna taasisi au wakala ambaye ni muhimu kwa ajili ya mtu kupokea msamaha wa Mungu. Mtu hupokea msamaha wake yeye mwenyewe na kuanza uhusiano wa moja kwa moja pamoja na Mungu.

► Je, tunawezaje kujua kama mtu anaweza kufanyika kuwa Mkristo katika kipindi fulani cha muda?

### Kazi za Kufanya

(1) Katika aya chache, elezea ni kwa jinsi gani kipengele kimoja au viwili miongoni mwa hivi vilikuwa ni muhimu sana wakati wa kubadilishwa kwako.

(2) Chagua dhehebu moja au dini moja isiyokuwa ya Kikristo kwa ajili ya kufanyia utafiti. Kwenye kurasa 2-3, fafanua jinsi wanavyokataa baadhi ya vipengele muhimu vya injili. Elezea kuhusu injili potofu wanayohubiri na onyesha ni kwa jinsi gani imejikita katika imani za uongo. Fafanua ni kwa jinsi gani utaweza kuwapa ushahidi wa kibiblia kwa ajili ya ukweli.

# Somo la 5
# Dhana ya kiuinjilisti (Evangelicalism) na Kipaumbele cha Injili

## Utangulizi

► Soma Waefeso 1:4-9. Je, kuna imani gani muhimu zinazofundishwa katika kifungu hiki?

## Kuelezea Dhana ya kiuinjilisti

Kanisa la Kiinjili ni kanisa ambalo hufundisha injili ya kimaandiko kuhusiana na wokovu kwa neema peke yake na kwa kupitia imani peke yake. Hakuna matendo yeyote mema ya kibinadamu yaliyoongezwa kwenye upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Kristo ambayo yanaweza kutusaidia sisi kustahili wokovu.

Kutangaza injili ya kweli ni kipaumbele cha kwanza cha kanisa la kiinjili kwa sababu watu ambao huiamini injili wanajua kwamba ni jambo muhimu zaidi kuliko kitu kingine chochote.

Injili ni hazina maalumu iliyokabidhiwa kwa kanisa na Mungu kwa minajili ya kuushirikisha ulimwengu.

Kuna tabia ambazo zinafanana baina ya makanisa mengi ya kiinjili. Tabia hizi zimeorodheshwa katia aya chache zifuatazo.

**(1) Watu wa injili huamini katika mamlaka kamili ya Biblia.** Kukataa mamlaka kamili ya Biblia ni kuifanya injili iwe ya hoja nyingi.

**(2) Watu wa injili (evangelicals) huamini katika historia, na imani za msingi za Ukristo.** Kuzikataa imani hizi ni kukinzana na injili. Kwa mfano, madhehebu yanayokataa uungu wa Yesu yanakataa pia kwamba kazi ya upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Kristo siyo toshelevu kwa ajili ya wokovu na badala yake hufundisha injili ya matendo.

**(3) Makanisa ya Kiinjili husisitiza uzoefu binafsi wa kiroho.** Tabia hii ipo kwa sababu wanaamini katika mabadiliko ya mtu binafsi na imani thabiti. Kwa sababu ya kuamini huku, watu wa injili husisitiza uinjilisti kwa watu wasioamini na mabadiliko ya kiroho kwa walioamini.

► Je, kanisa lako linaelezaje kuhusu tabia hizi? Je, kunazo tabia nyingine zinazoonyesha kwamba injili ni kipaumbele?

## Kiini cha Injili

Injili ndio iipayo kanisa dira ya umisheni. Kanisa ambalo kwake injili siyo kipaumbele cha kwanza limesahau kazi ya umisheni iliyotolewa na Mungu.

Tumejifunza kuhusu agizo Kuu la Kristo lililotolewa katika Mathayo 28:18-20. Ni nini msingi mkuu wa umisheni wa kanisa?

> "Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Kristo Bwana na umisheni wa kanisa kwa ajili ya dunia. Hii inajitokeza wazi wazi katika maelezo ya Mathayo kuhusiana na Agizo kuu la Kristo. Liko dhahiri kwa sababu mamlaka yote mbinguni na duniani yametolewa na Mungu Baba kwa Mwanae kwamba kanisa lina wajibu wa kuwafanya mataifa wote kuwa wanafunzi wake."
> - J. Herbert Kane, "The Work of Evangelism"

Injili hutengeneza kanisa mahali popote inapohubiriwa. Kanisa la kweli kwa mujibu wa historia hupatikana mahali ambapo injili inahubiriwa. Urithi wa kanisa tangu wakati wa mitume hauko kwenye uendelezaji wa taasisi, bali katika uendelezaji wa kuhubiri injili kwa imani.

Taasisi zozote zilizoanzishwa na kanisa zinapaswa zihudumu kwenye kipaumbele cha injili. Kwa mfano, ratiba ya kufundisha wachungaji inapaswa iendane na kuwaandaa katika kuliongoza kanisa kwenye kutimiza umisheni wake kwa ajili ya uinjilisti na ufuasi.

Taasisi zina tabia ya kujitengeneza zenyewe ziendelee kuwepo na kusahau umisheni wao wa asili. Msisitizo mpya unavyozidi kufanywa kwa ajili ya injili siku zote kunasababisha kufanyika kwa mabadiliko mapya kwenye taasisi.

Kanisa hukuza taratibu za imani, aina za kuabudu, maisha ya Kikristo na sera ya kanisa; lakini msisitizo mpya unavyozidi kufanywa kwa ajili ya injili kunasababisha kufanyika kwa mabadiliko ya taratibu husika.

## Mifano ya Kupoteza Kipaumbele cha Injili

### Mfano 1

Wakati kanisa linafanya kazi ya kutimiza umisheni wa uinjlisti, ni muhimu kutengeneza mipango, kuandaa timu za kazi, kutengeneza ratiba mbalimbali na kutafuta misaada. Kanisa linaanzisha taasisi za kutumika kwa makusudi ya kuwajibika kivitendo. Mara nyingi, taasisi huundwa wakati wa uamsho wa kiroho wakati watu wanapokuwa wamejikabidhi kutumika kabisa, na kanisa linakuwa limehamasika katika kutimiza umisheni wake.

Uwepo wa taasisi ni muhimu. Taasisi kimsingi ni muundo wa muda mrefu wa watu na rasilimali. Bila kuwepo kwa taasisi, hakutakuwepo na majengo ya makanisa, hakutakuwepo na huduma za nje za kimataifa, hakutakuwepo na uchapishaji wa Biblia au aina nyingine za Maandiko mbalimbali, hakutakwepo na mashule ya Kikristo au ratiba za mafunzo ya elimu, na hakutakuwepo na msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma. Hata kanisa la mahali pamoja ni taasisi ambayo haipo hadi kikundi cha watu kitakapojitolea kuwepo kwa ajili yake.

Endapo taasisi itafanikiwa, inaweza kuwa kubwa, kwa wingi wa watu na bajeti kubwa. Kuhakikisha taasisi inaendelea kuwepo kunahitaji nguvu nyingi na gharama za matumizi. Mara nyingine watu wanaofanya kazi kwenye taasisi huanza kujisisikia kwamba jukumu la kuijenga hiyo taasisi ni kipaumbele cha kwanza. Wanafikiri kazi yao ni kuiwezesha taasisi izidi kuendelea kuliko kutimiza lengo la awali la umisheni la taasisi.

Ingawaje uwepo wa taasisi ni muhimu, ni lazima mara kwa mara zifanyiwe tathmini na mabadiliko kutokana na kipaumbele cha injili.

**Mfano 2**

Kwa kuwa huduma ina uwezekano mkubwa wa kuingiza fedha, baadhi ya watu wameanzisha huduma kama biashara. Siyo vibaya kwa huduma kuuza vitu kwa ajili ya kusaidia gharama za uendeshaji, na pia siyo vibaya kwa huduma kuangalia vianzo vingine vya msaada wa kifedha. Hata hivyo, kama mtu anavutiwa zaidi na mapato ya fedha kuliko kipaumbele cha injili, kusudio la moyo wake limepotoka na kazi yake haimpendezi Mungu.[78]

Simoni alikuwa mtu aliyekuwa anataka apate karama ya kiroho ili aweze kuwa mtu mkubwa mwenye hadhi na faida ya kifedha, lakini mtume alimwambia kwamba moyo wake umepotoka.[79]

► Je, kuna kitu gani potofu katika hali ya mchungaji anayejaribu kuliuza kanisa lake? Je, kuna kitu gani potofu katika ufahamu wake kuhusu kanisa ni nini?

**Mfano 3**

Hii ni mchanganyiko wa Ukristo na imani zinazojichanganya na mapokeo kutoka katika dini nyingine. Mfano wake katika nyakati za Agano Jipya ni dini ya Kisamaria. Wageni waliokuwa wakiabudu sanamu waliingia katika taifa la Israeli wakachanganya dini ya wana wa Israeli na sanamu; Yesu akasema kwamba hawajui walichokuwa wanakiabudu.[80]

Mfano, mwingine ni kutoka katika historia ya Haiti. Wakati nchi ya Haiti ilipokuwa koloni la Mfaransa, watumwa kutoka Afrika walitakiwa kuwa wakristo. Walichanganya dini zao za awali na Ukatoliki. Watu wengi wa Haiti hadi leo wanashiriki Voodoo, ambayo ni ibada ya maroho, lakini wakitumia alama za Ukristo na majina ya watakatifu wa kikristo.

Mara nyingine mchanganyo huu wa imani hutokea kwa sababu Ukristo uliambatana na taifa lililokuwa linamilikiwa na taifa lingine. Watu walikuwa wanataka kuliridhisha taifa lililokuwa chini ya umiliki wao, kwa hiyo walikubaliana na mila zao za kidini lakini wakizilinda imani zao za mwanzo.

► Je, umeshawahi kuona mifano gani ya michanganyiko kati ya Ukristo na dini nyingine?

---

[78] 1 Petro 5:1-2, 2 Petro 2:3
[79] Matendo 8:18-23
[80] Yohana 4:22

Malengo ya kidunia yanaweza kusababisha kuwepo na michanganyo Kama watu watafikiri kwamba kuikubali injili kutawaletea mafanikio ya kifedha, ushawishi wa kisiasa, au upendeleo kutoka kwa watu wenye ushawishi, wanaweza kukubaliana na mwonekano wowote wa Ukristo bila hata ya kuwa wamebadilika kiukweli. Kisha wataendelea kufuata imani zao za zamani na mapokeo yao lakini wakiziita kwa maneno ya Kikristo. Inakuwa ni vizuri zaidi wakati kanisa linapofanya uinjilisti lisitoe vitu ambavyo vinaweza kusababisha watu wakavipokea kwa malengo potofu.

Ukristo unaonekana kama ni dini ya kigeni wakati injili ilipoletwa na wamishenari wa kigeni. Hata hivyo, ni muhimu kwa Ukristo kuingizwa katika kila mila na kuchukua nafasi ya aina ile iliyoko katika mila hiyo. Haipaswi kuonekana kama ni dini ya kigeni. Hata hivyo, ni muhimu kwa wamishenari na wainjilisti kutambua kuna nini kwa kina kwenye mila ambayo haiwezi kuingiliana na Ukristo. Utambuzi huu ni mchakato ambao ni lazima upate msaada wa Wakrirsto wenyeji na hauwezi kumalizika kwa haraka.

**Mfano 4**

Mara nyingine dini hufikiriwa kama ni dini iliyoanzishwa kwa ajili ya taifa. Kwa mfano, kwenye baadhi ya mataifa, watu wengi ni Waislamu. Kwenye mataifa mengine, watu wengi wanajinasibu wenyewe kwamba ni Wakatoliki. Watu wengi hawafuati kwa ukweli kabisa viwango vya uadilifu vya dini yao na mara chache sana hutendea kazi mila zo za kidini; lakini wanasema kwamba wao ni wafuasi wa dini hiyo.

Watu wengi wanajiita Wakristo kwa sababu katika mitazamo yao katika jamii watu wote wazuri wanachukuliwa kama ni Wakristo. Kiuhalisia huwa hawajatubu. Wanafuata viwango vyao wenyewe vya uadilifu.

Injili ni wito wa kufikia kwenye toba na kujikabidhi kabisa kwa Kristo. Yesu alisema kwamba mtu hawezi akawa mwanafunzi wake hadi awe amejikana mwenyewe na awe mfuasi wake wa kweli.[81]

Tafsiri ya kuwa Mkristo haiwezi ikafanywa kwa kupendwa katika jamii ya watenda dhambi. Hali ya kawaida ya uadilifu ya jamii siku zote iko chini ya kiwango cha uadilifu cha Ukristo, na Mkristo anahitilafiana kabisa na dunia.

► Je, ni kwa jinsi gani Ukristo unaopendwa bila toba mara nyingi unaonekana mara nying katika jamii yako?

**Mfano 5**

Hatuwezi tukategemea kuona kwamba Wakristo wote wakubaliane katika imani zote. Kuna tofauti miongoni mwa Wakristo, ingawaje wanakubaliana na Biblia kama mamlaka yao kwa ajili ya imani.

---

[81] Luka 9:23

Mara nyingine makanisa huwekea mkazo zaidi kwenye imani ambazo zinawatofautisha wao na makanisa mengine, lakini imani hizo siyo muhimu kama imani za msingi za Ukristo. Kanisa haliwezi likasema kwamba makanisa mengine siyo ya Wakristo wa kweli, kama makanisa hayo yanafundisha injili ya msingi.

Kanisa halipaswi kuanzisha utambulisho wake wenyewe kwa kupigana na makanisa mengine. Linapaswa lijitambulishe kwanza kwa njia ya injili, kisha kwa kujenga ushirika wa kikundi cha watu waliojikabidhi kabisa.

► Je, ni kwa misingi gani kanisa linapaswa likubali kanisa lingine kuwa ni la kweli la Kikristo?

**Mfano 6**

Hata imani ya ukweli inaweza ikawekewa msisitizo sana kiasi kwamba ikaonekana kuhitilafiana na ukweli mwingine. Kwa kuwekea msisitizo wa rehema, kanisa linaweza kuonekana likipunguza kiwango cha uhitaji wa utii kwa Mungu. Kwa kuwekea msisitizo katika kusaidia na kuombea watu kuokoka kunaweza kufanya kusahau mchakato wa kufanya wafuasi. Wakati wa kuweka msisitizo wa uaminifu wa Mungu kwa mtu aliyerudi nyuma kiimani, kanisa linaweza likashindwa kuonya kuhusu hatari ya kuasi imani. Wakati wa kuheshimu karama za kiroho, kanisa linaweza kupuuza undani wa mambo ya kiroho na tabia ya Mkristo.

Hitilafu ya Imani hujitokeza kwa muda fulani na inakuwa na athari za muda mrefu. Fundisho lolote ambalo (1) linasababisha kutoonesha kujali kuhusu suala la dhambi, (2) linapoteza uhakika wa wokovu, (3) linaloongeza ugumu wa ziada katika njia ambayo mtu angeweza kukubaliana na injili, au (4) linaficha usahihi wa injili, hiyo ndio hitilafu ya imani.

## Uamsho wa kihistoria na Matengenezo ya Kanisa

Wakati mwingine katika historia ya kanisa injili ilionekana kusahauliwa na taasisi zilizokuwa maarufu. Makosa yaliyokuwepo kama ya kujiimarisha zaidi kwa taasisi, michanganyo, na hitilafu ya imani kulijidhihirisha wazi zaidi kuliko injili. Viongozi walipaswa kuwa mifano ya viongozi wa kiroho, lakini walionekana kuwa wanaoonyesha mtazamo potofu, tabia potofu na kupenda sana mambo ya kidunia.

Mara nyingine Mungu amekuwa akituma uamsho mkubwa sana kwa kanisa. Uamsho wenye matokeo mapana na ya muda mrefu uko katika vipengele vitatu.

1. Kunakuwepo na matengenezo ya kitheolojia, wakati ukweli wa kiroho uliopuuzwa unaporejeshwa tena kwa upya.
2. Kunakuwepo na uhuishwaji mpya wa kiroho, pamoja na maombi kwa wingi, kuabudu kwa hamasa kali, na mabadiliko ya watu kwa wingi.

3. Kunakuwepo na mbinu mpya za huduma, wakati kanisa linapata njia mpya za kufanya uinjilisti na uanafunzi.

Matengenezo ya Kiprotestanti (yaliyofanyika katika Bara lote la Ulaya katika miaka ya 1500) yalikuwa ni kufufua upya injili ya wokovu kwa njia ya neema peke yake na kwa imani peke yake. Maelfu ya watu walibadilika. Maandiko yalitafsiriwa katika lugha mbalimbali na kutawanywa katika maeneo yote husika.

Waanabaptisti (katika Bara lote la Ulaya kwenye miaka ya 1500 na baadaye) walikuwa watu waliohusika sana kwa sababu wafuasi wengi wakati wa matengenezo walidhania kwamba kuamini imani sahihi kulikuwa kunatosha kwa ajili ya wokovu. Watu wengi walikiri kuupokea ukweli wa injili lakini walikuwa hawajawahi kupata uzoefu wa mabadiliko. Wanabaptisti walisisitiza kuhusu mabadiliko ya mtu binafsi.

Watu waliokuwa na uchaji wa Mungu (mwishoni mwa miaka ya 1600 nchini Ujerumani) walikuwa watu waliotambua umuhimu wa kufanya ufuasi. Walianzisha vikundi vidogo vya huduma na mifumo ya kufundisha waamini kwa ajili ya ukuaji wa Mkristo.

Uamsho wa Wamethodisti (mwishoni mwa miaka ya 1700 nchini Uingereza) kulianza na huduma ya John Wesley. Wengi wa makasisi wa Kanisa la Uingereza walipinga kuwepo kwa uwezekano wa uhakika wa wokovu kwa mtu binafsi. Wesley alihubiri kwamba kila mtu anaweza akajijua kwamba anayo imani iliyo hai ndani ya Kristo na uhakika wa wokovu kutoka kwa Roho Mtakatifu.

► Je, ni ukweli gani mkubwa unaohitaji kuwekea msisitizo katika jamii yako?

## Hitimisho

Taasisi nyingi za Kikristo, ndogo na kubwa (ikiwa na pamoja na makanisa ya mahali pamoja), yalianza na kujihusisha katika kipaumbele cha injili. Baada ya muda mrefu, mengi ya makanisa hayo yalibadilika na kugeuka kutoka katika kipaumbele hicho.

Ili kufufua upya ufanisi wa kanisa, hatuhitaji imani mpya za ajabu au mafunuo mapya. Tunachohitaji ni urejeshwaji wa kanuni ya kiinjili ya kipaumbele cha injili.

## Mtihani

Utaanza kipindi cha darasa kitakachofuata kwa kufanya mtihani unaohusiana na somo la 5. Jifunze maswali ya mtihani kwa uangalifu kwa ajili ya maandalizi.

(1) Je, kuna tabia ngapi tatu za makanisa ya kiinjili?

(2) Je, kuna njia ngapi sita ambazo kanisa linaweza kupoteza kipaumbele cha injili?

(3) Je, kuna ishara ngapi nne kwamba imani ina hitilafu?

(4) Je, ni mambo gani matatu ya uamsho wa muda mrefu?

(5) Andika taarifa ya ukweli kuhusiana na kila kimoja kinachofuata hapa:

- Matengenezo ya Kiprotestanti
- Waanabaptisti
- Watu waliokuwa na uchaji wa Mungu.
- Uamsho wa Wamethodisti

# Somo la 6
# Kazi ya Roho Mtakatifu

## Ukumbusho kwa mwalimu wa darasa

*Wape wanafunzi wafanye mtihani uliooneshwa kwenye somo lililopita. Wanafunzi wanatakiwa waandike majibu yao kutoka katika kumbukumbu zao tu bila ya kunukuu kutoka mahali popote au mtu kuzungumza na mwenzake.*

## Utegemezi wa Roho Mtakatifu

Wakati tunapofanya kila linalowezekana katika kupokea mafunzo ya huduma na njia za kujifunza, kuna hatari ya kutaka kutegemea uwezo wa kibinadamu kwa ajili ya huduma. Lakini, kama Mtume Paulo alivyosema, "Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu."[82]

Paulo alisema kwamba hakuwa anafundisha kwa hekima za kibinadamu au kwa kutegemea ushawishi wa kibinadamu; lakini alitumainia kwenye udhihirisho wa Roho Mtakatifu ili kwamba imani ya msikilizaji wake isiweze kutegemea kwenye hekima za kibinadamu, bali hekima za Mungu.[83] Paulo alikuwa mwanazuoni, lakini hakutegemea ufahamu na ujuzi wake katika kutengeneza matokeo ya kiroho.

Akiandika kwa Wathesalonike, Paulo alisema, "Injili yetu haikuwafikia katika maneno tu, bali na katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu, na uthibitifu mwingi."[84] Waliridhishwa na injili kwa sababu ya nguvu ya Mungu.

Yesu aliwaahidi mitume kwamba Roho Mtakatifu atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. "[85] Yesu alisema kwamba, hakuna watu wanaoweza kuja kwake, wasipovutwa na Baba.[86]

## Vipengele vichache vinavyohusiana na Kazi za Roho Mtakatifu

- Anamwona na hatia mwenye dhambi.[87]
- Anambadilisha mwenye dhambi aliyeonekana ana hatia.[88]
- Anamhifadhi mtakatifu aliyebadilishwa.[89]
- Humweka kazini mtakatifu aliyepatiwa hifadhi.[90]

[82] 2 Wakorintho 3:5
[83] 1 Wakorintho 2:4-5
[84] 1 Wathesalonike 1:5
[85] Yohana 16:8
[86] Yohana 6:44
[87] Yohana 16:8
[88] Yohana 3:5
[89] Waefeso 1:13, Waefeso 4:30

- Humpa uwezo mtakatifu aliyeingizwa kazini.[91]
- Anamfundisha mtakatifu aliyepewa uwezo.[92]
- Anamwongoza mtakatifu aliyepewa mafunzo.[93]
- Anatawala matendo ya matamanio ya mwili ya mtakatifu anayeongozwa na yeye na kwa jinsi hiyo anamfanya kuwa mwenye haki.[94]

► Je, ni kwa jinsi gani utegemezi wa Roho Mtakatifu unatuongoza sisi katika njia yetu ya kufikia kwenye uinjilisti? Ni mambo gani tunayafanya tofauti kwa sababu tunamtegemea Roho Mtakatifu?

## Thamani ya Mafunzo

► Je, tufikirie nini kuhusiana na mafunzo na mbinu za uinjilisti?

Tumeitwa ili kuwakilisha ukweli wa Mungu. Tunatakiwa tuwasilishe katika njia ambayo ni nzuri sana ili tuweze kueleweka.

Hatupaswi kufikiria kwamba kwa kuwa sisi ni tegemezi kwa Roho Mtakatifu hatupaswi tena kuendeleza uwezo wetu kwa njia ya mafunzo.

Paulo alisema alijaribu kuwashawishi watu.[95] Alimwagiza Timotheo kujifunza ili awe na uwezo wa kuwasilisha ukweli wa Mungu kwa usahihi.[96] Mojawapo ya sifa za askofu ni kwamba ana uwezo wa kufundisha.[97]

Apolo alikuwa na ufanisi mkubwa sana kama mwinjilisti. Anaelezwa kuwa ni mtu aliyekuwa na ushawishi mkubwa, alikuwa hodari katika Maandiko, na mwenye roho iliyokuwa ikiwaka kwa hamasa.[98] Uwezo wake wa asili, ukichanganya na karama za kiroho, zilimfanya awe mtu aliyekuwa wa baraka sana.

Mtume Petro anatuambia kwamba tuwe tayari siku zote kumjibu kila mtu aulizaye habari za tumaini lililo katika injili.[99]

Maandiko haya yanatueleza kwamba Mungu atabariki na kutumia uwezo wetu wa asili pamoja na mafunzo kama tutakuwa tumejitolea kabisa kwa ajili ya kusudi lake. Anatuita tuzitoe nguvu zetu na uwezo wetu kwa ajili ya kazi yake.

---

[90] Matendo 13:2, 4
[91] Matendo 1:8
[92] Yohana 14:26; Yohana 16:13; 1 Yohana 2:27
[93] Yohana 16:3, Matendo 8:29
[94] Warumi 8:13
[95] 2 Wakorintho 5:11
[96] 2 Timotheo 2:15
[97] 2 Timotheo 2:24
[98] Matendo 18:25-26
[99] 1 Petro 3:15

## Kujazwa Roho Mtakatifu

Katika Matendo 1:4-5, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kungojea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao aliuita "Ahadi kutoka kwa Baba." Tukio hili litajumuisha pamoja na ujazo wa nguvu za kustahimili zitakazowafanya wawe mashahidi wa ulimwengu wote.[100]

Ingawaje wanafunzi walikuwa wameokoka, walikuwa na hitaji la ndani ambalo lilikuwa ni lazima lipatikane kabla ya kuwa tayari kwa ajili ya huduma bila ya uongozi wa kimwili wa kuonekana wa Yesu. Hata miaka mitatu ya mafunzo chini ya Mwalimu mkuu Yesu haikuweza kuwakamilisha kabisa kwa ajili ya huduma, hivyo, hitaji hili la ndani bado lilikuwa limesalia. Kabla hawajaweza kuwa na huduma iliyopewa nguvu na kuongozwa na Roho Mtakatifu, kama vile Mugu alivyopanga, walihitajika kuwa na hitaji maalumu ndani ya moyo kutokana na kazi maalumu ya Roho Mtakatifu.

> "Kulichukua jukumu hili kubwa kabisa ambalo Bwana alikuwa analikabidhi mikononi mwao lilikuwa juu ya uwezo wa nguvu za mwanadamu. Kwa hiyo, aliwapa nyenzo isiyokuwa na kikomo ya Roho Mtakatifu. Alikuwa aushawishi ulimwengu kwa ajili ya dhambi, haki na hukumu; kwa hiyo, aliambatana nao kwenye huduma yao kwa uimara wa nguvu na matokeo ya kushangaza."
> - A.B. Simpson, *Missionary Messages*

Tatizo lilikuwa limejidhirisha lenyewe kwenye nyakati tofauti wakati wa miaka mitatu ya mafunzo. Mara nyingine katika tabia walikuwa watu wa kutaka kulipa kisasi *(au wasiotaka kusamehe)* kama walivyotaka waite moto ushuke juu ya watu waliokuwa wanawakataa.[101] Mara nyingine walijivunia kuwa katika kikundi cha mtazamo wa dini fulani tu, kama vile walivyomnyima mtu mmoja kuhudumu kwa vile tu alikuwa hajapata kibali kutoka kwao.[102] Walikuwa wabinafsi na wakijivunia matamanio yao, kama vile wanafunzi wawili walivyoomba wapewe nafasi za juu na wakakasirikiwa na wenzao.[103]

Walikuwa wakibishana wao kwa wao, ni nani aliye mkubwa.[104] Ukweli ni kwamba walikuwa wameaibishwa na jambo hilo wakati Yesu alipouliza jambo lilelile walilokuwa wanalijadili, na walikuwa na ufahamu moyoni kwamba makusudio yao yalipaswa yawe mazuri zaidi.

Kwenye chakula cha mwisho cha pamoja, Yesu aliwatawadha miguu wanafunzi wake na kuwataka wawe na tabia hiyo hiyo ya utumishi kama yeye alivyokuwa akiwadhihirishia.[105] Walikuwa bado hawajaweza kuwa na aina hii ya unyenyekevu; walikuwa wamekataa kuhudumiana siku hiyo jioni. Tatizo halikuwa ukosefu wa ufahamu, bali walijawa na majivuno na kiburi.

---

[100] Matendo 1:8
[101] Luka 9:54-55
[102] Marko 9:38
[103] Marko 10:35-41
[104] Marko 9:33-34
[105] Yohana 13:14

Yesu aliwaambia kwamba wanapaswa wawe na upendo utakaokuwa na nguvu za kutosha ili kuweza kutoa maisha yao kwa ajili ya wengine.[106] Walikuwa wakijidhania kwamba wanao upendo huu, lakini haikuwa hivyo; kwa kuwa walikimbia wakati Yesu alipokamatwa, ingawaje walikuwa wamedai kwamba watakuwa tayari kufa pamoja naye.[107]

Hawa ni watu ambao walitegemewa kuwa na jukumu la kuongoza na kuliongeza kanisa bila ya uwepo wa Kristo pamoja nao kimwili. Yesu alitambua kwamba hawakuwa tayari kwa ajili ya huduma hii hadi hapo hitaji lao la ndani litakapokamilishwa, kwa hiyo aliwapa maagizo ya kusubiri Yerusalemu hadi watakapoipokea "Ahadi ya Baba."[108] Ahadi hii inatambuliwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ilikuwa ni muhimu sana kwamba hawakutakiwa kuondoka na kwenda kuanzisha kanisa bila ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Hakuwaambia kwamba walichokuwa wanatakiwa wawe nacho ni mafunzo zaidi, au mchakato wa ukuaji wa muda mrefu. Walitakiwa tu wasubiri Yerusalemu kwa ajili ya tukio la kiroho/kufikia kilele cha ahadi.

Kile walichokutana nacho wanafunzi kwenye siku ya Pentekoste kinaelezewa kuwa ni ujazo wa Roho Mtakatifu.[109] Ingawaje mambo mengi yalitokea wakati wa tukio hilo, baadaye Petro alidhihirisha kwamba kazi muhimu ya Roho Mtakatifu ilikuwa ni kutakasa mioyo yao.[110] Hili ndilo lililokuwa hitaji la wanafunzi. Ushahidi wote wa hitaji lao la ndani lilionyesha kuwepo kwa tatizo katika moyo, uharibifu wa tabia uliorithiwa, ambao walihitajika watakaswe. Wakati utakaso huu ulipofanyika kwa ubatizo (ujazo) wa Roho Mtakatifu, hawakufikiria tena kuhusu usalama wao wenyewe au madaraka kuwa kama ndio lengo lao kuu.

Tukio la wakati wa Pentekoste, lilizindua kanisa kwenye enzi ya uinjilisti wa nguvu. Kwa furaha na kwa ushindi mkubwa kanisa lilisonga mbele pamoja na kuwepo kutokukubaliana kwa mambo mengine ya imani, majungu ya Wayahudi, malalamiko ya ndani, unafiki, uwepo wa nguvu za giza, mateso, na mazingira mengi magumu.

> Walikuwa watu walioungana pamoja, timu ya mashahidi wenye nguvu ya upako:
> Kufuatia mwito wa Mungu, wakitegemea nguvu za Mungu, na wakifanya kazi kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

**Mwamini anaweza akawa na hitaji linalofanana na lile la wanafunzi walilokuwa nalo. Hitaji hili linaweza kuondoka kwa kujazwa na Roho Mtakatifu.**

---

106 Yohana 15:12-13
107 Marko 14:31, 50
108 Matendo 1:4-5
109 Matendo 2:4
110 Matendo 15:8-9

Hii haina maana kusema:

1. Kwamba mwamini huwa hana Roho Mtakatifu hadi apokee huu ujazo maalumu.
2. Kwamba hakuna kazi za Roho Mtakatifu zinazoendelea ndani ya mwamini hadi huu ujazo wa Roho Mtakatifu utakapotokea.
3. Kwamba hakuna aina nyingine ya ujazo wa Roho Mtakatifu zaidi ya huu ambao hutakasa moyo.
4. Kwamba kila mtu ambaye amejazwa nguvu za Roho Mtakatifu atakuwa na huduma ya kitume.

Hatupaswi kuwa na dhana kwamba uzoefu wetu utakuwa sawasawa na ule wa wanafunzi. Hata hivyo, uhitaji wa utakaso wa moyo na uwezeshwaji wa nguvu kwa ajili ya huduma bado ni jambo muhimu sana kwetu.

Kutokana na mfano wa wanafunzi tunaweza kuona:

1. Kwamba kama mtu analo hitaji hili, hayuko tayari kikamilifu kwa ajili ya huduma au kuishi maisha matakatifu.
2. Kwamba Mungu hapendi amwache mtu katika hali hii.
3. Kwamba suluhisho siyo mafunzo au muda mrefu wa kukua kiroho.
4. Kwamba inawezakana hitaji hili likawezeshwa kwa kitambo, baada ya kutafuta kwa uhakika.

Je, inawezekanaje kwa mwamini kupokea kazi hii ya Roho Mtakatifu?

Petro alisema ilipokelewa kwa imani.[111] Yesu aliwaandaa wanafunzi wake kuwa na imani kwa kuwapa ahadi na kuwapa matarajio.

Kwa hiyo, kama mtu ataona hitaji lake na akaona utayari wa Mungu katika kulitimiza, anaweza kuipokea neema hii kwa Imani.

[111] Matendo 15:8-9

## Kazi ya Kufanya

Kila mwanafunzi ajitathmini mwenyewe kwa maombi na ajibu maswali haya kwa maandishi. Karatasi ya majibu haitahitajika iwasilishwe kwa kiongozi wa darasa.

- Je, mimi ni tegemezi kwa Roho Mtakatifu, au ninatumainia kufanya tu yale ambayo uwezo wangu unaruhusu?
- Je, ninazo baadhi ya tabia zilizoonyesha kwamba wanafunzi walihitaji ujazo wa nguvu za Roho Mtakatifu?
- Je, kunayo matendo yoyote, tabia, mwenendo au malengo ambayo sijayasalimisha kwa Mungu?
- Je, niko tayari kwa uamuzi wangu mwenyewe Roho Mtakatifu anitakase kabisa, ili niweze kutumiwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu?

# Somo la 7
# Maombi na Kufunga

## Utangulizi

> Kile ambacho kanisa linahitaji kwa wakati wa sasa siyo mashine zaidi au kitu kingine cha ziada, siyo mashirika mapya au ziada ya hayo, na siyo mbinu mpya, bali wanahitajika watu ambao Roho Mtakatifu anaweza akawatumia—watu wa maombi, watu wenye uwezo mkubwa kwenye maombi. Roho Mtakatifu hatiririki kupitia mbinu zilizopo, bali kupitia watu. Roho Mtakatifu haji juu ya mashine, bali juu ya watu. Roho Mtakatifu haachilii upako wake kwenye mipango, bali kwa watu—watu wa maombi.[112]

► Je, kuna kosa gani ambalo E. M. Bounds anajaribu kulisahihisha kupitia taarifa zilizoko hapo juu?

Kitendo cha maombi hutoa taarifa ya utegemezi kwa Mungu, Mtu ambaye anashughuli nyingi kwenye mambo yake hata akashindwa kuomba anafikiri kwamba kazi yake ni muhimu zaidi kuliko kazi ambayo Mungu ataifanya katika kujibu maombi yake.

Kwa kuwa sisi ni tegemezi kwa Roho Mtakatifu, maombi ni muhimu sana kwetu. Paulo aliwataka watu waombe kwa ajili ya kuieneza injili.[113]

## Kwa nini maombi ni muhimu

► Tunajua kwamba maombi ni muhimu kwa mwamini. Je, kuna sababu gani chache za kuomba ambazo ni muhimu kwa mtu ambaye ni mwinjilisi?

Maombi ni muhimu kwa ajili ya mwinjilisti:

**(1) Mwinjilisti ni lazima awe hai kiroho**.

Maombi ndiyo pumzi ya roho. Mwinjilisti huwaongoza watu wengine kwenye uhusiano na Mungu ambao tayari yeye anao

**(2) Mwinjilisti hawezi akadumisha ari kwa ajili ya huduma bila ya kutumia muda wake na Mungu kwenye maombi**.

Bila ya maombi, mtu anayejaribu kufanya huduma ya uinjilisti atakuwa na motisha potofu (aidha wa kutafuta mafanikio binafsi au kufurahia mabishano).

---

[112] E. M. Bounds, *Power through Prayer*
[113] 2 Wathesalonike 3:1, Wakolosai 4:3, Waefeso 6:19

**(3) Mwinjilisti ni lazima awe tegemezi kwa Mungu katika kumwonyesha mwenye dhambi kwamba ana hatia na aweze kumpa matamanio yatakayomwezesha kuokoka**.

Uinjilisti hautegemei nguvu za mwanadamu peke yake. Mwinjilisti anategemea kupata nguvu kutoka kwa Roho Mtakatifu. Sababu za kufikirika za mwanadamu peke yake haziwezi kumfanya menye dhambi akubali kwamba ni mwenye hatia na atamani kumtafuta Mungu.[114]

> "Kama matamanio yako ya kusoma yanazidi matamanio yako ya roho za wengine, simama, na omba hadi mtamanio yako kwa ajili ya roho za wengine yatakapozidi matamanio yako ya kusoma."
> - William Smith,
> (Mwanzilishi wa
> Union Bible College)

**(4) Mwinjilisti anamtegemea Mungu ili amsaidie kuhubiri Neno kwa ufanisi**.[115]

**(5) Mwinjilisti anahitaji uongozi wa Mungu katika huduma yake.**[116]

## Utekelezaji wa Maombi

### Maisha Binafsi ya Maombi

Kila Mkristo anapaswa awe mwaminifu katika maombi ya kila siku, na umuhimu ni mkubwa zaidi kwa mtu ambaye anataka kuwa na ufanisi kwenye uinjilisti.

Anapaswa awe na muda wake maalumu kila siku ambao anautumia yeye peke yake na Mungu. Ikiwezekana, anatakiwa akae eneo la peke yake lisilokuwa na mwingiliano wa kitu chochote. Anaweza kuhitajika kuamka mapema sana ili aweze kuomba pasipo usumbufu kabla ya ratiba ya shughuli za kila siku haijaanza. Kama hawezi kufanya maombi yake maalumu katika muda wa mapema, anaweza kuchukua muda wa dakika chache kwenye mwanzo wa siku ili kuweza kuzungumza na Mungu.

Anapaswa asome baadhi ya maandiko kila siku na afanye tafakuri ya maandiko hayo, akiomba Mungu atimize ukweli uiloko katika Maandiko hayo kwenye maisha yake.

### Orodha ya Mambo ya Kuombea

Ni vyema kuorodhesha mambo ambayo tunapaswa kuyaombea. Vinginevyo, inawezekana tusikumbuke baadhi ya mambo muhimu ya kuombea. Tunatakiwa tuwe tunaomba kwa ajili ya injili ienee duniani kote, hasa katika nchi ambazo Wakristo wako kwenye mateso. Tunatakiwa tuwe tunaomba kwa ajili ya mafanikio ya injili katika nchi yetu wenyewe. Tunatakiwa tuwe tunaomba kwamba kanisa likamilishe mpango wa Mungu wa umisheni kwa ajili ya jamii yetu. Tunatakiwa tuwe tunaomba kwamba Mungu atusaidie binafsi katika kushirikisha injili kwa ufanisi mkubwa.

---

[114] Yohana 16:8, Yohana 6:24
[115] Warumi 1:16, Isaya 55:11
[116] Matendo 11:12

Orodha pia inamsaidia mtu katika nyakati ambazo ana matatizo endelevu yaliyombana.

Siyo muhimu kutumia orodha ya maombi kila wakati unapokuwa unaomba. Mara nyingine unajisikia kuomba kwa ajili ya mambo fulani, na una uwezo wa kuyakumbuka bila ya kuwa na orodha ya maombi.

► Je, ni mambo gani mengine yanapaswa yawe kwenye orodha ya maombi?

**Orodha ya Majina kwa ajili ya Maombi**

Orodhesha majina ya watu kumi ambao unajua wanahitaji waokoke. Watu hawa wawe ni wale ambao mara nyingi uko pamoja nao. Jihusishe katika kuwaombea kila siku. Kama Mungu atafungua nafasi zungumza nao; kama hakuna nafasi ya kuzungumza nao, endelea kuwaombea. Kwa mujibu wa ushuhuda wa watu wengine ambao waliwahi kufanya hivyo, kama utafanya hili, kabla ya mwaka mmoja kupita baadhi ya hao watu watakuwa wameokoka.

> "Watu ambao kwenye mabega yao yalibeba wajibu wa msingi wa kuifanya dunia iwe ya Kikristo walikuja kwa Yesu wakiwa na ombi moja kuu. Hawakusema, 'Bwana, tufundishe kuhubiri,' au 'Bwana, tufundishe jinsi ya kufanya miujiza,' au 'Bwana, tufundishe jinsi ya kuwa na hekima' lakini walisema, 'Bwana tufundishe jinsi ya kuomba.'"
> - Billy Graham

**Wabia wa Maombi**

Ni vyema kwa Mkristo kuwa na rafiki ambaye atakuwa akishirikiana naye katika maombi mara kwa mara. Watapaswa washirikishe mahitaji na ushindi kwa pamoja. Wanaweza wakakutana kila wiki, au mara nyingi zaidi.

Kwa njia hii mume na mke wanaweza kushirikiana kuomba pamoja; lakini ni jambo jema zaidi kwa mwanamume kuwa na mwenzake wa kiume katika maombi, na mke akawa na mwanamke mwenzake wa kuomba naye kama mbia wake wa maombi.

► Je, ni uzoefu gani walio nao washiriki darasani katika kuwa na wabia wa maombi?

**Matembezi kwa ajili ya Maombi**

Kutembea katika maombi kunaweza kufanyika kwa sababu ya huduma kujisikia inawajibika kwa ajili ya majirani wanaowazunguka. Kikundi au watu binafsi wanaweza kuwa wanatembea kwenye eneo husika wakiwa wanaomba kwa ajili ya mahitaji ya eneo hilo. Maombi yanaweza kuwa ni ya kimya kimya. Wanaweza kuzungumza na watu wanaokutana nao, lakini kusudi la msingi la matembezi hayo ni maombi. Matembezi kwa ajili ya maombi yanaweza yakafanyika mwanzoni mwa huduma katika eneo husika au yanaweza yakafanyika baadaye.

**Kituo cha Maombi**

Baadhi ya makanisa yameanzisha vituo vya maombi vya muda kwenye maeneo ya wazi ambayo watu wengi wanapita. Wanaweka hapo ishara inayosema "Kituo cha Maombi" na wanajitolea kuomba na watu wanaopita eneo hilo. Wanauliza, "Je, unalo hitaji ambalo

ungetaka mimi niombe kwa ajili yake?" Onyesha kuwa mtu unayehusika na mahitaji ya watu na siyo kuanza mabishano. Mara nyingi huwa wanapata nafasi ya kushiriki injili.

► Je, ni eneo gani linafaa kwa ajili kuweka kituo cha maombi katika eneo lako?

## Maombi ya Kibiblia

Maombi aliyoomba Yesu pamoja na mitume yanatuonyesha kwamba tunapaswa kuomba, kwa sababu tunajua kwamba waliomba katika mapenzi ya Mungu. Hapa kuna mifano mitatu:

**Sala ya Bwana**: Katika Mathayo 6:9-13, Yesu alitoa mfumo wa maombi kwa wanafunzi wake. Tunapaswa tuombe kwa maneno haya, lakini pia tunapaswa tuombe kwa ujumla pamoja na vipaumbele hivi.

**Maombi ya Paulo kwa Waefeso**: Katika Waefeso 3:14-19, Paulo aliomba kwa ajili ya kufanywa imara kwa waamini. Tunapaswa tuombe maombi hayo hayo kwa ajili yetu wenyewe na watu wengine.

**Maombi ya Mavuno**: Katika Mathayo 9:36-38, Yesu alitaka wanafunzi wake kushirikisha huruma zake kwa wenye dhambi na kuomba kwamba Mungu atume watendakazi kwenye mavuno ya kiroho

## Utekelezaji wa Kufunga

Kufunga ina maana ya kuweka mtazamo wetu kwenye mambo ya kiroho na ya milele, mbali na mambo ya kimwili na yale ya muda mfupi yanayopita. Kufunga kunadhihirisha kwamba mambo ya kiroho na ya milele ni muhimu zaidi kuliko mambo ya kimwili na yale ya muda yanayopita. Hii ni njia mojawapo ya kuimarisha imani yetu.

► Je, Ni kwa jinsi gani kufunga kuna tofauti na mtu anayejitesa kwa njaa ili kumshawishi Mungu amtendee jambo fulani?

## Mifano ya Kimaandiko kuhusiana na Kufunga

Hii ni mifano iliyo kwenye kumbukumbu za Maandiko katika nyakati ambazo mtu alikuwa na dhamira kubwa ya Mungu kuingilia kati katika maisha yake ambayo ilimsukuma kufunga. Mifano hii imechaguliwa miongoni mwa mifano mingi ya kurejelea katika Maandiko ili tu kuonyesha kwamba Biblia kwa kawaida hupendelea kuzungumzia kuhusu kufunga. Katika Maandiko, mara nyingi yametajwa kama sehemu ya maelezo ya ni kwa nini Mungu aliingilia kati.

► Soma mojawapo ya haya Maandiko kuhusiana na kufunga na wajadili mazingira yaliyoelezwa katika kifungu hicho.

| Maandiko | Matokeo ya Kusali na Kufunga |
|---|---|
| 2 Mambo ya Nyakati 20 | Kufunga kwa taifa zima kulileta ushindi kwenye vita. |
| Ezra 8:21 | Ezra alifunga na kuomba ili kuomba ulinzi wa Mungu kutoka katika hatari. |
| Esta 4:16 | Wayahudi walifunga kwa ajili ya Mungu kuingilia kati katika mpango uliokuwa umeandaliwa wa kuwaangamiza kwa mauaji ya kimbari. |
| Yona 3:5-9 | Ninawi walifunga kwa ajili ya kuomba rehema ya Mungu. |
| Waamuzi 20:26 | Israeli ilifunga kwa ajili ya kupata mwongozo wa Mungu katika vita. |
| 1 Samweli 7:6 | Israeli ilifunga kwa ajili ya msamaha na ukombozi. |
| Nehemia 1:4 | Nehemia alifunga kwa ajili ya kumwomba Mungu awawezeshe kulijenga jiji kwa upya tena. |
| Danieli 9:3 | Danieli alifunga kwa ajili ya ukombozi wa Israeli kutoka utumwani. |
| Yoeli 2:12 | Kufunga kuliitishwa kulikoambatana na kuomba masamaha na kuepukana na hukumu. |
| Mathayo 4:2 | Yesu alifunga kwa siku arobaini (40) kwa ajili ya maandalizi ya huduma yake hapa duniani. |
| Luka 2:37 | Anna alikuwa nabii wa kike aliyeutumia muda wake mwingi katika kufunga na kuomba. |
| Matendo 10:30 | Kornelio alikuwa katika hali ya kufunga wakati alipopokea ujumbe kutoka kwa Mungu. |
| Matendo 13:2-3 | Wakiwa katika kufunga, kanisa liliagizwa na Mungu litume wamishenari. |
| Matendo 27:21 | Paulo alifunga na kuomba katika nyakati za migogoro. |

## Maelekezo ya Yesu

Yesu alisema kwamba wanafunzi watapaswa kufunga wakati atakapokuwa hayupo tena pamoja nao kimwili.[117] Aliwaelekeza njia sahihi ya kufunga. Alisema kwamba kufunga kusingepaswa kuwe ni onyesho la watu wengine kuona.

> Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.[118]

## Mifano ya Kihistoria kuhusiana na Kufunga


Baadhi ya waamini katika kanisa la kwanza walifunga kwa kutokula mlo mmoja kila Jumatano na Ijumaa ya wiki, mbali na siku za kufunga zilizokuwa zimeratibiwa katika mwaka. Martin Luther, John Calvin, John Knox, Jonathan Edwards, Charles Finney, na D. L. Moody wote kwa pamoja walifunga sana. Kila uamsho uliokuwa na mwisho mwema wa mafanikio muhimu ulianza kwa maombi na kufunga.

► Je, ni watu gani unaowajua ambao walishawahi kupata matokeo mazuri kutokana na kufunga?

## Udhaifu wa Kanisa la Sasa

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba walikuwa wameshindwa kumsaidia mtu aliyekuwa amepagawa na mapepo kwa sabau ya kutokuamini kwao. Kisha baadaye akasema, "Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga."[119] Alimaanisha kwamba maombi na kufunga ndio njia ya kuimarisha imani; Na, kwa hiyo, ndiyo tiba ya kutoamini. Hakumaanisha kwamba wanafunzi wataanza tu kufunga wakati kunapojitokeza mgogoro; alimaanisha kwamba maombi na kufunga mara kwa mara kunapaswa kuwe ni sehemu ya maisha yao, ili waweze kuwa na imani inayohitajika kwa ajili ya kukabiliana na migogoro.

Tukitafakari kutokana na maneno ya Yesu na kutokana na mifano mingi ya kimaandiko na kihistoria, tunaweza tukatengeneza umbo la mchoro wa baraka zetu zinazopatikana kwetu kwa kuwa na mchoro wa pembe tatu iliyogawanyika katika viwango (ngazi) kadhaa. Viwango vya chini vya baraka vinaweza kupatikana kutokana na kiwango cha imani tuliyofikia katka maombi peke yake. Viwango vya juu vya baraka vitapatikana tu kutoka kwenye imani iliyofikiwa kupitia katika maombi na kufunga kwa tukiwa pamoja.



[117] Mathayo 9:15, Luka 20.
[118] Mathayo 6:16-18
[119] Mathayo 17:21

## Jinsi ya Kufunga kwa Usahihi

- Changanya kwa pamoja maombi na kufunga ili kwamba kufunga kusiwe tu ni kitendo cha nje, bali kufanywa upya kiroho na kufanya imani yao kuwa endelevu.
- Funga kwa madhumuni ya kumtukuza Mungu na siyo kwa ajili ya majivuno.
- Wakati unapokuwa unaomba na kufunga, tafuta mapenzi ya Mungu kuhusiana na hitaji lako.
- Usifanye utiifu kuwa ni mbadala wa kufunga.
- Usiuumize mwili wako.

► Jadili tendo la kufunga na kuomba vitakavyoweza kufanyika kwa pamoja.

## Usalama wa Kufunga

Kufunga haina madhara ya afya kama ikifanywa kwa njia iliyo sahihi. Kwa kweli, kuna faida nyingi za kiafya zinazoambatana na kufunga mara kwa mara.

- Kunywa maji wakati wa kufunga. Usifunge kunywa maji.
- Anza kwa kufunga mara moja. Hatua kwa hatua ongeza vipindi virefu zaidi vya kufunga. Kuwa na wiki moja la kutumia chakula kikawaida kati ya siku moja ya kufunga au zaidi.

Vipndi vya kichefuchefu na maumivu ya kichwa ni jambo la kawaida kwa watu ambao hawana uzoefu wa kufunga. Kama mtu alie na afya njema akifunga mara kwa mara, hataweza kuwa na dalili hizo baada ya siku chache za mwanzo. Ladha mbaya kwenye mdomo na harufu mbaya huja wakati wa kupumua kwa sababu mwili unatoa sumu zilizoko kama uchafu.

Kwenye ufungaji wa muda mrefu, wingi wa dalili za kutojisikia vizuri hutoweka baada ya siku chache.

- Unapotoka katika kumaliza mfungo wa muda mrefu anza kwa kutumia juisi, kisha chakula chepesi.

## Kazi za Kufanya

(1) Fikiria ni nini utakachofanya katika kuendeleza uzoefu wako mwenyewe wa maombi. Chagua muda na kiwango cha muda utakachokitoa kwa ajili ya maombi ya kila siku. Fikiria kuandaa ratiba yako ya kufunga mara kwa mara.

(2) Soma vifungu viwili vya Maandiko kutoka katika vifungu vya kufunga. Andika aya moja nzuri kwa kila aya, ukielezea mazingira na matokeo ya kufunga.

# Somo la 8
# Mbinu za Yesu

## Utangulizi

► Soma Mathayo 19:16-22. Ni nini cha kukushangaza katika jibu la Yesu kwa mwanamume huyu? Kama ungesikia rafiki yako akitoa jibu hilo kwa mtu ambaye ameuliza ni kwa jinsi gani aurithi uzima wa milele, ungependa ueleze nini kwa huyo rafiki yako?

## Karama ambayo Haikueleweka

Jaribu kufikiria kwamba uko kwenye afya nzuri, lakini rafiki yako akaja kwako na kusema kwamba amenunua dawa ya tiba kwa ugonjwa fulani unaoweza kusababisha madhara ya kifo.[120] Ili kuweza kuinunua dawa hiyo, aliuza nyumba na vitu vyote alivyokuwa navyo. Aliinunua dawa hiyo ya tiba kwa ajili yako.

► Je, utasema nini kwa rafiki yako wakati akikupa zawadi yako hiyo?

Kwa vyovyote utamshukuru kwa ukarimu wake, lakini hutakuwa umeilewa hiyo zawadi. Kwa nini atumie gharama kubwa kiasi hicho kwa ajili ya kukununulia kitu ambacho huna hitaji nacho?

Sasa jaribu kufikiria tena taarifa nyingine tofauti. Umekuwa kwa daktari na ukakutwa una ugonjwa wenye madhara makubwa. Dawa kwa ajili ya tiba yake ni ya gharama kubwa, na huna namna yeyote ya kuweza kuilipia. Unaondoka kwenda nyumbani huku ukiwa unawaza kuhusu kifo, ukitambua kwamba familia yako itakukosa na kamwe hutakuwa na uwezo wa kutimiza kile ulichokuwa umetegemea katika maisha yako.

Kisha akajitokeza rafiki na kukuambia kwamba alitoa kila kitu alichokuwa nacho kwa ajili ya kukununulia hiyo dawa. Utaridhika na jambo hilo kwa sababu kwanza unaelewa hitaji lako. Zawadi yake ni uhai kwa ajili yako.

Sasa fikiria kuhusu majibu ya watu wa dunia wakati wanaposikia habari za injili. Neno *injili* lina maana ya "habari njema," lakini watu wengi hawaelewi kwa nini ni habari njema.

Jaribu kufikiria kuhusu mtu aliyeitwa Petro. Marafiki zake wanamwambia kwamba, "Yesu alikufa msalabani kama dhabihu ili kwamba dhambi zako ziweze kusamehewa."

Petro anafikiria, "Mimi siyo mtu mbaya. Mimi ni mzuri kwa marafiki zangu na kwa familia yangu. Kwa nini kuhitajike dhabihu kubwa kiasi hicho kwa ajili ya dhambi zangu? Kwa nini msamaha ni jambo muhimu kiasi hicho? Petro anaweza kukasirika kwamba rafiki yake

[120] Wingi wa taarifa za somo hili zinawasilishwa na Ray Comfort kwenye mahubiri yake "Hell's Best-Kept Secret" na kitabu chenye kichwa hiki hiki cha somo. Nyenzo nyingine zinapatikana kutoka katika http://www.livingwaters.com.

anamfikiria ni mtu mbaya mtenda dhambi ambaye atahitaji kifo cha Yesu kwa ajili ya msamaha wake.

Biblia inatuambia kwamba watu wanakerwa na msalaba. Watu wanataka wapate njia ya kujihesabia haki wao wenyewe. Hawafikiri kwamba wanahitaji dhabihu ya Yesu, kwa hiyo msalaba unaonekana kama ni upumbavu kwao.[121]

Kama yalivyo maelezo kuhusiana na dawa ya tiba kwa ajili ya ugonjwa, watu hawakubaliani na msalaba kwa sababu hawaelewi ni kwa nini wanauhitaji.

Njia ya kibiblia ya kuwaandaa watu kwa ajili ya habri njema ni kuwaonyesha ni kwa nini wanahitaji injili. Wanapaswa kutambua kwamba wao ni watenda dhambi ambao muda siyo mrefu watahukumiwa na Mungu.

► Je, ni kwa nini mtu anapaswa kufurahi anaposikia injili?

## Umuhimu wa Hukumu

Ukweli kwamba wenye dhambi watahukumiwa na kupewa adhabu ndiyo sababu ya muhimu ya mwenye dhambi kuwa na furaha ya kusikia injili.

> Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.[122]
>
> Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.[123]

► Soma maelezo ya hukumu ya mwenye dhambi katika Ufunuo 20:12-15.

Hukumu ya mwisho ya wenye dhambi ndiyo sababu kuu ya msingi ya kila mwenye dhambi kuhitajika kuokoka.

Mungu ameagiza kila mtu atubu, "Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki."[124]

Kama mtu hawezi kuelewa kwamba dhambi yake inamweka kwenye hali mbaya, anakosa sababu muhimu sana ya kuhitaji wokovu.

► Je, ni nini kitakachomfanya mwenye dhambi ajitambue kwamba dhambi yake inamweka kwenye hali mbaya?

## Matumizi ya Sheria

Watu wengi hawako katika hali ya kuitamani injili kwa sababu hawajioni wenyewe kwamba ni wenye hatia. Biblia inasema kwamba watu wengi wanajihesabia wenyewe

[121] 1 Wakorintho 1:18
[122] Waebrania 9:27
[123] Mathayo 12:36
[124] Matendo 17:30-31

kwamba ni watu wazuri (*hawana hatia*). [125] Kama utamwuliza mtu yeyote kama yeye ni mtu mzuri, bila shaka atakujibu kwamba “ndiyo” na kuwa tayari kujitetea mwenyewe. Watu wengi wanafikiri kwamba dhambi zao siyo uovu, na kwamba watapaswa kuwiwa radhi. Watu kama hao kuwapa neema na msamaha hakuleti maana yeyote.

Mtu ni lazima ajiangalie mwenyewe kama mtenda dhambi na ajisikie mwenye hatia katika dhamira yake kabla hajajiona mwenye kuhitaji nema. Mungu ametoa sheria kuonyesha kuhusu dhambi.

Kwa kusema *sheria* hatumaanishi hususani taratibu za ibada za Agano la Kale ambazo ziliwaongoza watu kuabudu kwenye sinagogi. Pia hatuzungumzii kuhusu sheria zilizokuwa zimetolewa kwa ajili ya serikali ya Israeli, ambazo hazitumiki kwetu kwa njia inayofanana. Tunazungumzia kuhusu kipimo cha Mungu cha haki. Mfalme Daudi aliandika katika kitabu cha Zaburi 119 jinsi alivyokuwa ameipenda sheria ya Mungu kwa jinsi alivyokuwa anampenda Mungu, kwa sababu ilitoka katika tabia ya utakatifu ya Mungu mwenyewe.

Sheria ya Mungu inatuonyesha jinsi ya kuishi, na tuna hatia kwa kuikataa. Hakuna mtu atakayehesabiwa haki kwa kuishika sheria[126] kwa sababu kila mtu ametenda dhambi. Mtu anaitumia sheria vibaya kama atakuwa nafikiria kwamba kwa kujaribu kuifuata sheria atapata wokovu wake.

Sheria ya Mungu inayaongoza maisha yetu,[127] lakini siyo njia ya wokovu wetu. Sheria haingeweza kutuleta sisi kwenye wokovu kwa sababu hatuna uwezo wa kutekeleza kwa ukamilifu mahitaji yake yote tangu kuzaliwa. [128]

Sheria haipingani na injili kwenye mpango wa Mungu. Biblia inatuambia kwamba sheria inatumika kwa kusudi la kumfanya mwenye dhambi atambue hitaji lake la wokovu. Injili haijaivuruga sheria[129] au haijaifanya sheria isiwe na maana kwetu. Sheria inatumika kama maandalizi makamilifu kwa ajili ya injili, siyo kwa nyakati za kale tu bali hata sasa.

“Sheria (torati) imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo,”[130] Baadhi ya watu wanafikiri kwamba kulikuwa na kipindi ambacho sheria ilishapita , na kwa sasa kuna kipindi cha neema. Ukweli ni kwamba kila mtu ni lazima atakutana na sheria ya Mungu na atatambua kwamba anahesabika mwenye hatia kabla hajaelewa kuhusu neema. Mtume Paulo alisema, “Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria.”[131]

Paulo alisema kwamba sheria imetolewa ili wenye dhambi waonyeshwe kwamba wana hatia na hawawezi kujitetea; kwa sababu, kwa sheria watu hutambua kwamba wao ni

---

[125] Mithali 20:6
[126] Wagalatia 2:16, Warumi 3:20
[127] 1 Wakorintho 9:21
[128] Warumi 8:3, Wagalatia 3:21
[129] Mathayo 5:17
[130] Wagalatia 3:24
[131] Warumi 7:7

watenda dhambi.[132] Kila mtu yuko "chini ya sheria" na kufanywa mwenye hatia na hiyo sheria hadi atakapokuwa ameokoka.

Injili huwa siyo habari njema kwa mtu ambaye hataki kujua kwamba dhambi yake imemweka mahali pabaya. Injili ni habari njema kwa mtu anayeelewa kwamba yeye ni mwenye hatia na hivi punde atakutana na hukumu ya Mungu.

► Soma Luka 18:10-14. Kama angetokea mtu akamweleza yule Farisayo kwamba bila ya gharama yeyote anaweza akasamehewa kwa neema ya Mungu, angewezaje kujibu hili?

## Kosa la makanisa ya leo ya ki-injili (evangelicals)

Leo makanisa ya kiinjili mengi hawataki kuwekea mkazo kila mtu ni mwenye hatia kutokana na dhambi na anastahili adhabu ya Mungu.

Hawataki kuwaambia watu kwamba wao ni watu wabaya.

> "Kubadilika kunahusisha kutengana kikamilifu na mambo ya zamani ambayo huitwa yamekufa. Sisi tumesulubiwa pamoja na Yesu. Kupitia katika msalaba wake, tumekufa kwa mambo maovu ya dunia, matarajio yake na vipimo vyake vyote."
> - Kamati ya Dunia ya Uinjilishaji ya Lausanne, *Taarifa ya Willowbank*

Wanataka kuzungumzia mambo chanya tu badala ya hasi.

Wanataka kutoa manufaa ya haraka ya wokovu, badala ya manufaa ya milele, kwa sababu wanazungumza na watu ambao wameweka mtazamo wao kwenye mambo ya dunia hii.

Wanachukulia kwamba sheria ya Mungu ni jambo baya, ni adui wa wokovu, na ni muhimu tu kwa watu ambao wanataka waokoke kwa matendo yao. Biblia inasema kwamba sheria ni nzuri na takatifu; [133] mtu anayetaka kumpendeza Mungu atajaribu kufuata maelekezo ya Mungu katika maisha yake yote. [134]

Wanadhani kipimo cha Mungu haiwezekani na hakiingii akilini, na kwamba hupaswi kujilaumu kwa ajili ya dhambi zako.

Tatizo ni kwamba kama mtu kwa uhakika siyo mwenye hatia, hawezi akatubu. Hawezi akajutia kwa yale anayotenda labda iwe anajua kwamba amechagua mwenyewe kutenda uovu. Kama mtu haamini kuwa yeye ni mwenye dhambi pale anapoomba msamaha, kwa ukweli ni sawa tu na kuomba Mungu akubaliane na makosa yake ya kibinadamu.

Ukweli ni kwamba wenye dhambi hawahesabiwi kuwa na hatia kwa ajili ya kuzaliwa na asili ya dhambi. Wanahesabiwa kuwa wana hatia kwa matendo na mienendo yao ya dhambi wanayofanya kwa hiari yao wnyewe ambayo ni uasi dhidi ya Mungu.[135]

---

[132] Warumi 3:19-20
[133] Warumi 7:12-14
[134] Zaburi 119:1-8
[135] Yuda 15

Watu wengi wanaamini kwamba Mungu ni wa upendo na mwenye kusamehe, lakini hawatambui pia kwamba ni Mungu anayehukumu kwa haki. Wanategemea kwamba endapo itatokea wakakutana na Mungu, atawasamehe hata kama kamwe hawakuwahi kutubu. Injili isiyokuwa kamili ambayo waiiisikia imewafanya wawe watu wa kuridhika sana katika dhambi zao.

Makanisa mengi ya ki-injili leo hii yanasisitiza kwamba kama mtu anakuwa Mkristo, atakuwa na maisha yenye furaha zaidi. Wanasema kwamba dhambi haimridhishi mtu, lakini Mungu anafanya hivyo. Wanasema kwamba mtu atapokea upendo, amani, na furaha. Wanasma kwamba Mungu anao mpango wa ajabu kwa ajili ya maisha ya kila mtu, na kwamba mpango huo utatimilika kama mtu ataokoka.

Ahadi hizi inawezekana zisieleweke. Mungu hutoa upendo wake na amani, lakini kutakuwepo na mgogoro kwa watu ambao wanamkataa Mungu.[136] Anatoa furaha, lakini wakati huo huo panaweza kuwepo na mateso.[137] Ana mpango kwa kila mtu, lakini Mkristo anaweza akakutana na mazingira magumu na mambo makubwa yaletayo huzuni.[138] Kama mtu ataamua kuwa Mkristo kwa sababu ya kudhania kwamba maisha yake yatakuwa mazuri zaidi, anaweza akakatishwa tamaa sana. Watu wengine wanapata mateso makubwa sana kwa sababu tu wao ni Wakristo.

Kama Wakristo, tunaelewa kwamba maisha pamoja na Mungu ni mazuri sana, hata kama tunateseka katika mazingira magumu. Tunaweza kusema kwamba kumtumikia Mungu ni maisha mazuri sana. Hata hivyo, watu wengi ambao hawajaokoka hawana wazo sahihi kwamba maisha mazuri sana ni nini. Kama utawauliza kutoa ufafanuzi wa maisha mazuri sana watakujibu kwa kuzungumzia afya, fedha, uhuru, amani, na hali nyingine nzuri. Hawatakuwa wanaelewa kwamba Mkristo anayeumizwa kwa mateso na kuteseka anamaisha mazuri sana. Kwa hiyo, kama utamweleza mwenye dhambi kwamba kama akiwa Mkristo atakuwa na maisha mazuri sana, inawezekana asielewe kitu unachomwahidi.

Kuna tatizo lingine la ufahamu potofu wa injili. Mtu anaweza akaukubali ujumbe bila ya kujikagua mwenyewe kama ni mwenye dhambi anayestahili kuhukumiwa. Kwa sababu haoni uzito na madhara ya dhambi, kwa ukweli hatubu. Hatafuti wokovu wa kuachana na dhambi, bali kwa ajili ya manufaa mengine. Anaweza akafikiri kwamba ameokoka wakati kiuhalisia sivyo alivyo.

Hawezi pia hata kupokea manufaa ya kweli ya wokovu kwa ajili ya maisha yake, kwa sababu hajaokoka. Anajaribu kwa muda mfupi kisha anaacha kwa kukata tamaa.

Matokeo mabaya zaidi ya injili potofu ni kwamba mtu aliyekuwa amekata tamaa ana uwezekano mkubwa wa kutokubaliana na injili ya kweli katika siku za baadaye.

---

[136] Mathayo 10:34-36
[137] 1 Wathesalonike 1:6
[138] 2 Wakorintho 11:24-27

Kwa muhtasari, matatizo yanayotokana na injili ya maisha mazuri sana ni kama yafuatayo:

1. Inatoa ahadi ambazo Mungu hajawahi kuahidi.
2. Haieleweki kwa mwenye dhambi.
3. Mtu hataweza kuwa amebadilika kiukweli.
4. Hatapata manufaa aliyokuwa anategemea.
5. Ana uwezekano mkubwa wa kutokubaliana na injili ya kweli katika siku za baadaye.

► Soma Matendo 14:21-23. Je, ni kitu gani mitume walichowaambia waumini wapya wategemee?

Yesu aliwaonya wanafunzi wake kwamba watu watawachukia kwa sababu ya imani yao katika Kristo. Aliwaambia hawatakuwa wameokoka hadi hapo watakapokuwa wamevumilia hadi mwisho. Waandishi watatu miongoni mwa waandishi wa injili waliandika haya maneno.[139] Wengi wa mitume wa kwanza walikufa kwa ajili ya Kristo.

Mamilioni ya Wakristo wameshauawa kwa ajili ya imani yao. Hili siyo tatizo kwa ajili ya zamani tu. Zaidi ya nusu ya wafia imani waliuawa katika karne ya 20.

Kama mtu atabadilika kwa sababu ya ahadi ya wokovu bila ya ahadi ya maisha mazuri, hatakata tamaa kwa sababu ya maisha magumu. Atakuwa tayari kuhimili majaribu kwa ajili ya wokovu wa milele. Majaribu hufanya wokovu kwa mtu huyu kuwa kitu cha thamani sana kwake.

► Je, kwa nini Wakristo wanastahimili mateso?

## Kuonyesha Upendo

► Soma 2 Timotheo 2:24-26. Je, aya hizi zinatueleza nini kuhusu tabia ya mwinjilisti?

Mwinjilisti hapaswi kuwa mtu anayeonekana kupambana na watu anaowafanyia huduma ya uinjilisti. Shetani ni adui, na wenye dhambi ni mateka wa shetani. Tunapaswa tueleze ukweli kwa upole. Kusudi letu ni kuwasaidia, na siyo kuwashinda kwa mashindano. Maneno yanayotumika katika kifungu hiki yanahusisha pamoja na upole, unyenyekevu, na uvumilivu.

► Soma Tito 3:2-5. Kifungu hiki kinaseme nini kuhusiana na mwenendo wa mwinjilisti?

Tunapaswa tukumbuke kwamba bila ya neema ya Mungu, tutakuwa kama watu wa kidunia. Mungu alikuja kwetu siyo pamoja na hukumu, bali alikuja kwetu kwa upole na upendo.

[139] Mathayo 10:22, Marko 13:13, Luka 21:17

Mwinjisti hapaswi kuwa na hasira na mwenye dhambi, bali dhidi ya dhambi na Shetani. Hapaswi kuwa mkali. Hapashwi kufurahia katika kutafuta makosa yao, lakini anapaswa kuwajibika kwa ajili ya wokovu wao.

Tumejifunza kwamba hatupaswi kuonyesha upendo kwa mwenye dhambi kwa kuahidi ahadi ambazo Mungu hakuwahi kuahidi. Hatupaswi kuonyesha matendo ya huruma kana kwamba matatizo yao ya maisha ni ya muhimu zaidi kuliko hatima yao ya milele.

Yesu alikamilisha unabii kwamba Masihi hangelikuwa mtu wa vurugu, bali mpole, na hangekuwa mtu wa kumuumiza mtu ambaye amejeruhiwa na dhambi.[140]

► Je, ni kwa njia gani tunaweza kudhihirisha upendo wa Mungu wakati tunapofanya uinjilisti?

## Uinjilisti wa Kibiblia

Mtazamo wa kibiblia katika uinjilisi ni kutumia sheria ya Mungu katika kuwaandaa watu waipokee injili. Sheria inawahukumu wenye dhambi na kuwaonyesha kwamba watahukumiwa endapo hawatatafuta kusamehewa.

Yohana Mbatizaji alihubiri kwamba watu wanapaswa kutubu kwa ajili ya maandalizi ya ujio wa Bwana na ili kuepukana na hukumu.[141]

Yesu alihubiri mara nyingi kuhusu hukumu na moton. Alitoa neema kwa wale waliojutia kuhusu dhambi zao.

► Soma Luka 7:36-50. Je, ni aina gani ya mtu anayepaswa kupewa msamaha?

Hatuoni mahali popote katika huduma ya Yesu kwamba alitoa msamaha kwa watu ambao hawakuwa wamejutia dhambi zao. Alionya watu kuhusu uwepo wa hukumu. Baada ya kuonyesha maafa ambapo watu wengi waliuawa, Yesu aliuambia umati wa watu kwamba wote wataangamia kama hawatatubu.[142]

Yesu alitoa mfano wa mtoza ushuru na Mfarisayo walioomba maombi tofauti. Mtoza ushru alijutia makosa yake na akapokea msamaha. Mfarisayo alijaribu kujiinua na kujiridhisha mwenyewe kwamba siyo mtenda dhambi. Haingekuwa na maana yeyote kutoa msamaha kwa Mfarisayo kwa sababu hakuwa anaamini kama aliuhitaji huo msamaha.

Mtume Petro alihubiri ahadi ya maisha ya uzima wa milele na akawataka watu kutubu ili wapokee msamaha.[143]

Stepheno, akiwa anahubiri kwa watawala wa Kiyahudi, hakutamka neema juu yao, bali aliwashutumu kwa kumkataa Mungu na kuvunja sheria yake.[144]

[140] Mathayo 12:19-20
[141] Mathayo 3:1-12
[142] Luka 13:1-5
[143] Matendo 2:38, Matendo 3:19, Matendo 5:31

Paulo alihubiri kwamba watu wanapaswa kutubu kwa sababu Mungu hatakuwa na msamaha juu ya dhambi.[145]

Siyo jambo baya kuzungumzia kuhusu furaha na baraka zinazotokana na mtu kuwa Mkristo; lakini mbinu ya msingi ya wainjilisti katika Biblia ilikuwa ni kuhubiri hadi kumleta mtu ajisikie kwamba ni mwenye kuhitaji msamaha, akipokea wokovu badala ya hukumu.

► Soma 2 Wakorintho 5:11. Je, Mtume alisema nini kwa ajili ya kushawishi?

► Soma Matendo 24:25. Je, mtume Paulo alisema nini kuhusu Feliki? Je, Feliki aligusikaje?

### Mfano wa Uinjilisti wa Kibiblia

Andrea alikuwa akisambaza mialiko ya kuja kanisani wakati alipokutana na Petro.

Petro: Silihitaji kanisa.

Andrea: Biblia inaema kwamba kila mtu atasimama mbele ya Mungu kuhukumiwa kwa ajili ya dhambi zake. Je, unafikiri kwamba Mungu atakukubali wewe kwa jinsi ulivyo?

Petro: Ndiyo, Ninafikiria hivyo.

Andrea: Wewe ni mtu mzuri?

Petro: Ndiyo, nadhani ndivyo nilivyo.

Andrea: Inawezekana ni mzuri ukilinganishwa na watu wengine. Inawezekana ni mzuri kwa marafiki zako na familia yako. Lakini, je, unajua viwango ambavyo Mungu anavitumia? Biblia inatueleza sisi jinsi Mungu anavyohukumu wenye haki na wasiokuwa na haki. Kwa mfano, sehemu ya sheria zake inaitwa Amri Kumi za Mungu. Je, wewe unazijua Amri Kumi za Mungu?

Petro: Baadhi yake.

Andrea: Kwa mfano, amri moja inasema, "Usiseme uongo." Je, katika maisha yako hujawahi kamwe kusema jambo lolote ambalo halikuwa la ukweli?

Petro: Hakika ndiyo, kila mtu amewahi kufanya hivyo kwa wakati fulani.

Andrea: Lakini kusema uongo ni kuvunja amri ya Mungu. Amri nyingine inasema usiibe. Je, ulishawahi kuiba kitu chochote?

Petro: Vitu vidogo vidogo sana, na sijawahi kumfanya mtu akaumizwa kwa kuiba vitu hivyo kutoka kwake.

---

[144] Matendo 7:51-53
[145] Matendo 17:30-31

Andrea: Lakini Mungu hatuachii sisi tuamue kitu cha kuiba. Amri yake ni kwamba tusiibe. Amri nyingine ni kwamba tusilitaje jina la Bwana Mungu wetu bure, kulitaja bila kuonyesha unyenyekevu na heshima, au kulitumia kama neno la kulaani.

[Kila amri kutoka katika hizo Amri kumi za Mungu, zinaweza kutumika, lakini zote hazipaswi kutumika katika mazungumzo ya aina moja. Kuna mifano hapa chini.]

- Mungu anatuambia sisi kwamba tusiwe wazinzi, na Yesu akasema kwamba kumwangalia mwanamke kwa matamanio ni kufanya uzinzi ndani ya moyo wako.
- Mungu alisema tusiue, na Yesu akasema kumchukia mtu mwingine ni sawa na kuua ndani ya moyo.
- Mungu anatuambia sisi kwamba tuikumbuke Siku ya Bwana na kuitakasa. Je, umekuwa ukiitakasa Siku ya Bwana kila wiki?
- Mungu anatuambia sisi kwamba tusitamani mali za wengine, tusifikiri kwamba mali na vitu vingine vitatufanya sisi tuwe na furaha badala ya Mungu, tukitamani kuwa tungekuwa na vitu walivyo navyo watu wengine.
- Mungu anatuambia sisi kwamba tusiwe na miungu mingine, tusiruhusu kufanya kitu chochote kuwa chenye umuhimu kuliko yeye Mungu, ikimaanisha kwamba haturuhusu kitu chochote kituweke mbali na kumtii na kumwabudu Mungu kama anavyostahili.

[Baada ya kutumia amri kadhaa kuonyesha kwamba mwenye dhambi ana hatia, ndipo tunaenda kwenye hitimisho.]

Andrea: Kama leo hii Mungu atakuhukumu, hutafaulu. Utakuwa mwenye hatia kwa viwango vyake. Je, utataka kujua jinsi ya kupata msamaha ili kwamba usiwe na hofu ya hukumu ya Mungu?

[Kisha, mwinjilisti anaweza kumshirikisha injili na kumwalika mwenye dhambi kwenye hatua nyingine ya kuomba naye.]

► Wanafunzi wawili watapaswa kuonyesha mazungumzo ambayo mmoja anawakilisha injili kwa kutumia Amri kumi za Mungu. Kikundi kinaweza kujadili kuhusu onyesho lao. Wanafunzi watapaswa kugawanyika kwenye vikundi vya watu wawili wawili kwa ajili ya kufanya mazoezi ya jinsi ya kuwasilisha injili.

► Je, utajuaje kwamba uwasilishwaji wa injili ulikuwa wa mafanikio?

Ni wazi kwamba mtu anapochagua kutubu na kuokoka baada ya uwasilishaji wetu wa injili, tunajua kwa uhakika kwamba ulikuwa wa mafanikio. Lakini, hicho siyo kipimo pekee cha mafanikio. Mungu ndiye anayehusika katika kuharakisha ukweli ukae ndani ya moyo wa mtu. Kama uliwasilisha injili kwa njia ambayo msikilizaji alikuelewa, ulikamilisha jambo fulani la muhimu sana hata kama kamwe hukuona matokeo. Kama atajisikia kwamba una mzigo juu yake na una nia ya kutaka kumsaidia, jambo hilo ni jema pia. Kama alikuwa

mwenye hasira au mizaha, hiyo haina maana kwamba umeshindwa hasa zaidi kama alikasirika kwa ukweli aliousikia kutoka kwako. Mungu huheshimiwa kwa ujumbe wa injli; wakati unapouwakilisha, una mafanikio katika jambo fulani muhimu.

## Ukumbusho kwa Kiongozi wa Darasa

*Hii ni njia yenye ufanisi sana kwenye kuwasilisha injili. Ni muhimu kwa sababu wanafunzi hujifunza kuitumia. Kwenye darasa lako linalofuata, wape wanafunzi muda wa kuelezea uzoefu wao wakati watakapokuwa wakishirikisha injili kwa kutumia mbinu hii. Wape nafasi ya kutiana moyo na kushauri kila mmoja na mwenzake. Itakuwa ni jambo la busara sana kuchukua kipindi kizima kwa njia hii na kungojea hadi wakati mwingine wa kwenda kwenye somo linalofuata.*

## Kazi ya Kufanya

Wasilisha injili kwa angalao watu watatu kwa kutumia ile njia ya Andrea katika somo hili. Andika aya moja yenye kuelezea kila mazungumzo yanayofanyika. Jiandae kuelezea kuhusu hili kwenye kipindi cha darasa kitakachofuata.

# Somo la 9
# Uwasilishaji wa injili "Daraja"

## Utangulizi

*Kumbukumbu kwa Kiongozi wa Darasa: Mwanzoni mwa kipidi hiki, wanafunzi watapaswa kutoa taarifa ya uzoefu wao wa ushirikishaji wa Injili kwa kutumia mbinu iliyoko kwenye somo lililopita. Kumbuka kwamba wanafunzi wanahitaji kutiana moyo mmoja kwa mwingine. Kila mwanafunzi aliyeshirikisha injili amekamilisha jambo fulani la muhimu sana hata kama msikilizaji wake hakuonyesha uwajibikaji ulio chanya.*

*Kwenye maandalizi ya somo hili, hakikisha kwamba una ubao wa kuandikia kwa chaki, ubao mweupe au makaratasi makubwa kwa ajili ya kuelezea michoro kwa wanafunzi wa darasa.*

> Hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.[146]

► Je, kuna sababu gani aliyoitoa mtume kuhusiana na kushirikisha injili?

Tumepata uzoefu wa nini maana ya kukutana na Mungu na kuokoka, kwa ajili ya kuanzisha uhusiano pamoja naye. Pia tuna uhusiano na watu wengine ambao nao wako kwenye uhusiano na Mungu. Tunaposhirikisha injili, tunawakaribisha watu wengine kuja kwenye uhusiano ambao na sisi tunao pamoja na Mungu na wngine wanaomjua yeye.

## Kuwasilisha Injili

Uwasilishaji huu wa injili ni wa maneno machache na ya kukumbuka. Uwasilishaji unatumia mchoro ambao utaweza kukumbukwa na mtu yeyote anayeuona jinsi unavyowasilishwa.Unaweza ukawasilishwa kwa dakika mbili, au muda ukaongezwa kwa ajili ya majadiliano na utolewaji wa maelezo endapo msikilizaji ni mwenye uhitaji wa kusikia.

Siyo lazima uwe mchoraji mwenye ujuzi. Mchoro wenyewe ni mrahisi, na kutokana na urahisi wake kunamsaidia msikilizaji kuweza kukumbuka.

Sasa tutaenda kwenye hatua za uchoraji, pamoja na maelezo ya maneno yatakayokwenda na kila sehemu itakayochorwa.

*Kumbukumbu kwa Kiongozi wa Darasa: Onyesha uwasilishaji wakati wanafunzi wakiwa wanaangalia.* ***Jitahidi usiongeze maneno ya ziada kwenye uwasilishaji wako.***

[146] 1 Yohana 1:3


***Uwasilishaji unapaswa uwe mfupi ili wanafunzi waweze kujifunza kwa urahisi.*** *Wanafunzi hawapaswi kuandika kwenye mchoro wakati wakiwa wanaangalia ukitolewa maelezo kwa mara ya kwanza.*

*Katika kutoa maelezo kwa mara ya pili, wanafunzi watapaswa kuchora kila hatua ya mchoro wakati kiongozi wa darasa atakavyokuwa anauchora kwenye karatasi au ubao mkubwa zaidi ambao darasa wataona. Usijaribu kuongeza maelezo ya ziada kwenye uwasilishaji. Baada ya maelezo ya mara ya pili, wanafunzi wataendelea kugundua maelezo yaliyotolewa kwenye sehemu ya pili, kisha watarejea tena nyuma kufanyia mazoezi uwasilishaji.*

**Kitu cha kusema kwenye kila sehemu ya Mchoro**


Sehemu ya 1

“Mungu alimwumba kila mtu awe kwenye uhusiano pamoja naye na kuishi maisha yaliyobarikiwa. Hakupanga maisha yawe ni ya matatizo na mateso chungu zima.”




Sehemu ya 2


“Mwanadamu ametenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Watu wa mwanzo walitenda dhambi, na tangu hapo kila mtu ametenda dhambi dhidi ya Mungu.”



Sehemu ya 3

“Mungu ni hakimu wa haki, na siku moja wenye dhambi watahukumiwa kwenda kwenye moto wa milele isipokuwa wawe wametafuta rehema za Mungu na kurejea kwenye uhusiano tena pamoja na Mungu.”


[Chora mshale na andika neno “motoni.”]




Sehemu ya 4

“Hakuna lolote tunaloweza kulifanya kwa ajili ya kuturejesha tena upya kwa Mungu au kupata rehema – siyo kwa matendo mema, siyo kwa kwenda kanisani, siyo taratibu za kimadhehebu, na wala siyo kutoa fedha....”


[Chora mshale kuonyesha kila kilichotajwa kwenye orodha.]



Sehemu ya 5

“Hali yetu ingekuwa mbaya sana kama Mungu hangefanya njia kwa ajili yetu ya kurejea kwake. Yesu, Mwana wa Mungu alikufa juu ya msalaba ili tuweze kusamehewa. Baada ya siku tatu, alifufuka kutoka kwa wafu.”


[Chora msalaba.]




Sehemu ya 6

“Lakini haitoshi tu kujua haya. Kila mtu binafsi atapaswa kufanya chaguo la kuokoka na kurejea tena kwa Mungu. Mtu ni lazima atubu, ikimaanisha kwamba ni kujutia kikamilifu kuhusu dhambi na kuwa tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana nazo. Mtu anayetubu anaweza kupata msamaha kwa kumsihi Mungu kwenye maombi.”

[Chora mshale kisha andika maneno “tubu” na “pokea.”]




Sehemu ya 7

"Ni wapi unapofikiri kwamba upo katika mchoro huu? Je, kumewahi kutokea kuwepo na muda maalumu katika maisha yako ambao ulitubu dhambi zako, ukapokea msamaha wa Mungu, na ukaanza kuishi kwa ajili ya Mungu; au bado umetengwa na Mungu kutokana na dhambi yako?”

[Subiri kupata jibu. Watu wengi watakiri kwamba bado wametengwa na Mungu.]

"Uko tayari kufuata hatua hii—Kutubu, kupokea msamaha, na kuanza kuishi kwa ajili ya Mungu? Nitapendezwa sana kuomba pamoja nanyi sasa hivi."

[Fanya maombi yanayokaribia kufanana na haya yafuatayo.]

"Bwana, ninajua mimi ni mwenye dhambi na ninayestahili adhabu ya milele. Ninajutia dhambi zangu na niko tayri kuachana nazo. Ninaomba unisamehe, siyo kwa sababu ninastahili, bali kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yangu. Asante kwa wokovu wako. Kuanzia sasa, nitaishi kwa ajili yako tu."

**Maelezo**

Sehemu ya 1

Mwanzo wa kuwasilisha unaweza kurekebishwa ili kuendana na mahitaji ya msikilizaji. Badala ya "maisha yawe ni ya matatizo na mateso chungu zima" mwinjilisti anaweza kutumia kitu kingine cha uhakika zaidi ambacho kitafanana na uzoefu wa msikilzaji.

Sehemu ya 2

Ni muhimu kwa msilizaji wako kutambua kwamba yeye binafsi ni mwenye hatia kutokana na dhambi na ametengwa na Mungu. Hayuko kwenye hali ambayo imetokana na dhambi ya Adamu.

Sehemu ya 3

Hii inaonyesha hali mbaya ya mwenye dhambi.

Sehemu ya 4

Kusudi la sehemu hii ni kumwonyesha msikilizaji kwamba hapaswi kuweka utii wake kwenye kitu kinachopotosha kwa ajili ya wokovu. Sehemu hii inaweza kutumika katika kufananisha na mahitaji ya msikilizaji. Mwinjilisti atapaswa ajitahidi kutaja vitu ambavyo inawezekana msikilizaji akaweka utii kwake.

Sehemu ya 5

Njia rahisi ya kuelezea mateso na kifo cha Yesu msalabanini kusema kwamba "Yesu alikufa juu ya msalaba kama dhabihu ili kwamba tuweze kupata msamaha." Kusudi la sehemu hii ni kumsaidia msikilizaji ajue kwamba anapaswa kutegemea kwenye wokovu ambao Mungu aliutoa.

Sehemu ya 6

Mwinjilisti anajaribu kumleta msikilizaji kwenye kipindi cha kuweza kufanya maamuzi. Msikilizaji anahitaji kutambua kwamba atapaswa afanye maamuzi binafsi. Anahitajika afahamu tafsiri sahihi ya toba, ili awze kujua kwamba toba ni zaidi ya kuwa na majuto na ni zaidi ya kusema anaomba samahani. Anahitajika ajue kwamba anapaswa aombe ili amsihi Mungu kwa ajili ya msamaha.

Sehemu ya 7

Kwenye hatua hii, Mwinjilisti anajaribu kumleta msikilizaji kwenye kukiri hitaji lake la kuokoka. Uwasilishaji umepangwa katika kumsaidia mtu ambaye hajaokoka kutambua kuwa bado hajaokoka. Swali limeandliwa kwa umakini mkubwa sana. Watu wengi wanafikiri wanaweza kila siku wakaomba kwa ajili ya msamaha wakati wanaendelea kuishi kwenye maisha ya dhambi. Swali linauliza kuhusu muda maalumu ambao mtu anaokoka na kuhusu maisha mapya anayoanza. Anatakiwa atambue kwamba kama bado hajawahi kuwa na uzoefu wa mabadiliko, ametengwa na Mungu kwa dhambi yake. Kisha mwinjilisti atapendekeza kufanya maombi pamoja naye kwa ajili ya wokovu.

Kama msikilizaji haelewi hitaji lake au hayuko tayari kutubu, mwinjilisti asimhimize kuingia kwenye maombi. Kama atajilazimisha kuomba bila ya kutubu kwa kumaanisha na kujionea mabadiliko, anaweza akawa na wokovu wa uongo au anaweza akaamini kwamba mabadiliko hayawezi yakatokea kwake. Kwa vyovyote vile, inawezekana asije kuokoka hapo baadaye.

Mchoro unaweza kuwasilishwa kwa haraka. Kama unayo nafasi ya kushirikisha injili, kwa wepesi tu unaweza ukauliza, "Je, ninaweza kuchukua angalau dakika mbili za kukuonyesha mchoro unaoelezea kile ambacho Biblia inaelezea kwamba ni njia ya kujua kwa uhakika kama kweli umeokoka? Kwa hatua hiyo kunamfanya mtu ajue kwamba hutaenda kutumia muda wake mwingi. Kama ataonyesha kuvutiwa na anataka kuzungumzia kuhusu hiyo, hapo unaweza kuchukua muda mrefu zaidi.

Kwa kawaida, watu wengi huvutiwa na michoro. Mara nyingi mtu ataomba kuuhifadhi mchoro huo baada ya mwinjilisti kumaliza huduma.

### Kumbukumbu kwa Kiongozi wa darasa

*Onesha uwasilishaji tena kwa mara kadhaai. Epuka kuingiza ushauri wa zida au ufafanuzi kwenye uwasilishaji kwa sababu wanafunzi watajifunza kwa urahisi zaidi kama utakuwa mfupi. Baada ya maonesho kadhaa, wanafunzi baadhi wanaweza wakafanya maonesho kwa kubadilishana kwenye kikundi, wakati wanafunzi wenzao katika kikundi wakiwasaidia kukumbuka mambo muhimu kwa undani zaidi. Kisha, wanafunzi wanaweza wakagawanyika kwenye vikundi vya watu wawili wawili na kufanya mazoezi ya uwasilishaji kila mmoja na mwenzake.*

### Kazi za Kufanya

(1) Wasilisha injili kwa kutumia daraja la mchoro kwa angalau watu watatu ambao hawajaamini. Andika aya moja kuelezea kila uzoefu na ujiandae kuelezea kuhusu uzoefu huo kwenye kipindi kingine cha darasa kitakachofuata.

(2) Katika maandalizi ya somo litakalofuata, soma na utafakari katika Warumi 1-3, Warumi 5, na Warumi 10.

# Somo la 10
# Barabara ya Kirumi

## Kumbukumbu kwa Kiongozi wa Darasa

*Watake wanafunzi watoe taarifa zao za uwasilishaji wa injili kwa kutumia daraja la mchoro.*

## Utangulizi kuhusiana na Kitabu cha Warumi

Paulo alipanga kufanya safari ya kwenda Rumi. Alikuwa anahitaji kwenda kuhubiri injili katika eneo hilo,[147] kuwaimarisha waamini,[148] na ili kupata msaada wa kanisa la Rumi kwa ajili ya safari yake ya umisheni ya kwenda Hispania.[149]

Kusudi la barua kwa Warumi ilikuwa ni kumtambulisha Paulo na theolojia yake ya wokovu kwa waamini wa Kirumi. Barua inaonesha misingi ya kazi ya umishenari duniani kote kwa kuelezea thelojia ya wokovu.

Paulo alipanga kulitumia kanisa la pale Rumi kama kituo chake cha kuzindulia juhudi za umishenari katika nchi ya Hispania, amabyo ilikuwa ni koloni la zamani la Kirumi katika eneo la magharibi na kitovu cha ustaarabu wa Kirumi katika eneo hilo la Dunia wakati huo.

Ziara ya Paulo Rumi haikutokea kama alivyokuwa amepanga. Alikamatwa akiwa Yerusalemu. Ilipoonekana kwamba hatapata haki, alikata rufaa kwa Kaisari. Baada ya safari ndefu ya hatari, iliyokuwa ni pamoja na kuvunjika kwa meli yake alifika Rumi kama mfungwa mwaka wa 60 B.K. Ingawaje alikuwa amefungwa, alikuwa huru kupokea wageni, na alikuwa na huduma yake ambayo ilifika katika jiji lote.[150] Paulo alisema kwamba mfuatano wa matukio hayo ulitokea kwa ajili ya “kupeleka injili mbele."[151] Kulikuwa na watu wapya ambao walishabadilika hata katika nyumba ya Kaisari. Aliachiliwa baada ya miaka miwili. Haijulikani kama alifanikisha kuendelea na safari yake ya kwenda Hispania au la.

Kuna maswali kadhaa ambayo katika hali ya kawaida yatainuka kuhusiana na ombi la Paulo kwamba asaidiwe kuzindua safari yake ya umishenari. Mtu anaweza akauliza, “Kwa nini uwe wewe ndiye unayetaka uende?” Kwa hiyo, Paulo alianza barua yake kwa kutaja

[147] Warumi 1:15
[148] Warumi 1:11-12
[149] Warumi 15:24
[150] Matendo 28:30-31
[151] Wafilipi 1:12

kujitoa kwake kwa ajili ya kazi ya umisheni.[152] Baadaye alielezea wito wake maalumu kama mtume kwa Mataifa.[153]

Swali lingine ambalo linaweza kuulizwa ni, "Je, kwa nini kila mtu anataka aisikie injili? Inawezekana ujumbe huu hautakiwi kila mahali." Paulo alifafanua uzito wa injili kwa mwanadamu katika ulimwengu wote[154] na uharaka uliopo wa kazi ya umishenari.[155] Alionesha kwamba ujumbe unahusika kwa kila mtu ulimwenguni na kwamba kila mtu ana hitaji kubwa la kuusikia.

## Kitabu cha Warumi kuanzia Wakati Ule hadi Sasa

Waraka huu bado unatimiza kusudi lake la awali la kutoa msingi wa kazi ya umishenari. Hata hivyo, unafanya kazi ya ziada. Kama Paulo alivyoelezea ni kwa nini kila mtu anahitaji kusikia ujumbe, alieleza kwamba ujumbe ni nini na ni kwa nini watu wanaweza tu wakaokolewa kwa njia hii. Alijibu baadhi ya upinzani wa kawaida. Maelezo haya na utetezi wa ujumbe aliohubiri unachukua sehemu kubwa ya kitabu na unatoa muundo wake.

Tunachokipata katika kitabu cha Warumi ni maelezo ya theolojia ya wokovu. Theolojia ya wokovu ya Paulo inayotetewa kwenye waraka ilitoa ulinzi wa mara moja dhidi ya Wayahudi; na unatumika pia katika kusahihisha makosa ya wakati wa sasa katika elimu ya wokovu (imani za wokovu).

William Tyndale, kwenye utangulizi wa kitabu cha Warumi, alisema, "Wazo kuu la Paulo katika waraka huu lilikuwa ni kutambua na kutoa kwa ufupi mafunzo yote ya injili ya Kristo na kuandaa utangulizi kutokana na yale yote yaliyohusika na Agano la Kale."[156]

Kupitia katika historia, Mungu ameutumia waraka wa Warumi kurejesha kwa upya kweli nyingi zilizokuwa muhimu wakati zilipokuwa zimesahaulika.

Katika mwaka wa 386, Agustino alijiondoa kwenye maisha yake ya dhambi baada ya kuwa amesoma Warumi 13:13-14.

Katika mwaka wa 1515, Martin Luther alitambua maana iliyokuweko katika Warumi 1:17. Aliona kwamba mtu atakayeachwa kwenye hukumu ya Mungu ni Yule aliye na imani iokoayo. Jambo hili lilimpa msingi wa uhakika wa wokovu ambalo kwa muda mrefu alikuwa amelihitaji. Ilikuja kuwa ndio msingi wa ujumbe wake kwamba imani peke yake ndio njia inayoweza kutufanya tuokoke.

Katika mwaka wa 1738, John Wesley alipata uhakika wa wokovu alipokuwa kwenye kikao na vijana wadogo waliokuwa wanakutana mara kwa mara kujadili jinsi ya kufuata Ukristo wa kimaandiko. Wakati mtu mmoja alipokuwa akisoma Utangulizi wa Luther kwa kitabu

---

[152] Warumi 1:1
[153] Warumi 15:15-20
[154] Warumi 1:14, 16; Warumi 10:12
[155] Warumi 10:14-15
[156] William Tyndale, "Prologue to Romans," *English New Testament*, 1534.

cha Warumi, Wesley alijisikia moyoni mwake "moto wa ajabu ukiwaka." "Nilijihisi kuwa mtiifu kwa Kristo, Kristo peke yake, kwa ajili ya wokovu wangu: na uhakika ulitolewa kwangu kwamba amezifuta dhambi *zangu,* hata *mimi,* na akaniokoa kutoka katika sheria ya dhambi na mauti."[157]

Kwa hawa watu wote watatu, kuelewa ujumbe wa kitabu cha Warumi kulikuwa ni motisha kamili ya kufanya uinjilisti kwa ari kubwa. Kitabu hiki bado kinakamilisha kusudi lake la kutoa msingi kwa ajili ya umisheni kwa kuelezea theolojia ya wokovu.

***Kitabu chote cha Warumi ni ufafanuzi wa maelezo yote yaliyoko katika Warumi 1:16-18.***

Kila kitu kwenye aya 1-14 ni mwendelezo hadi aya ya 15 ambapo Paulo anasema, "Niko tayari kuhubiri injili," Aya za 16-18 zinaelezea kwa muhtasari injili ni nini na ni kwa nini kila mtu anaihitaji. Injili ni ujumbe ambao wenye dhambi wanaweza kuhesabiwa haki kwa imani. Sababu iliyopo ya kila mtu kuhitaji ujumbe huu ni kwamba wako chini ya laana ya Mungu.

"Kusudio la ujumla la waraka huu ni kuudhihirisha umilele, kusudi lisilobadilika au tamko la Mungu, ambalo ni, 'Kila aaminiye ataokoka: na kila asiyeamini atahukumiwa."
- John Wesley

**Njia nyingine ya kuelezea kusudi la msingi la kitabu cha Warumi ni kwamba ni ufafanuzi wa injili, iliyo katika msingi wa tamko la Mungu kwamba kila aaminiye ataokoka, na kila asiyeamini atahukumiwa.**

Kilele cha kitabu kiko kwenye Warumi 10:13-15, ambapo Paulo anaelezea kwa nini ni jambo la haraka kwa wajumbe kupeleka injili. Watu wanaokoka kwa kuamini, lakini hawawezi kuamini pasipo kuisikia injili.

### Uwasilishaji wa Injili kutoka katika Kitabu cha warumi

Injili inaweza kufafanuliwa kwa kutumia aya peke yake kutoka katika kitabu cha Warumi. Uwasilishaji huu wa injili mara nyingine unaitwa "Barabara ya Kirumi."

Sentensi ya kwanza ya ufafanuzi kwa kila kinachorejewa ni jambo muhimu sana la kukumbuka.

[157] John Wesley, *The Works of John Wesley,* (Kansas City: Nazarene Publishing House, n.d.), 103.

**Warumi 3:23**

"Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

**Kila mtu amefanya dhambi kwa kufanya mambo anayojua kwamba ni uovu.** Aya hii inaonyesha tatizo halisi watu walilo nalo. Hawajamtii Mungu; kwa makusudi wamekataa kumtii Mungu. Hakuna hata mtu mmoja ambaye anaweza kuepukana na hili. Hakuna mtu ambaye anaweza kukubaliwa na Mungu kwa msingi kwamba mara zote anatenda yaliyo mema.

Kwa msisitizo zaidi katika suala hili, unaweza ukatumia Warumi 3:10 ("Hakuna mwenye haki hata mmoja.") na Warumi 5:12 ("mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi").

**Warumi 6:23**

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

**Wenye dhambi wamevuna kifo cha milele, lakini Mungu anatoa maisha ya milele kama zawadi kupitia kwa Yesu.**

Aya hii inaonyesha ni kwa jinsi gani dhambi ilivyo na madhara makubwa. Kwa sababu ya dhambi, adhabu ya kifo imepitishwa kwa kila mtu. Ni kifo cha milele, adhabu ya Mungu ambayo kila mwenye dhambi anastahili.

Kwa ulinganifu wa kifo ambacho tulikivuna, Mungu anatoa zawadi ya maisha, kitu ambacho hatujawahi kukivuna.

**Warumi 5:8**

"Bali Mungu aonesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu."

**Zawadi ya Mungu ilitolewa kwa kifo cha Kristo kwa sababu yetu.**

Mungu alikuwa hayuko tayari kutuachia sisi tuchukue hukumu tuliyostahili. Kwa kuwa anatupenda, aliandaa njia kwa ajili yetu ya kupokea rehema. Yesu alikufa kama dhabihu ili kwamba tuweze kupokea msamaha. Mungu hakutungojea sisi tufanye jambo lolote linalostahili wokovu – lilikuja tu kwetu "tukiwa wangali bado wenye dhambi." Wokovu hautolewi kwa watu wema, bali kwa wenye dambi.

**Warumi 10:9**

“Kwa sababu, ukimkiri Yesu… na kuamini… utaokoka.”

**Hitaji peke yake kwa ajili ya wokovu ni kwa mwenye dhambi kukiri kwamba yeye ni mwenye dhambi na aamini ahadi ya Mungu ya msamaha kwa sababu ya kifo na kufufuka kwa Yesu.**

Vipi kuhusu toba? Kama mtu atakiri kwamba amefanya makosa na anahitaji asamehewe, inaonyesha kwamba huyu mtu yuko tayari kuachana na dhambi kwa hiari yake mwenyewe.

**Warumi 10:13**

“Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.”

**Sadaka ya wokovu ni kwa ajili ya kila mtu.**

Hakuna mtu hata mmoja aliyetengwaa katika hili. Hakuna sifa nyingine zozote zinazohitajika.

**Warumi 5:1**

“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu.”

**Kuamini ahadi ya Mungu kunatufanya sisi tuwe rafiki wa Mungu, hatuhesabiwi wenye hatia tena.**

Kuwa na amani na Mungu inamaanisha kwamba sisi siyo maadui wa Mungu tena; tumepatanishwa. Dhambi ambayo ilitutenganisha na Mungu inaondolewa kwenye njia zetu. Kuhesabiwa haki inamaanisha kwamba tunahesabika hatuna hatia tena. Kuhesabiwa wenye haki kwa imani ina maana kwamba kuamini ahadi ya Mungu ndiyo kitu peke yake muhimu kinachohitajika kwa ajili ya msamaha wetu.

**Warumi 8:1**

“Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.”

**Kwa kuwa tumeunganishwa kwa Kristo, hatuna hukumu tena kwa dhambi tulizotenda.**

Yesu aliishi maisha yasiyokuwa na dhambi na akakamilisha mahitaji yote ya haki kwa kifo chake juu ya msalaba. Kwa imani, tunajinasibisha naye, na tumekubaliwa na Mungu aliye Baba yetu. Mungu anawajibika na sisi kana kwamba hatujawahi kutenda dhambi tena.

**Hitimisho**

Elezea kwamba mwenye dhambi anaweza akaokoka kwa kumwomba Mungu, akikiri kwamba yeye ni mwenye dhambi na akiomba msamaha kwenye msingi wa dhabihu ya kifo cha Yesu na kufufuka kwake.

## Kwa ajili ya Kujifunza na kufanya Mazoezi

Njia nzuri ya kujifunza na kufanyia mazoezi mbinu hii kwanza ni kuweka alama kwenye kila aya itakayotumika katika kitabu cha Warumi kwa kuzungushia alama ya mviringo au kwa kupiga msatari. Kisha weka namba pembeni mwa kila kimoja kuonesha mtiririko wa matumizi yake. Kwa mfano: nyuma ya aya itakayonza kutumika kwanza, andika namba 1.

Fanya zoezi la kuwasilisha injili. Soma kila aya na toa maelezo yanayoendana na aya hiyo. Uwe na uhakika wa kuingiza maudhui yaliyoko kwenye sentensi ya kwanza baada ya kila aya. Ongeza hitaji lolote la maelezo yanayohitajika, kwa kutumia sentensi zinazofuata kama inaonekana zitakuwa na msaada. Siyo lazima kutumia maneno yale yale ambayo yametolewa kwenye somo hili.

Fanya mazoezi hadi utakapoona unaweza kufanya vyema bila ya kuangalia mahali pengine popote isipokuwa Biblia tu.

*Kumbukumbu kwa kiongozi wa darasa: Wanafunzi wawili au watatu watapaswa kuonesha matumizi ya Barabara ya Kirumi kwenye kikundi. Kikundi kitajadili njia ambazo wanaweza kuboresha katika uwasilishaji. Kisha, wanafunzi itabidi wagawanyike kwenye kikundi cha watu wawili wawil kwa ajili ya kufanya mazoezi. Kila mwanafunzi atapaswa kufanya uwasilishaji mara mbili, kwa wasikilizaji tofauti.*

## Kazi za Kufanya

(1) Kwa kutumia Barabara ya Kirumi, wasilisha injili kwa angalau watu watatu. Andika aya moja kuhusiana na kila wasilisho ulilofanya na jiandae kutolea maelezo wakati utakapokuja kwenye kipindi kingine cha darasa kinachofuata.

(2) Jipange kuandika kutoka kwenye kumbukumbu zako (kwa kutumia Biblia yako tu) marejeo ya Maandiko ya Barabara ya Kirumi na angalao sentensi moja yenye maelezo ya kila kimoja mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.

(3) Somo linalofuata ni kuhusu mahubiri ya Kiuinjilisti. Kwa ajili ya maandalizi ya somo hili, andika muhtasari wa mahubiri ya kiuinjilisti ambayo ulishawahi kuyahubiri, moja ambalo umeshahi kulisikia, au moja ambalo utapenda kulitengeneza mwenyewe. Njoo pamoja nalo kwenye kipindi kingine cha darasa kinachofuata.

**Mtihani**

Andika kumbukumbu ya Maandiko yanayotumika katika uwasilishaji wa injili ya Barabara ya Kirumi. Chini ya kumbukumbu hizo, andika angalau sentensi moja yenye ufafanuzi. Usiziandike hizo aya.

(1) Warumi _______

(2) Warumi _______

(3) Warumi _______

(4) Warumi _______

(5) Warumi _______

(6) Warumi _______

(7) Warumi _______

# Somo la 11
# Kuhubiri Kiuinjilisti

## Utangulizi

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 1:17-25 kwa ajili ya kikundi. Je, mbinu ya Mungu ya kuokoa watu waliopotea ni ipi?

Wayahudi walikuwa wanatafuta nguvu za kulikomboa taifa lao. Walihitaji ujumbe wa nguvu pamoja na alama za nguvu kuthibitisha kwamba itafanya kazi.

Mataifa walikuwa wanatafuta hekima ya kuelewa maisha na kwa ajili ya kupata mafanikio katika dunia. Walihitaji ujumbe ambao ungewafafanulia jinsi ya kupata kile walichokuwa wanahitaji.

Msalaba uliwakilisha kujisalimisha na dhabihu. Kwa Wayahudi ambao walikuwa wanataka nguvu, ilionekana kama ni udhaifu. Kwa Mataifa ambao walitaka hekima ya kidunia, ilionekana kama ni upumbavu. Kiuhalisia, nguvu na hekima ya Mungu ilidhihirishwa katika kifo cha Kristo. Msalaba ulionekana kama ni udhaifu na upumbavu wa Mungu, lakini ulikuwa ni bora zaidi kuliko juhudi nyingi sana za wanadamu.

Ujumbe wa injili uko kinyume na vitu, na tamaa za dhambi za kibinadamu. Unatoa wito wa kutubu na kujisalimisha kwa Mungu. Unaonekana kama ni ujumbe wa kipumbavu, kwa sababu watu wanataka kusikia kuhusu jinsi ya kupata kile wanachokitaka.

Mungu amechagua kutumia injili kwa ajili ya kuokoa watu. Ametoa jukumu la mawasiliano kwa waamini. Neno *kuhubiri* halina maana ya kurejelea kwa mtu anayezungumza na umati wa watu tu, bali ni kwa mawasiliano ya injili kwa njia mbalimbali. Kiini cha kifungu siyo kwamba kuhubiri hadharani ndiyo mbinu ya Mungu iliyochaguliwa. Kiini ni kwamba injili ni mbinu ya Mungu.

► Je, kifungu kinamaanisha nini kinaposema kwamba kuhubiri kuhusu msalaba ni upumbavu kwa wale wasioamini?

## Kufafanua kuhusa Kuhubiri Kiuinjilisti

Neno *kuhubiri* linaweza kutumika katika ufahamu mpana zaidi katika kurejelea kwenye aina mbalimbali za kuwasilisha Neno la Mungu. Hata hivyo, kwenye somo hili, tutatumia neno *kuhubiri* katika hali yake ya kawaida: ikirejelea kwa mtu kuzungumza Neno la Mungu kwenye kongamano la watu.

Kuhubiri Kiuinjilisti ni wakati ambapo injili inawasilishwa kwenye kongamano la watu. Siyo tu hali ya kuwasilisha kichwa cha habari chochote au kifungu cha Maandiko. Ni uwasilishaji wa injili.

Mhubiri wa kiinjili kwa kawaida hushawishi wasikilizaji wake kuchukua hatua za mara moja kutokana na ujumbe, kwa lengo kwamba watabadilika mara moja. Ujumbe umeandaliwa kwa ajili ya kuwaleta kwenye huo uamuzi.

Taarifa iliyoko kwenye ujumbe wa kiinjili unachambuliwa kwa umakini sana. Kusudi la ujumbe kimsingi siyo kwa ajili ya elimu, Mhubiri hujaribu kutoa taarifa ambayo wasikilizaji wanaihitaji kwa ajili ya kufanya maamuzi na kubadilika. Taarifa hii huhusisha pamoja na ufafanuzi wa injili ya msingi, jinsi msikilizaji atakavyokuwa na mwitikio, na uwezekano wa madhara ya uamuzi.

Mahubiri yanaweza yakafanyika kwenye eneo lenye ukimya, lililopangika vizuri kama vile kusanyiko la wafuasi wa kanisa kwenye jengo la kanisa au kwenye eneo lingine lenye umati mkubwa wa watu waliokusanyika kwa ajili ya malengo mengine. Inawezekana kusanyiko likawa rafiki na ujumbe wa injili, au wanaweza wasikubali.

► Je, ni maeneo gani tofauti yaliyoandaliwa ambayo umewahi kuona injili ikihubiriwa?

## Miongozo kuhusiana na Kuhubiri Kiuinjilisti

Kwa kuwa kuna tofauti kati ya kuhubiri ndani ya kanisa na kuhubiri kwenye kikundi kingine kilicho tofauti, kwanza tutatoa miongozo ambayo inatumika kwenye mahubiri ya kiuinjilsti katika kanisa. Kwenye sehemu nyingine huko mbele ya somo hili, tutatoa baadhi ya miongozo ambayo inatumika kwenye mahubiri ya nje.

### (1) Elezea kwa kinaganaga kifungu cha andiko.

Neno la Mungu lina nguvu sana, kwa hiyo mhubiri anahitajika kulitumia. Siyo lazima kwamba kifungu kiwe kirefu sana au mhubiri atumie muda mrefu akielezea kwa undani kilichopo. Anapaswa atumie Maandiko yanayounga mkono ujumbe wa injili. Anapaswa ahakikishe kwamba kauli zake nyingi anazozitoa zina msingi wa Maandiko, ili nguvu ya Neno la Mungu iweze kutumika. Hapaswi kuchagua sehemu ya aya kwa ajili ya kutumia kwenye maana nyingine tofauti na ile maana iliyoko kwenye maudhui yake.

### (2) Unapaswa afafanue maana za maneno *toba* na *imani.*

Wasikilizaji wanaweza wakawa na mawazo potofu kuhusiana na maana za maneno haya. Wanaweza wakafikiri kwamba toba maana yake ni kufanya maisha yako yawe mazuri zaidi ili uweze kukubalika na Mungu. Wanahitaji kujua kwamba toba maana yake ni kuwa na majuto ya kutosha kutokana na dhambi zako kiasi kwamba uko tayari uondolewe kutoka katika hizo dhambi.

Wasikilizaji wanaweza kufikiri kwamba imani maana yake ni kuamini katika dini au kutekeleza mila na taratibu za dini. Wanahitaji kujua kwamba imani inayookoa inakufanya uweke utiifu wako kabisa kwenye kifo na mateso ya Kristo msalabani kwa ajili ya wokovu.

**(3) Sisitiza kwamba mtu huwa ni Mkristo mara tu anapookoka.**

Watu wengi wana mawazo potofu kuhusu nini maana ya kuwa Mkristo na ni kwa jinsi gani mtu anaweza akawa Mkristo. Wanaweza wakadhania kwamba mhubiri anawataka tu wazidi kuwa watu wa dini au wawe sehemu ya kanisa. Wanaweza wakafikiri kwamba anawataka tu waanze kuishi maisha ya utiisho mkali. Sisitiza kwamba wakati wa mabadiliko mwenye dhambi hutubu, akapokea msamaha, na kuanza uhusiano wake binafsi na Mungu.

**(4) Kataa au pinga sababu za kupotosha walizo nazo watu kwa kukiri kuwa ni Wakristo.**

Kwnye jamii kadhaa, watu wengi wanafikiri kwamba wao ni Wakristo. Wanaweza wakafikiri kwamba wao ni Wakristo kwa sababu wamekuweko makanisani, wamefanya matendo mema, wanaamini baadhi ya mambo, au wamekuwa na uzoefu kidogo wa kiroho. Mbali na kusisitiza mabadiliko, elezea maisha yenye uhusiano na Mungu na utii unaotakiwa ambao unafuata baada ya kufanya toba.

**(5) Hakikisha kwamba watu wasiokuwa wa makanisa wanakuelewa.**

Usitumie maneno ambayo watu wa kidini tu ndio wanaoyafahamu. Usirejelee kwenye mila na taratibu za kidini ambazo hawawezi kuzielewa.

► Je, ni baadhi ya maneno gani yanayotumika katika kanisa lako ambayo watu katika ujirani wako wanaweza wasielewe?

**(6) Toa msamaha, uhusiano na Mungu, na uzima wa milele**.

Hizi ndizo faida muhimu zaidi za kuokolewa. Onyesha uzito wa hali ya mtenda-dhambi kwa kueleza hukumu na adhabu ya milele itakayowapata watenda-dhambi.

**(7) Epuka kutoa ahadi za mafanikio ambazo hazijawahi kuahidiwa kwenye injili.**

Kama watu wanafikiri kwamba kuokoka kunahusisha pamoja na kupata faida ya mali kutoka kwa Mungu au kanisa, mafanikio, kuponywa magonjwa, au aina nyingine yeyote ya kuendeleza hali ya maisha, watakuwa wamejaribu kupata hizo faida bila ya kutubu kwa uhakika.

Unaweza ukaelezea kwamba wakati Mungu akiwa katika uthibiti wa maisha ya mwanadamu, ataongoza, atabariki, na atakuwa ni msaada kwenye matatizo yao. Hata hivyo, hatupaswi kutoa ahadi kwamba matatizo yao yote yatatatuliwa kama watakuwa Wakristo. Kwa baadhi ya watu wengine, maisha yanaweza kuwa magumu zaidi kwa sababu ya mateso.

**(8) Usiunganishe kuokoka kwa mtu na uanachama wa kanisa la mahali pamoja.**

Uanachama wa kanisa utapatikana mara tu baada ya mtu kubadilika kwa ukweli, lakini vigezo vya uanachama vinahitajika vielezwe baada ya mabadiliko. Usizungumzie kuhusu

mahitaji ya kuwa mwanachama wakati unapojaribu kumshawishi mtu aweze kutubu dhambi zake. Mwinjilisti atapaswa kujielekeza katika kumleta msikilizaji kwenye kukutana na Mungu.

► Je, kuna baadhi ya mahitaji gani ya uanachama katika kanisa lako ambayo siyo muhimu kwa ajili ya kuokoka?

**(9) Usiweke viwango kwa ajili ya mabadiliko yanayoendana na kukua.**

Mwite msikilizaji ajitokeze kwa ajili ya kutubu dhambi zake anazozifahamu. Usimweleze masharti kuhusiana na undani wa maisha ambayo hatawza kuelewa hadi hapo atakapokuwa amekuwa Mkristo kamili kwa muda fulani. Wito wa toba na imani una matatizo ya kutosha. Usiongeze matatizo yatakayoweza kumfanya mtu aikatae injili.

**(10) Fafanua unataka watu wafanye nini.**

Usitake kudhania kwamba msikilizaji anajua kwamba anapaswa kuomba na kumsihi Mungu kwa ajili ya msamaha. Usitake kudhania kwamba anajua jinsi ya kujitokeza mbele na kupiga magoti. Wakati unapowaalika wasikilizaji ili wajitokeze, wafafanulie kabisa ni kitu gani unataka wafanye. Tafakari ni kwa jinsi gani utafanya mambo yawe mepesi kwa kadri itakavyowezekana kwa mtu ambaye ni mwepesi kutishwa na mazingira ya kanisa.

## Kuomba na wenye Mahitaji

Watu wanaweza wakakusanyika kuomba madhabahuni kwa sababu nyingi. Mara nyingine mchungaji anaweza akawaalika watu kwa ajili kuombea mahitaji mbalimbali. Miongozo iliyoorodheshwa hapa haimaanishi kwamba ni lazima itumike kwenye nyakati zote za maombi ya madhabahuni. Miongozi hii inatumika katika kuomba pamoja na wale ambao wameitikia wito wa mwaliko baada ya mahubiri ya kiuinjilisti.

Mchungaji anapaswa ahakikishe kwamba baadhi ya watu wa kanisa wamefundishika katika kuwasaidia watu wanaoomba kwa ajili ya kuokoka. Atapaswa kuwa na watu hawa wakiwa wamejiandaa kusaidia wakati atakapotoa wito wa mwaliko wa kiuinjilisti.

Mara nyingine mtu anayetaka kusaidia kuomba na watu wengine anakuwa ni kikwazo badala ya msaada. Mchungaji atapaswa kuyaangalia matatizo akiwa madhabahuni na kuwa tayari kutoa msaada. Kama mtu anakuwa kikwazo kwenye muda wa maombi madhabahuni kwa tabia isiyokuwa ya hekima au ushauri mbaya, mchungaji atafanya kila linalowezekana kusahihisha tatizo hilo.

Tunaamini kwamba mtu anaweza kutubu, akaamini, na kujionea mabadiliko mara moja. Imani hiyo inaongoza busara ya kuomba na wenye mahitaji.

## Miongozo ya kuomba na Waombaji waliona hitaji

**(1) Angalau mwamini mmoja aliyekomaa atapaswa kumsaidia kila mwenye hitaji la maombi.**

Usimwache mwenye mahitaji ya maombi aombe peke yake na kuondoka madhabahuni bila ya msaada. Tunataka mwenye mahitaji ya maombi afikie ushindi kamili.

**(2) Tafuta ni kwa nini mwenye mahitaji anaomba.**

Usitake kudhania kwamba anaomba kwa ajili ya kuokoka. Hata baada ya mahubiri ya kiuinjilisti kumalizika, watu huja kwenye madhabahu kwa sababu nyingi. Siyo lazima kumsumbua mwenye mahitaji ya maombi akiwa katika maombi; lakini wakati mwingine, mwamini anayemsaidia anaweza akamwuliza, "Je, unataka Mungu akufanyie nini?" Kisha mwamini anaweza akaomba pamoja naye kwa hitaji lolote alilo nalo.

**(3) Mtie moyo mwenye mahitaji ya maombi afanye toba kamili.**

Uliza, "Je, uko tayari kutubu dhambi zako, na umruhusu Mungu akukomboe kutoka katika dhambi yako?" Mtie moyo amwambie Mungu kuhusu toba yake. Siyo lazima kwake kukiri dhambi zake kwa mchungaji au mtu mwingine yeyote, labda iwe kuna dhambi maalumu dhidi ya watu hao.

**(4) Mhakikishie mwenye mahitaji ya maombi kwamba Mungu atamsemehe.**

Mwambie amwombe Mungu kwa ajili ya msamaha na atii ahadi ya Mungu ya kusamehe. Kama itaonekana anapata shida kutokana na kuwa na mashaka, mwoyeshe ahadi ya kimaandiko (1 Yohana 1:9, Yohana 3:16, Warumi 5:8).

Kama itaonekana mwenye mahitaji ya maombi anashindwa kuomba kwa maneno yake mwenyewe, msaidizi anaweza akamsaidia maombi ambayo itampasa arudie ayafuatishe. Inaweza ikawa kama maombi yafuatayo:

"Bwana, ninajua mimi ni mwenye dhambi na ninayestahili adhabu ya milele. Ninajutia dhambi zangu na niko tayari kuachana nazo. Ninaomba unisamehe, siyo kwa sababu ninastahili, bali kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yangu. Asante kwa wokovu wako. Kuanzia sasa, nitaishi kwa ajili yako tu."

Kwa kawaida, kama mwenye mahitaji ana ugumu wa kuomba na kupata ushindi kamili, itakuwa kuna dhambi ambayo hajawa tayari kuachana nayo. Hawezi kuwa na imani kwa ajili ya msamaha hadi pale atakapokuwa ametubu kwa ukweli.

**(5) Mtake mtu aliyeokoka akupe ushuhuda.**

Kama mwenye mahitaji ya kuomba ataonekana anapata ushindi, mtu atapaswa kumwuliza, "Je, Mungu alikufanyia nini?" Mtie moyo atoe kauli yenye msimamo. Anaweza akatoa ushuhuda kwenye mkusanyiko wa waumini, lakini atapaswa angalau kwa mtu ambaye alisaidiana naye katika kuomba.

**(6) Toa maelezo yaliyochapishwa kuhusiana na wokovu.**

Mtu aliyebadilika anapaswa apewe maelezo yaliyochapishwa kuhusiana na wokovu ili aondoke nayo. Yanapaswa yawe yanaelezea kuhusu wokovu. Yatamsaidia mtu huyu kuelewa ni nini kilichotokea na pia yatamsaidia katika kuelezea kwa watu wengine.

**(7) Andaa hatua ya kwanza ya kufanya huduma ya ufuasi.**

Hatua ya kwanza ya kufanya huduma ya ufuasi kwa kawaida itakuwa ni kukutana na mchungaji au mwamini aliyekomaa kiroho. Hakikisha mtu aliyebadilika anaelewa ni nini kilichotendeka kwake. Baada ya hapo, anaweza kujiunga na kikundi kidogo au kuwa anakutana na mwamini mwingine mara kwa mara.

Inatakiwa kuwe na mtu wa kutembelea familia yake, kuhakikisha wanajua kuhusu mabadiliko yao, na kuwakaribisha kuhudhuria kwenye kanisa. Inawezekana kukawepo na nafasi ya kushirikishana injili pamoja nao.

► Je, kuna mila na taratibu gani katika kanisa lako kwa ajili ya kuomba na mtu mwenye mahitaji ya maombi? Unahitaji ufanye nini ili kuongezea orodha iliyotajwa hapo juu?

## Kuhubiri kwenye Mkutano wa Nje

Kuhubiri kwenye mkutano wa nje ni kwa kusudi la kuwafikia watu ambao hawaji kanisani. Ni vigumu sana kwa sababu wasikilizaji wako pale kwa makusudi mengine na wanaweza wasiwe makini na kinachoendelea. Inawezekana kukawepo na makelele na mambo ya uvurugaji. Kunakuwa hakuna mazingira ya kuabudu yaliyoandaliwa na kusanyiko la kanisa kama ambavyo ingewezekana ikawa ndani ya kanisa.

Hitaji la wazi la kwa mhubiri wa mkutano wa nje ni kwamba anatakiwa awe na sauti yenye nguvu ya kutosha kwa ajili ya watu kumsikia, au anaweza kutumia vyombo vya kupaazia sauti.

Changamoto ya kwanza ya kuhubiri kwenye mkutana wa nje ni kupata utulivu na usikivu wa makini. Watu walioko kwenye eneo la mkutano huamua mara moja kama wanataka kusikiliza au la. Baadhi yao watasikiliza kwa dakika chache. Wengi wao watasikiliza sentensi mbili au tatu kabla hawajaamua kama wanayo au hawana nia ya kuendelea kusikiliza.

Mhubiri anapaswa atumie sentensi fupi, na kila sentensi iwe na maudhui ya kutosha. Ni lazima akumbuke kwamba kila sentensi ni lazima iwe sentensi ya kwanza ambayo baadhi ya wasikilizaji wataisikia. Kuwa na pointi ya kusemea kwenye kila sentensi kutasaidia kugusa usikivu wa makini wa wasikilizaji. Kama atafanikiwa kupata kundi la kumsikiliza, anaweza kutoa vielelezo na kufafanua pointi zake kwa ufasaha zaidi.

Ikiwezekana, mhubiri atapaswa kuwa na kikundi cha waamini pamoja naye. Kama watu wanaopita wakiona kuna watu wengine wanaosikiliza, na wao pia kuna uwezekano mkubwa wakasimama na kusikiliza. Kama kuna wana muziki wa maudhui ya Kikristo

ambao wanaweza kuwa wanatumbuiza nyimbo kabla ya kuhubiri, kwa kawaida husaidia katika kuwakusanya watu.

Mhubiri anapaswa awakaribishe watu wasogee kule mbele aliko yeye na kuwaombea kwa ajili ya wokovu.

Wasaidizi watapaswa kugawa vipeperushi vyenye taarifa zilizochapishwa kwa watu katika eneo hilo.

► Je, kuna utaratibu gani uliopo kwa ajili ya mahubiri ya mkutano wa nje katika maeneo ya majirani zako?

### Ukumbusho kwa Kongozi wa Darasa

*Sasa kila mwanafunzi aangalie mahubiri yake ya kiuinjilisti aliyokuja nayo. Ayafanyie tafakuri ni kwa jinsi gani yanatimiza miongozi 10 ya mahubiri ya kiuinjilisti. Atapaswa kupanga ni kwa jinsi gani yatakavyoweza kufanyiwa mapitio ili kusahihisha na kufanya yawe bora zaidi.*

*Inawezekana kusiwe na muda wa kutosha wa kujadili mahubiri ya kila mwanafunzi aliyoandaa, lakini baadhi yao miongoni wao watapaswa watoe mahubiri yao yajadiliwe ili kuonyesha mifano.*

*Katika kipindi kitakachofuata cha darasa hakutakuwepo na somo lingine. Wanafunzi watapaswa washughulike na kuwasilisha mahubiri ya kiuinjilisti waliyoyaandaa na kisha kuyajadili. Siyo lazima wafanye mahubiri yote hadi kukamilisha kabisa, lakini yafupishwe na yawekwe kwenye muhtasari ambao kila mahubiri yanaweza kuwasilishwa kwa takribani dakika 5-7. Kipindi kingine cha darasa kitakachofuata baada ya kipindi cha mazoezi kitakuwa kwenye somo la 12.*

### Kazi ya Kufanya

Tayarisha mahubiri ya kiuinjilisti ambayo yatazingatia mtiririko wa miongozo iliyotolewa katika somo hili. Hayo mahubiri siyo lazima yaandikwe yote kwa ukamilifu, lakini yatapaswa yawe na taarifa za msingi zilizoandikwa. Ziletwe kwenye kikao cha darasa kitakachofuata kwa ajili ya majadiliano.

# Somo la 12
# Milango iliyofunguka

## Utangulizi

► Je, kuna ulazima wowote wa kuomba kwa ajili ya wenye dhambi? Je, ni mahali gani kwenye Bibilia tunapoagizwa kwamba tuombe kwa ajili ya wenye dhambi?

Siyo rahisi kupata aya kwenye Biblia inayosema moja kwa moja kwamba tunapaswa tuombe kwa ajili ya mabadiliko ya wenye dhambi. Kitu tunachoweza kukipata ni aya nyingi zinazotueleza kwamba tunapaswa kuomba kwa ajili ya ufanisi wa usambazaji wa injili.[158]

Hatujui kwamba tunapaswa tuombe kwa ajili mabadiliko ya wenye dhambi pamoja na kuomba kwa ajili ya ufanisi wa usambazaji wa injili. Tunaambiwa tuombe kwa kila mtu, ikiwa ni pamoja na kuomba kwamba wenye dhambi wapate kubadilika.[159] Tunaambiwa tujaribu kuleta watu kwenye toba,[160] na litakuwa jambo sahihi kuomba msaada wa Mungu kwenye kazi hiyo.

## Uinjilishaji katika Kizazi cha Kwanza

Wakati kanisa linapokuwa kwenye hali nzuri, uinjilisti ulionekana kutokea kwa hiari na kwa njia ya kawaida. Katika kizazi cha kwanza cha kanisa kilichoelezwa katika kitabu cha Mtendo, inaonekana kwamba kila mtu alikuwa mwenye furaha wakati wa kueneza injili.

► Mwanafunzi anatakiwa asome Matendo 2:46-47 kwa ajili ya kikundi.

Inavyoonekana, ushirika wa kanisa ulikuwa wenye nguvu sana na wenye uhai kiasi kwamba kwa njia ya kawaida sana uliweza kuwavutia watu kujiunga nao. Hali hii inatuashiria kwamba kama kanisa halina mvuto kwa watu wapya, ushirika wake siyo wenye nguvu kama ambavyo ingetakiwa iwe.

► Mwanafunzi anatakiwa asome Matendo 5:42 kwa aili ya kikundi.

Mitume na watu wengine walipata fursa nyingi za injili kila mahali na kwa watu wote. Makanisa mengine yamekuwa hayafanyi uinjilisti, na hawana uhakika ni kwa jinsi gani waanze. Hawajui namna ya kutafuta fursa kwa ajili ya injili.

[158] 2 Wathesalonike 3:1, Waefeso 6:19, Wakolosai 4:4, Matendo 4:29
[159] 1 Timotheo 2:1
[160] 2 Timotheo 2:25

► Mwanafunzi anatakiwa asome Matendo 8:1-4 kwa aili ya kikundi.

Kwa sababu ya mateso, Wakristo wengi waliondoka Yeusalemu kwenda kuishi kwenye maeneo mengine. Walishirikisha injili kwenye maeneo yote waliyokwenda. Kwao, kushirikisha injili kulikuwa ni sehemu ya maisha yao ya Kikristo.

## Mabishano ya Makanisa

Unatakiwa uepukane na mashindano yanayoibuka kuhusiana na makanisa mengine mbele ya watu ambao hawajaokoka. Usijaribu kutoa shutuma kwa makanisa yao wakati unapokuwa unashirikisha injili. Watu ambao hawajaokoka hawana ufahamu wa kiroho wa kuja kwenye maamuzi sahihi kwenye mabishano ya kidini. Watu wengi wa kidunia wanasema kwamba migogoro iliyoko miongoni mwa makanisa ni sababu za wao kutoamini katika Ukristo.

Kama mtu ataweka msisitizo kwenye kuulizia kuhsu tofauti za kiimani, mpatie majibu kutoka kwenye maandiko, lakini jaribu kumrejesha kwenye kipaumbele cha injili. Unaweza kusema, "Maswali kama hayo ni muhimu, lakini jambo muhimu zaidi ni kuokoka na kuwa kwenye uhusiano na Mungu." Kama watakuelezea kuhusu Mkristo waliyemjua, labda mtu katika jamii au mchungaji, jaribu kutoelezea mambo ya lawama kuhusiana na imani ya mtu huyo.

Kama una kitu cha kuelezea ni kwa nini kanisa lako ni tofauti na kanisa lingine, unaweza ukasema, "Ni muhimu kwa mtu kutubu dhambi zake, akasamehewa, na akaishi kwenye maisha ya utiifu kwa Mungu. Makanisa yetu huwekea mkazo kipaumbele hicho, kwa hiyo tuko tofauti na makanisa mengine yaliyo na msisitizo wa mambo mengine."

## Maswali Magumu

Baadhi ya Wakristo wana hofu ya kufanya uinjilisti kwa sababu wanahofia kuulizwa maswali magumu. Ni vyema kuendelea kujifunza, lakini ukweli ni kamba wakristo wengi hawajui jinsi ya kujibu maswali yote magumu. Hauhitaji kujua majibu ya maswali yote.

Kama mtu atakuuliza swali ambalo unaliona ni gumu kuweza kujibu, unaweza ukasema kama ifauatavyo: "Sijui jibu sahihi kwa swali lako. Kuna mtu kwenye kanisa letu anaweza akasaidia kujibu swali hilo. Lakini mimi ninaiamini Biblia, na jambo muhimu zaidi ninaloliamini ni kumjua Mugu na kuokoka. Ninajua ni kwa jinsi gani unaweza kufanya ili uokoke."

Kama mtu atasema, "Mimi siiamini Biblia," au "Mimi siamini katika Mungu," kuna mielekeo miwili tofauti unayoweza kuitumia kuelekeza mazungumzo hayo. Unaweza ukamwuliza sababu iliyo katika mawazo yake na ukajaribu kumpa baadhi ya ushahidi ulio nao. Mwelekeo mwingine ni kusema, "Inaelekea ulikuwa na wazo katika hili na ukajaribu kuja kwenye uamuzi wenye maana. Lakini hata kama huiamini Biblia, kama mtu mwenye busara unatakiwa kujua ujumbe wa msingi wa Biblia. Je, ninaweza kukuonyesha ni kitu gani?" Kwa kufanya hivi, unaweza ukajikuta unashirikishana injili pamoja naye bila ya

kushindana. Mungu anaweza akautumia ujumbe huo katika kugusa maisha yake kwa wakati wa baadaye.

Wakati unapokuwa unapofanya uinjilist, unaweza kukutana na mtu ambaye nia yake anataka tu ashindane na wewe. Unapaswa uepuke kupoteza muda mwingi na mtu wa aina hii. Hata kama utasema mambo yote yaliyo sahihi, inawezekana asikubaliane na ukweli wako. Jaribu kumshirikisha misingi ya injili kisha ondoka hapo ukazungumze na mtu mwingine.

### Kuitetea Injili

► Soma Tito 1:9-11. Je, aya hii inatoa sababu gani kwamba sisi tunapaswa tuilinde injili?

Mojawapo ya uwezo ambao mchungaji anapaswa kuukuza ni uwezo wa kuulinda ukweli wa Ukristo dhidi ya falsafa za dunia. Hii haina maana ya kuzungumzia kuhusa ushindani wa imani za makanisa tofauti, bali ukinzani wa dunia dhidi ya injili.

Sababu ya kutufanya tuutetee ukweli siyo tu kwa sababu ya kutaka kumbadilisha mtu anayeshindana, bali kuwasaidia watu ambao wanavutiwa na yeye. Watu wengi bado hawajawa na uamuzi wa kitu gani cha kuamini. Wanahitaji kusikia utetezi wa ukweli wa Kikristo.

Wakristo wengi bado hawajajazwa kwa ukamilifu uwezo huu wa kufanya aina hii ya ushindani. Kila Mkristo anatakiwa ajifunze kwa kadri inavyowezekana, lakini kuna baadhi ambao wamejaliwa karama hii na wako tayari kwa ajili ya kazi hiyo.

Wakati wa ushindani, ni muhimu sana kuonyesha kusudi lako. Hauko hapo kwa kujaribu kushinda mashindano. Haupambani na mtu kama adui yako binafsi. Unapaswa uonyeshe kwamba ukweli ni muhimu kwako kwa sababu unawajali watu. Kama hataiamini injili, roho yake itapotea. Ndio maana uko hapo kwa kusudi la kutaka kubadilisha ufahamu wake. Unaweza ukasema jambo lolote kama, “Ninakutaka wewe umfahamu Mungu na uokoke, na nina wasiwasi kwamba unaamini kitu ambacho hakitaweza kukupeleka kwa Mungu.”

### Kukuza ujuzi wa Kutengeneza fursa

Tunazo kumbukumbu katika nyakati za Biblia ambapo mwinjilisti alitafuta nafasi maalumu kwa ajili ya kushirikisha injili.

► Mwanafunzi atapaswa asome Matendo 8:26-39 kwa ajili ya kikundi. Mwanafunzi mwingine anaweza akaulizwa kufanya muhtasari wa maelezo kwa ajili ya kikundi. Je, ni kwa jinsi gani Roho wa Mungu aliwajibika kwenye hili tukio? Ni kwa jinsi gani Filipo aliitambua fursa iliyojitokeza kwa ajili ya injili?

Mfano mwingine wa mwinjilisti kutambua nafasi inayojitokeza kwa ajili ya injili ni Yesu mwenyewe.

► Mwanafunzi atapaswa asome Yohana 4:7-14 kwa ajili ya kikundi. Mwanafunzi mwingine anaweza akaulizwa kufanya muhtasari wa maelezo kwa ajili ya kikundi.

Mazungumzo haya kati ya Yesu na mwanamke Msamaria yalihusisha pamoja na mada za migogoro ya kimila, utata wa kidini, na mfumo mzima wa maisha. Yesu hakuchukua muda mrefu katika mada hizo, lakini aliyaongoza mazungumzo yake kwenye mada ya mahitaji ya kiroho ya yule mwanamke.

Utakapokuwa umejifunza jinsi ya kuwasilisha injili, utatafuta nafasi za kushirikisha watu wengine. Mara chache, mtu anaweza akataka kuisikia injili, lakini nafasi kama hiyo haiko wazi hivyo.

Baadhi ya Wakristo huhisi kwamba ni vigumu kushirikisha injili kwa sababu wanadhania kwamba watu hawana haja ya kusikiliza. Wanafikiri kwamba ni vigumu kuanzisha mazungumzo yanayohusiana na dini.

Injili huhusika na mambo mengi waliyo nayo watu. Kwa hiyo, hakuna tatizo la kuanza kuzungumzia injili katikati ya mazungumzo yanayoendelea.

Katika somo hili, baadaye tutazungumzia kuhusu sababu wanazokuwa nazo watu hata kutamani injili.

## Aina mbali mbali za dhamira

Watu wana aina nyingi za sababu za kuupokea wokovu. Wakati mwingine kunakuwepo na dhamira mbaya, lakini kuna sababu nyingi za dhamira sahihi.

► Je, kulikuwa na sababu gani zilizokufanya wewe ukakubaliana na injili? Toa nafasi kwa wanafunzi waeleze sababu zao wenyewe zilizowafanya wakakubali kuokoka.

Hapa kuna aina nyingi dhamira ambazo zinawafanya watu wahitaji kuokoka.

- Kwenda mbinguni na siyo motoni (au hofu ya hukumu)
- Kuwa na utimilifu na kusudi katika maisha
- Kuwa na ulinzi, amani ya rohoni, na kuwa huru kutokana na hofu
- Kupata msamaha, uhuru wa kutokuwa na hatia (dhamira iliyo wazi)
- Kuwa msafi kiroho na katika mambo yote
- Kuwa na ushirika na Mungu (kumjua Mungu)
- Kuwa na ushirika na Wakristo wengine
- Kuwa na utoshelevu wa matamanio ya kiroho (furaha ya kweli)
- Kupokea ukombozi kutokana na dhambi
- Kuujua ukweli

Haya ni mafanikio ya moja kwa moja ya upatanisho na Mungu. Siyo mambo ya kidunia ambayo yanapingana na thamani za umilele. Mtu anakosa vitu hivi kama anakuwa ametengwa na Mungu.

► Angalia kwenye orodha hii na jaribu kutafakari ni vitu gani ambavyo ni muhimu kwako. Ni vitu gani vilikuvutia wewe kabla hujabadilishwa na kuokoka? Ni vitu gani ambavyo vilikuwa ni vya muhimu sana kwako baada ya kubadilishwa na kuokoka?

Mtu ambaye hajaokoka anaweza akaonesha kwenye mzungumzo yake kwamba anajisikia kuhitaji mojawapo ya manufaa haya ya kuokoka. Mwinjilisti anaweza akabadilisha njia yake aliyokuwa anaitumia kuwasilisha injili ili kushughulika na hitaji hili. Sema, "Sababu ambayo watu hawana ______ ni kwamba wametengwa na Mungu. Biblia inatuambia jinsi ya kurejea tena upya kwenye uhusiano na Mungu."

Ni muhimu kuhakikisha kwamba hatutoi ahadi za furaha ya dunia kwa mtu yeyote ambaye anataka kuwa Mkristo. Mtu ambaye anaamua kuwa Mkristo, kwa sababu hiyo inawezekana siyo wa kutubu dhambi yake kwa ukweli, na, kwahiyo, hataweza kupata haya mafanikio ya kuokoka. Sababu nyingine zinazotufanya tusitoe ahadi za furaha ya dunia ni kwamba Biblia haitoi ahadi ya hali zilizo nzuri kwa Wakristo; badala yake, inatabiri mateso.[161]

Sababu kubwa na ya muhimu inayomfanya mtu kutaka kuwa Mkristo ni kwamba anajitambua ni mwenye hatia na kwamba kuna hukumu inayokuja. Vitu vingine vilivyoko kwenye orodha hapo juu vinaweza kutumika kumsaidia mtu katika kujitambua kwamba ametengwa na Mungu.

### Kutambua Nafasi Zinazojitokeza kwenye Mazungumzo

► Je, ni upenyo gani umewahi kuutumia katika kupata nafasi ya kushirikisha injili?

► Je, imeshawahi kutokea ikaoneakana ni vigumu kwa yeyote kati yenu kupata nafasi ya kushirikisha injili? Je, Unafikiri ni kwa sababu gani?

Mara nyingine nafasi inaweza ikajitokeza kwa urahisi. Kwenye hali kama hiyo, unaweza tu kirahisi kuanza kuelezea kuhusu injili. Kama utataka uwaonyeshe aya za maandiko, unaweza ukawauliza, "Je, ninaweza nikatumia dakika chache kuwaonyesha kile ambaco Biblia inasema kuhusiana na jinsi ya kuwa Mkristo? Kama utataka kuonyesha daraja la mchoro, unaweza ukawauliza, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili kuwaonyesha mchoro ambao unaoelezea kile ambacho Biblia inasema kuwa ni njia ya kujua kwa uhakika kwamba umeokoka?"

Upenyo hujitokeza katika mazungumzo kwenye namna nyingi za mada. Kwa upenyo wowote unaotokana na mazungumzo ulioelezewa hapa unaweza kutumika kwa ajili ya kuwasilisha daraja la mchoro au kuwasilisha injili kutoka kwenye Maandiko kama vile Barabara ya Kirumi.

► Je, ni watu wengi kiasi gani mmeshasikia wakilalamika kuhusu hali ngumu ya maisha yao?

[161] 2 Timotheo 3:12

Mara nyingine watu hulalamika kuhusu hali ngumu katika maisha yao. Waulize, "Je, Kwa nini maisha yamekuwa magumu kiasi hicho?" Baada ya kukujibu, sema, "Je, ninaweza kuwaonyesha mchoro ambao unaelezea ni kwa nini maisha yamekuwa magumu kiasi hicho?" Anza kwa kusema kwamba Mungu alitukusudia sisi tuishi kwenye mahusiano pamoja naye na hajakusudia kwetu maisha yawe magumu kama yalivyo sasa. Dunia imeharibiwa na dhambi. Kisha endelea na uwasilishaji wa mchoro.

Kutaka kuwasilisha moja kwa moja kutoka kwenye Maandiko, kama Barabara ya Kirumi, Unaweza kusema, "Biblia inafafanua kwamba maisha ni magumu kwa sababu kila mtu ametenda dhambi. Dhambi imeleta laana juu ya dunia." Sasa, endelea kwenye Barabara ya kirumi.

Kama mtu ataonekena kuwa wa kidini zaidi, unaweza ukamuuliza imani anayoiona ni muhimu sana kwake ni ipi. Au unaweza kumwuliza, "Je, unaamini ni njia ipi ambayo mtu anaweza akajua kwamba ataingia mbinguni?" Baada ya kusikia jibu lake, mwulize, "Je, ninaweza kuchukua dakika mbili za kukuonyesha mchoro ambao unaelezea kile ambacho Biblia inasema kuhusiana na jinsi mtu atakavyoweza kuingia mbinguni?"

► Je, umeshawahi kusikia watu wakizungumzia kuhusu hali mbaya ya dunia au matatizo ya kitaifa? Ni kwa jinsi gani utaweza kutumia hali hizi kama upenyo wa nafasi ya kushirikisha injili?

Kama mtu anazungumzia kuhusu matatizo ya kitaifa, njaa ya dunia au umaskini, au majanga ya vita, mwulize, "Je, ninaweza kukuonyesha Maandiko ambayo yanafafanua ni kwa nini dunia imekuwa kama ilivyo sasa?"

Onesha kwamba hali ya dunia iko kama ilivyo kwa sasa kwa sababu wenye dhambi wametengwa na Mungu. Usitake kuonesha kwa ujumla, kwamba kuokoka kunamaliza matatizo yote, lakini onesha kwamba kuokoka kwa mtu binafsi ni mwanzo wa suluhisho la Mungu. Siku moja kutakuwepo na mbingu mpya na nchi mpya na matatizo hayo hayataonekana tena kwa watu ambao kwa sasa wamepatanishwa na Mungu.

## Kutumia Maswali ya Kufungua

Maswali yanaweza kutumika katika kuanzisha mazungumzo, na kisha mazungumzo hayo yatafungua nafasi kwa ajili ya injili.

Swali la kwanza kabisa ni kuuliza tu kirahisi kwamba "Wewe ni Mkristo?" Mara nyingi watu wengi hawakwaziki na swali hili. Kama mtu atasema, "Hapana," unaweza ukauliza, "Je, ninaweza nikakueleza ni kwa jinsi gani mtu anakuwa Mkristo?"

Mtu huyo akisema, "Ndiyo, mimi ni Mkristo," unaweza kusema, "Hiyo ni nzuri sana. Ulipataje kuwa Mkristo?" Kama jibu ni potofu au inaonekana mtu amechanganyikiwa, unaweza ukachagua kufafanua Biblia inasema nini kuhusiana na mtu kuwa Mkristo.

Maswali yaliyoko kwenye sehemuya hapo juu yanaweza yakatumika kama maswali mengine ya kufungua wakati wa mazungumzo. Hapa chini kuna maswali ya nyongeza.

“Unafikiri kusudi la maisha ni nini?” Acha mtu atoe maoni yake. Kubaliana na kila kitu kinachooneka ni chema katika kauli zake. Kisha utasema, “Sehemu muhimu sana katika kusudi letu ni kumjua Mungu. Alituumba sisi ili tuishi kwenye uhusiano na yeye. Je, ninaweza kukuonyesha kile ambacho Biblia inasema kuhusu jinsi ya kuwa kwenye uhusiano na Mungu?”

“Je, unafikiri msingi mkuu wa furaha ni nini?” Lolote litakalojibiwa, unaweza kusema, “Watu wengi walio na furaha hawaonekani kuwa na furaha kwa muda mrefu. Biblia inatuambia kwamba furaha inatoka kwa Mungu.[162] Je, ninaweza kuwaonyesha mchoro ambao unaelezea ni kwa jinsi gani mtu anaweza akawa kwenye uhusiano na Mungu?”

“Je, unaamini kwamba kuna maisha mengine baada ya kufa? Unadhani yanafananaje?” Kisha, “Biblia inasema kwamba kila mtu aidha ataingia mbinguni au ataingia motoni. Je, ninaweza kukuonyesha kile ambacho Biblia inasema kuhusu jinsi ya kuingia mbinguni?”

“Je, unadhani msingi mkuu wa ujumbe wa Biblia ni nini?” Hapa inakupa wewe nafasi ya kuonyesha mchoro ulioko katika somo la 9.

► Je, kuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye tayari alishawahi kutumia njia inayofanana na mojawapo katika hizi? Ilifanyaje kazi?

Siyo kila mwanafunzi atajisikia vyema na mbinu zote ambazo zimeelezwa katika somo hili. Inawezekana kabisa kwamba mbinu mojawapo isionekane inafaa katika kila mila.

Kusudi la somo ni kumsaidia mwanafunzi kutafuta jinsi ya kukuza upeo wake wa njia zake mwenyewe za kuwasilisha.

### Ukumbusho kwa Kongozi wa Darasa

*Somo linalofuata limehusisha maelekezo kwa ajili ya kusambaza vipeperushi. Wanafunzi watahitaji kujua ni mahali gani wanatakiwa wapate hivyo vipeperushi kwa ajili ya kuvisambaza. Kama itawezekana, njoo na vipeperushi vya kusambaza kwenye kipindi kingine cha darasa kitakachofuata.*

### Kazi ya Kufanya

Utakapokuwa unaendelea kuwasilisha injili katika wiki hii, jaribu baadhi ya haya maswali ya kufungua mazungumzo au andaa yako mwenyewe. Fanya kuangalia kwa makini ni kwa jinsi gani yanafanya kazi na andika aya moja kuelezea haya. Uwe tayari kueleza uzoefu wako ulioupata kwenye kipindi kingine cha darasa kitakachofuata.

[162] Zaburi 16:11

# Somo la 13
# Uboreshaji Mbinu za Uinjilisti

## Utangulizi


► Je, unafikiria kuwa kazi ya uijilisti leo ni tofauti na nyakati za Agano jipya?

► Je, unafikiri kuwa uinjilisti katika nchi yako ni tofauti na wakati ambapo wamisionari wa kwanza walipokuja?

## Uinjilisti katika Historia: Mifano ya John Wycliffe na John Wesley

John Wycliffe alikuwa mchungaji nchini Uingereza. Aliishi kuanzia mwaka 1324-1384. Wakati ule, Biblia ilikuwa haipatikani kwenye lugha za watu zinazoeleweka. Watu walikuwa wanategemea kile kilichokuwa kikifundishwa kutoka katika Kanisa Katoliki la Kirumi. Watu wengi walikuwa hawaijui injili. Hata makasisi wengi wa Kikatoliki walikuwa hawaijui Biblia vizuri. Makasisi walisafiri nchi nzima wakifanya mila za kidini na kutaka wapewe fedha. Makanisa mengi yalikuwa yanaongozwa na makasisi ambao walikuwa hawahubiri injili. Wycliffe na wasaidizi wake waliitafsiri Biblia kwenda katika lugha ya Kiingereza. Uchapishaji kwa mashine haukuepo kwa wakati huo, kwa hiyo walinukuu maandiko kwa kutumia mikono. Walisafiri wakiwa watu wawili wawili na kufundisha Biblia kwa makundi mbalimbali kila mahali. Watu waliwaita "makasisi maskini" kwa sababu walikuwa hawaombi fedha.

Mbinu za uinjilisti ni lazima zitumiwe kutokana na mazingira ya jamii. Wycliffe na wasaidizi wake walikamilisha sehemu yao ya msingi ya uinjilisti; waliupeleka ujumbe wa Bibilia moja kwa moja kwa watu.



John Wesley aliishi katika nchi ya Uingereza kuanzia mwaka 1703-1791.[163] Kuanzia wakati ule, Kanisa la Anglikana lilikuwa limefanyika kuwa ni kanisa la matajiri. Walikuwa watu wa matambiko na hawakufundisha injili iliyo wazi. Watu wengi katika taifa waliokuwa maskini sana hawakualikwa waingie makanisani na walikuwa hawaijui injili. Wesley alikuwa ni kasisi wa Kianglikana, lakini alikuwa anataka aipeleke injili kwa watu. Siku moja asubuhi, alikwenda kwenye shamba ambalo wachimba mkaa wengi walikuwa wakipita njiani kuelekea kazini. Alianza kuhubiri, na wachimba mkaa wengi wakasimama ili kusikiliza.

[163] Image: "John Wesley preaching on his fathers grave", by Currier & Ives, retrieved from the Library of Congress Prints and Photographs Division, https://www.loc.gov/pictures/item/2002707689/, "no known restrictions."

Baada ya hapo, alikuwa anahubiri mikutano ya nje kila siku kwa kipindi chote cha maisha yake. Maelfu ya watu walibadilika kupitia huduma yake.

► Je, ni mmisionari gani anayekumbukwa kwa kuwa mtu wa kwanza kuleta injili kwenye eneo lako?

## Hitaji la kurekebisha Mbinu

Katika mwaka wa 2003, mtu mmoja alikuwa anasafiri nchini Uingereza pamoja na familia yake na akasimama katika bustani kwa ajili ya mapumziko. Alimwona mwanamke mmoja akiwa amesimama kwenye kilima kimoja cha ile bustani. Alikuwa na Biblia na alikuwa akiongea. Alimsogelea karibu na akawa anamsikia akizungumzia kitu kama cha kidini. Alitambua kwamba alikuwa na rafiki aliyekuwa amesimama pembeni mwake, kwa hiyo akamwuliza yule rafiki yake ni nini kilichokuwa kinaendelea mahali pale. Yule rafiki akamjibu, "Sisi ni sehemu ya kikundi ambacho tunaendeleza mila ya kuhubiri mikutano ya nje kama alivyokuwa anafanya Wesley. Mara kwa mara tunaenda kwenye maeneo ya wazi ya kijamii kwa ajili ya kuhubiri." Hata hivyo, yule mtu aliangalia kwa makini na kuona kwamba yule mama alikuwa amekaa kwenye eneo ambalo watu wachache walikuwa wakipita, siyo wote waliokuwa wanamsikia, na mbinu yake aliyokuwa akitumia ilikuwa haina ufanisi wa kufanya watu waliokuwa kwenye maeneo hayo ya nje waweze kumsikiliza. Alikuwa anajaribu kuendeleza mila, lakini alikuwa amepoteza kila kitu ambacho hapo awali kilifanya mbinu za kuhubiri mikutano ya nje kuwa na ufanisi.

Ni lazima kurekebisha mbinu ziendane na mazingira mbalimbali. Mara nyingine watu hudhania kwamba kuna njia moja tu ya kufanya uinjilisti, na wanaendelea na mbinu ambayo haina ufanisi tena. Mara nyingine, watu hufikiri kwamba mbinu iliyokuwa na ufanisi katika eneo moja itakuwa pia na ufanisi kila mahali katika maeneo mengine, lakini hiyo siyo kweli.

Katika maeneo mengi kanisa lilikuwa likifanya uinjilisti wa kwenda nyumba kwa nyumba, wakigonga hodi kwenye milango ya watu ambao walikuwa bado hawajawahi kukutana nao. Mbinu hii ilisababisha kuwepo na watu wengi sana waliobadilika na kuokoka, lakini haikuwa na ufanisi kwenye kila eneo.

Baadhi ya makanisa yalinunua mabasi na kuyatumia kuleta watu kwenye nyumba za ibada. Kila Jumapili asubuhi wataendesha basi katika maeneo yote ya jirani wakikusanya watu. Watu wengi walibadilika na kuokoka kupitia "huduma ya mabasi," lakini mbinu hii hakufanya kazi kwa kila eneo.

Makanisa mengi yamekuwa yakifanya uinjilisti kwa kuhubiri injili kwa kundi la watu waliokuwa wanakuja kwenye nyumba za ibada siku za Jumapili. Wanawaalika kuja mbele madhdbahuni kwa ajili ya kuokoka. Maelfu ya watu wamebadilika na kuokoa kupitia mbinu hii, lakini watu wengi wasiookoka hawaji kwenye nyumba za ibada. Watu wengi hawataweza kuisikia injli hadi hapo mtu ashirikishane pamoja nao kibinafsi kwenye mazungumzo.

Mtume Paulo alikuwa ni mfano wa kuigwa wa kurekebisha mbinu za uinjilisti. Alikuwa anaweza kuzungumza ndani ya masinagogi ya Kiyahudi kwa sababu alikuwa ni rabi wa Kiyahudi aliyekuwa amefuzu, na aliweza kuwaelezea kwamba Yesu ni Masihi. Aliweza pia kuongea kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu waliokuwa wakipeana mawazo ya kifalsafa. Mara nyingine aliongea kwenye maeneo ya masoko. Mara nyingi alikuwa anaongea kwenye makundi yakiwa majumbani kwao.

## Baadhi ya Mbinu za Kisasa

Watu wamekuwa wakitumia njia nyingi tofauti katika kuanzisha mazungumzo kuhusu injili. Baadhi ya makanisa wamekuwa wakitumia maswali ya kiuchunguzi. Wanaenda kwenye maeneo yote katika jamii na kuuliza mawali kama haya: "Je, unafikiri kanisa lifanye nini kwenye jamii? Ni imani gani muhimu sana ya Kikristo? Unawezaje kuelezea kuhusu Mkristo ni nani? Ni kwa jinsi gani mtu anakuwa Mkristo? Baada ya kusikiliza kwa ustahimilivu mkubwa maoni ya watu, Mkristo anaweza akauliza, "Je, ninaweza kukuonyesha kile ambacho tunaamini Biblia inasema kuhusu Mkristo ni nani?"

Wakati mwingine wainjilisti wakiwa kwenye maeneo ya wazi ya kijamii wanawafanya watu kuvutiwa pamoja na kuwa na umakini kwa kuweka bango lililochorwa picha au mchoro vikielezea kuhusu injili. Wengine hutengeneza michoro kwa kutumia chaki. Baadhi ya wainjilisti huweka picha nzuri za rangi kwenye mbao za matangazo huku wakiwa wanatoa maelezo yao.[164]

Baadhi ya makanisa kutoa semina juu ya somo la kivitendo linalohitajika na watu wa eneo husika katika jamii. Somo linaweza kuwa kuhusu ndoa, jinsi ya kuwakuza watoto, kanuni za biashara, afya, au mafunzo yanahusiana na aina fulani ya kazi. Kanisa linafanya jambo jema linapokuwa linatoa huduma kwenye mahitaji ya kijamii ya eneo husika. Kanisa lina wajibu wa kuonyesha jinsi kweli za Biblia zinavyofanya kazi kwenye maisha ya kila siku. Semina inaweza isilenge kwenye uwasilishaji wa injili moja kwa moja, lakini inafundisha ukweli wa Biblia na kukuza mahusiano kati ya kanisa na majirani zake.

Baadhi ya makanisa yameanzisha vituo vya maombi vya muda kwenye maeneo ya wazi ya kijamii ambayo watu wanapita. Wanaweka hapo alama ya ishara inayosema, "Kituo cha Maombi" na hupanga kujitolea kuomba pamoja na watu wanaopita njiani. Wanauliza, "Je, unalo hitaji ambalo ungependa mimi niombe kwa ajili yake?" Wanaonyesha kuhusika na mahitaji ya watu na hawaanzishi mabishano. Mara nyingi, wanakuwa na nafasi ya kushirikisha injili. [165]

Hitaji la msingi na la muhimu sana la mbinu ya uinjilishaji ni kwamba injili inawasilishwa kwa uwazi kwa watu ambao wanahitaji kuisikia. Kwa kuwa Mungu hulipa nguvu Neno lake na Roho Mtakatifu huleta hukumu na mguso ndani ya wale wanaolisikia, mbinu ya uinjilisti

[164] Kwa ajili ya mifano ya mbinu hii, ona: The Open Air Campaigners websites: www.oacgb.org.uk and www.oacusa.org.
[165] Kwa ajili ya picha na taarifa, ona mitandao ifuatayo: www.prayerstations.org and www.prayerstand.com

ina uwezekano mkubwa wa kuleta ufanisi kama itawasilisha injili kwa uwazi na kwa njia ya moja kwa moja.

Changamoto ya kanisa katika maeneo yote na kila wakati ni jinsi ya kutafuta njia ya kuleta usikivu mkubwa wa watu na kufikisha injili kwenye jamii yote.

► Je, kuna njia gani ambazo kanisa katika mji wako au eneo lako linatumia katika kupata usikivu wa watu? Je, mbinu hizo zinafikisha ujumbe wa injili?

### Kufanya Uinjilisti kwa Marafiki

Aina ya uinjilisti ulio na ufanisi mkubwa sana ni ule ambao mtu anamweleza moja kwa moja mtu mwingine ambaye anamjua na anamwamini.

Mkristo anapaswa awe na ufanisi mkubwa wakati anaposhuhudia kwa marafiki zake, watu anaowafahamu na jamaa zake kwa sababu wanakuwa wameshaona mfano wa maisha yake. Kama maisha yake ni mazuri, kuna uwezekano mkubwa wao kuamini ushuhuda wake. Ni muhimu sana kwa Mkristo kudhihirisha imani yake ili siku zote watu wajue kwamba yeye ni Mkristo. Hapaswi kujisikia kwamba ni fedheha au anatahayarishwa kwa ajili ya watu kumwona akisoma Biblia au akiomba. Watu wanaomjua hawatamshangaa watakapokuwa wanamwona akifanya hayo kwa sababu wanatambua kwamba yeye ni Mkristo.

Mkristo anaweza akaheshimika kwa mfano wake shuleni au sehemu yake ya kazi hata na watu ambao hawaupendi ukristo. Hata wale watu wanaomsababishia mateso watamheshimu kama atakuwa ni mtu mwenye msimamo katika matendo yake na tabia zake. Baadhi ya watu watakuja kwake kwa ajili ya maombi na kupata ushauri.

### Makabiliano binafsi ya Mtu kwa Mtu

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba ni lazima wawe wanamjua mtu kwa kitambo fulani kabla ya kumshuhudia. Wanajaribu kuwa marafiki kwanza kabla ya kumshuhudia habari za Mungu. Ni ukweli kwamba mtu ana uwezekano mkubwa wa kumsikiliza rafiki yake. Hata hivyo, inawezekana kuonesha ukakumjali mtu kwa dhati usiyemfahamu na kuonesha hamasa kwa haraka sana. Kama hatutaweza kujifunza jinsi ya kushirikisha injili kwa watu tunaokutana nao, tutakosa upenyo wa nafasi nyingi zitakazotufanya tuwe na ufanisi. Somo lililotangulia kuhusu “Kufungua Milango” linatupa mbinu za kuanzisha mazungumzo kwa ajili ya injili.

Mtu mmoja alisema, “Wakati wowote niwapo mwenyewe pamoja na mtu mwingine kwa dakika chache, ninautumia muda huo kama ni kikao kilichoandaliwa na Mungu. Alimaanisha kuwa anaamini kwamba Mungu humpa watu wa kukutana nao kwa kuwatumia kwa ajili ya injili.

### Injili kwa Maandiko

Unaweza ukafanya jambo katika kupeleka injili ambalo Mtume Paulo hakuweza kulifanya.

Tunayo mbinu ya kupeleka injili ambayo ilikuwa haipatikani katika kanisa kwa karne nyingi: taarifa zinaweza kuchapishwa na mashine kwenye karatasi.

► Je, unafikiri kulikuwa na tofauti gani kihuduma kabla ya kuwepo kwa uchapishaji?

Jaribu kufikiria huduma katika nyakati ambazo kulikuwa hakuna uchapishaji. Kila nakala ya kitabu ilihitaji siku nyingi za kufanyiwa kazi na mwanazuoni kwa sababu kilikuwa ni lazima kiandikwe kwa mkono. Unaweza ukafikiria kwamba vitabu kwa wakati huu ni ghali, lakini fikiria kulipia kitabu kwa bei ile ile ambayo ungepaswa kumkodisha mtaalamu mwenye ujuzi kwa kazi ya siku kumi.

Takribani hakuna mtu yeyote aliyekuwa na nakala yake mwenyewe ya Maandiko. Hata mchungaji ingewezekana asiwe na Biblia yote nzima. Fikiria kama hungekuwa huna uwezekano wa kusoma Biblia ukiwa nyumbani.

Mafunzo kwa wachungaji mara nyingi yalifanyika kwa kuzungumza, na walipaswa kujaribu kukumbuka kile walichokisikia. Kulikuwa hakuna jinsi yeyote ya kupeleka makabrasha ya mafunzo sehemu nyingine. Bila uchapishaji, hakuna kitu ambacho kingeweza kikaandikwa na kusambazwa kwa wingi.

► Je, kuna njia gani ambazo uchapishaji husaidia kuenea kwa injili?

Vipeperushi ni vipande vidogo vya karatasi vilivyochapishwa makala, kwa kawaida zikiwasilisha injili. Wakristo wanaweza wakavigawa kwa watu wanaokutana nao. Vinaweza pia vikatolewa kwa kiwango kikubwa kwenye maeneo ya wazi ya kijamii. Vinaweza vikaachwa katika maeneo ambayo watu watavisoma.

Kama mtu hajawahi kufanya sana uinjilisti kwa watu wageni, kugawa vipeperushi ndio njia nzuri ya kuanzia.

Kipeperushi kinahitajika kiwe cha kupendeza na chenye kichwa cha habari chenye mvuto. Wakati wa ugawaji wa vipeperushi kwa watu barabarani au maeneo mengine ya wazi ya kijamii, kuwa mtu wa kucheka na kusalimia watu. Unaweza ukasema, “Haloo, umeshapata mojawapo ya vipeperushi hivi?” Hiyo itawafanya watu kuwa na shauku ya kutaka kuona ni nini kilichopo.

Inawezekana ikaonekana kwamba watu wengi hawana shauku na vipeperushi ambavyo umewagawia. Watu wengi wanaweza wakavitupa bila hata ya kuvisoma. Hata hivyo, pia, kuna matokeo mazuri. Watu wengi wamebadilika na kuokoka kwa sababu ya ujumbe wa vipeperushi. Kwa kawaida hutajua matokeo yaliyotokana na vipeperushi ulivyogawa.

### Kutana na mahitaji kwa vitendo

Mara nyingine watu wana wasiwasi na hitaji halisi la maisha. Wanaweza wakawa hawana chakula cha kutosha, au maeneo ya kujisitiri kwa malazi, au matibabu. Wanakuwa na hisia kwamba mahitaji hayo ni muhimu na ya haraka kuliko hitaji la kiroho. Kanisa linaweza kushiriki kwa vitendo kwenye mahitaji haya kama njia ya kushirikisha injili.

Tatizo la msingi hapa ni kwamba mtazamo wao unaweza ukaelekezwa kwenye mahitaji ya kidunia tu kuliko mahitaji ya kiroho, kama ulivyo mtazamo wa watu ambao hawajaokoka.

> "Wamisionari wa India, Uganda, na maeneo mengine wamekuwa wakilalamikiwa kwa kununua watu kuokoka kwa kuwapa fedha, misaada ya njaa, fursa za elimu, na huduma za matibabu, au kwa kuwapa mahitaji mengine yenye kipaumbele katika kuwahudumia."
> - J. Herbert Kane, "The Work of Evangelism"

Kanisa linapaswa liwajibike kwa vitendo kwenye mahitaji halisi lakini ni lazima lidumishe baadhi ya taratibu ambazo zinaweka mkazo kwenye kipaumbele cha kiroho.

1. Wanapaswa watoe ufafanuzi kwamba wanashirikisha upendo wa Mungu wanaposhughulikia mahitaji ya watu.

2. Wanapaswa wafanye kazi kwa pamoja kama familia ya imani, kuliko kuwa ni shirika linalojitofautisha na kanisa.

3. Wanapaswa wawaalike watu washiriki kwenye ushirika wa kanisa mahali ambapo kila mtu anamjali mwenzake.

4. Wanapaswa kushirikisha injili, wakifundisha kwamba maisha ya milele na baraka zinatoka kwa Mungu aliye mjuzi wa mambo yote.

Huduma nyingi hutoa programu ambazo zinaendana na mahitaji ya vitu. Wanatoa huduma kwa mahitaji ya jamii kwa kiwango kile ambacho uwezo wa raslimali zao unaruhusu. Lengo lao ni kutengeneza upenyo wa nafasi wa kushirikisha injili. Wanafikiri kwamba kusaidia watu kwa njia za vitendo kutawafanya wawe marafiki wao na wataweka mkazo au ustahimilivu kwa ajili ya injili. Kanuni inayotumika hapa ni Programu, kisha Uhusiano, halafu Injili.

Kuna njia nyingi ambazo programu za msaada zinaweza kwenda vibaya. Inawezekana kwamba hakutakuwa na uhusiano. Watu watatarajia tu kupata vitu kutoka kwa kanisa. Mara nyingine injili huonekana haina uhusiano na vitu vinavyotolewa, na watu wanaweza kuwa wapokeaji wa msaada tu bila ya kuwa na shauku katika suala la injili. Hata watu wanaofanya kazi kwenye hiyo programu wanakuwa katika kutoa msaada tu na hawashirikishi injili.

Kanuni ni lazima igeuzwe. Kanisa ni lazima liweke msisitizo wake kwamba injli ndiyo kipaumbele chake wakati wa kukutana na kila mtu kwa mara ya kwanza.

Wakati kanisa linapowasilisha injili kwa ulimwengu, ni lazima wawe waaminifu kuingiza maelezo ya maisha mapya ndani ya kanisa. Kuokoka siyo tu jambo la binafsi, na uamuzi wa mtu binafsi ambao unamwacha mtu peke yake katika hali ya maisha mapya ya kushangaza. Wenye dhambi kwa kawaida hawatakubaliana na injili labda wawe wamevutiwa na jamii ya watu wa imani ambayo inawasilisha injili.

Katika huduma ya Yesu na ya mitume, tunaona kwamba injili ni "Habari Njema" za ufalme wa Mungu. Ni ujumbe ambao mwenye dhambi anaweza akasemehewa na akawa kwenye

uhusiano na Mungu. Anakombolewa kutoka kwenye nguvu ya dhambi na kufanywa kiumbe kipya. Anaingia kwenye familia ya watu wa imani ambapo kaka na dada zake wa kiroho watamtia moyo na kumsaidia katika mahitaji yake.

Kanisa linapaswa lione msingi wake wa kwanza wa umisheni wa kueneza injili. Kanisa linapaswa lifanyie kazi jambo hilo wakati wote. Kila mtu anapaswa ajue kwamba kanisa ni kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu ziokolewe. Linawavutia watu ambao wana shauku ya injili. Watu hawa huja kwenye uhusiano na kanisa, kwa hiyo, huduma ya injili hutengeneza uhusiano.

Kisha, kanisa husaidia watu walio katika uhusiano na kanisa. Inawezekana siyo watu wote katika watu hao ambao watakuwa tayari wameshaokoka, lakini wako kwenye uhusiano na wanavutiwa na huduma ya injili ya kanisa.

Kwa hiyo kanuni iliyogeuzwa itakuwa kwanza ni Injili, kisha Uhusiano, halafu Msaada (na siyo programu). Kanisa halipaswi liwe kama ni shirika linalotoa programu zake za misaada. Badala yake, kanisa ni kikundi cha watu ambacho kinasaidia watu walio kwenye uhusiano pamoja nao. Kama wataanzisha programu mbalimbali, watu watakuja kwa ajili ya hizo programu na siyo kwa ajili ya uhusiano.

### Kazi za Kufanya

(1) Angalia kwa makini mbinu za uinjilisti zinazotumiwa na makanisa katika eneo lako. Je, hizo mbinu zilifanikiwa kuwavuta watu walio nje ya kanisa? Je, zinaeneza injili kwa uwazi? Andika kurasa 2-3 juu ya mambo uliyoyaona katika uchunguzi wako.

(2) Sambaza angalao vipeperushi visivyopungua mia moja. Andika sentensi chache kuhusiana na uzoefu wako ulioupata.

# Somo la 14
# Huduma kwa Watoto

## Utangulizi

► Soma Mathayo 18:2-6, 10-14. Je, kuna maonyo gani tunayoyaona katika aya hizi? Je, ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea umuhimu anaouna Mungu kwa watoto?

Mara nyingine watu husema kwamba watoto ni muhimu kwa sababu ni kizazi cha kesho, ni kanisa la baadaye, na viongozi wa baadaye. Hayo yote ni kweli; lakini mwanzo wa yote, watoto ni muhimu kwa sababu wao ni watu. Mara nyingine wazazi huonekana kusahau kwamba watoto ni watu wenye roho za milele na umaarufu na wana nguvu ambazo hazijaonekana bado.

> Mtu mmoja msafiri alisimama kwenye kijiji kimoja kidogo. Alimwona babu mmoja akiwa amekaa kando ya barabara na akasema, "Sijawahi kamwe kusikia lolote kuhusu kijiji hiki kabla ya hapo. Je, watu maarufu hawakuwahi kuzaliwa hapa? Yule babu akajibu, "Hapana. Ni watoto tu."

## Agizo la Mungu kwa ajili ya Huduma ya Watoto

Mungu aliwapa watu wa kale wa Israeli Agano. Aliahidi kuwabariki na kuwaweka kwenye uangalizi wake. Aliwapa mambo ya kufanya waliyotakiwa kuyatii.

Mungu alitaka agano lake liwe ni kwa ajili ya vizazi vyote. Aliwaambia, "Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii."[166]

Kuwakuza watoto katika kufuata mapenzi ya Mungu lilikuwa ni jambo muhimu kwa ajili ya agano, kwa sababu wingi wa baraka za Mungu zilikuwa na vigezo vya kufuata na ilitegemea kama watu wake wataendelea kumtii. Kama kizazi kilichofuata kingechagua kutokuwa waaminifu na watiifu kwa Mungu, basi wangepoteza manufaa yote ya uhusiano na yeye. Hii inamaanisha kwamba umakini mkubwa katika kufundisha watoto ulikuwa ni muhimu sana

► Je, unafikiri Waisraeli wangefanya nini katika kuhakikisha kwamba watoto wao wangekuwa ni watu wa kuamua kumfuata Mungu?

Mungu aliwapa maelekezo ya jinsi ya kuwafundisha watoto wao.

> Nayo wafunzeni vijana vyenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.[167]

[166] Kumbukumbu la Torati 6:6-7

Ni kitu gani Mungu alikuwa analenga hapa? Ilikuwa wawafundishe kwa bidii, kwa uaminifu, na kwa uendelevu, na siyo tu kwa mara chache. Walipaswa wawe na vitu vya kuwakumbusha kuhusu sheria za Mungu ambavyo vingewekwa kwenye maeneo yaliyo wazi. Walikuwa wayaone Maandiko kila mahali. Kamwe walikuwa hawatakiwi kusahau au kudharau maagizo ya Mungu

Mafundisho ya mara kwa mara yalimaanisha kwamba hawakutakiwa kuwa na mapambo, au sherehe au tabia ambazo zingekuwa kinyume na sheria ya Mungu.

Kwa hiyo, aya hizi msisitizo kwa wazazi kwamba wanawajibika kuwafundisha watoto wao maadili ya Mungu mara kwa mara na kwa uthabiti na kuwalinda kutokana na mafundisho na mifano ambayo vitawafanya waende kinyume chake.

► Agizo hili lilitolewa kwa wazazi. Je, ni mambo gani tuyafanye kwa ajili ya kutumika kwenye huduma ya kanisa?

Kwanza, tunajua kwamba kuwafundisha watoto ni wajibu wa kwanza wa wazazi. Kanisa linapaswa liwafundishe wazazi jinsi ya kuwafundisha watoto wao. Kamwe hatupaswi kuwa na dhana kwamba watoto wanatakiwa wapate tu maelekezo ya kiroho kutoka kwenye kanisa kwa sababu wazazi hawawezi kufanya hivyo.

Pili, kanisa linapaswa kuhudumia watoto kwa muktadha wa familia zao kwa kadri inavyowezekana. Wasaidie watoto kwa kuwasaidia wazazi wao. Wakati wa kufanya uinjilisti kanisa lijaribu kuwa kivutio cha kuzileta familia kwenye kanisa.

Baadhi ya watoto kutoka kwenye nyumba za familia zenye watu ambao hawajaokoka huja kanisani na kuokoka. Jambo kama hilo linapotokea, kanisa lijaribu kutoa huduma kwa ajili ya hiyo familia. Kama wazazi hawataitikia hilo, kanisa ni lazima liwe ni familia ya kiroho ya watoto hao. Washirika wa kanisa watapaswa wawe kama ndugu wakubwa kwa watoto hao ambao wataonyesha kuwajali na kuwatunza kiroho.

## Kufanya Tathmini ya Huduma ya Kanisa kwa Watoto

► Je, ni kwa jinsi gani unaweza kufanya tathmini ya mafanikio ya huduma ya watoto katika kanisa?

Huduma yako ya watoto siyo ya mafanikio hata kama…

- Waalimu wako wa watoto wana uwezo mkubwa.
- Idadi ya watoto na waalimu inaongezeka.
- Watoto wanajifunza habari muhimu za Biblia.
- Waalimu wanatumia vifaa vya thamani ya juu kufundishia.
- Watoto wanaifurahia huduma.

---

[167] Kumbukumbu la Torati 11:19-20

Tabia hizo zitakuwepo endapo huduma kwa watoto ni ya mafanikio. Kama huduma itakosa tabia hizi, kutakuwepo na tatizo. Hata hivyo, inawezekana kwa huduma kuwa na baadhi ya tabia, au kuwa nazo zote, lakini bado ni wa kushindwa.

Huduma yako ya watoto itakuwa ya mafanikio kama…

- Watoto watakuwa wamebadilika na kuokoka pamoja na kuwa na uhakika wa wokovu.
- Watoto hatua kwa hatua wanakua kiroho.
- Watoto wanavyozidi kuwa wakubwa, wanafuata maadili au kanuni za Mkristo.

Huduma yako haijafanikiwa ikiwa na mtoto ambaye…

- Siyo Mkristo.
- Amechagua kufuata mifano ya watu wengine wa kidunia.
- Anafuata sherehe na mahusiano machafu kadri anavyozidi kukua.
- Anakataa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yake na anafuata tamaa zake mwenyewe.

**Kutengeneza maisha yafanane na ukweli wa Mungu ni kazi ya ufuasi. Ni kumwendeleza mtu awe mfuasi wa Yesu aliyekomaa. Wakati wa kubadilika au kuokoka hakumwingizii mtu hapo hapo ukweli wa Mungu kupitia mwelekeo wake wa mawazo, tabia, dhana, na mfumo wa maisha. Kuingia huko kwa uweli huchukua muda. Hilo ndilo jukumu hasa la kufanya ufuasi.**

## Kitu cha Kwanza cha Lazima kwa ajili ya Huduma ya Watoto

► Je, unafikiri ni kitu gani cha kwanza unachohitaji kwa ajili ya huduma ya watoto?

Huduma ya watoto kwa haraka hutengeneza kikundi cha washiriki ambacho huhusisha watoto na wazazi wanaohusika nao. Kikundi hiki kinakuwa na viongozi wake wa kiasili, watu wanaokuwa na ushawishi kwa wengine kutokana na haiba zao, hata kama hawako kwenye nafasi za utendaji zilizo rasmi. Miongoni mwa wazazi na miongoni mwa watoto kuna viongozi wa asili.

Kitu cha kwanza kwa ajili ya huduma ya watoto ni mazingira ya Kikristo yenye hali chanya ya kiroho. Hapo unaweza kuwalea Wakristo wachanga kiakili, kimwili. kiroho na kijamii.

Hii ina maana kwamba watu wazima ni lazima wawe watu ambao ni mifano ya kiroho. Huwezi ukawatumia watu kwa ajili ya huduma ya watoto ambao siyo wakristo makini na wenye msimamo. Watoto wanaoshawishi watoto wengine kukataa ujumbe wako hawawezi kushiriki.

Huduma yako kwa watoto inakuwa tayari inaanguka kama …

- Watu wazima ambao wanatoa msaada kwenye huduma wako pale kwa sababu ya uwezo wao maalumu walio nao, au kwa sababu nyingine yeyote, lakini siyo watu walio mifano mizuri ya kiroho.
- Watoto wasio na shauku ya mambo ya kiroho wanatawala mazungumzo na mambo mengine ya kijamii ya kikundi.
- Shughuli zote za kiroho zinaongozwa na watu wazima tu ambao hawana ushiriki wowote muhimu kwa watoto.
- Watoto wachache tu ndio wanaotaka kushirikiana na kuonyesha shauku ya kiroho, lakini kijamii hawakubaliki na wengi miongoni mwa wenzao.

Angalia kwenye kikundi cha watoto na jiulize mwenyewe maswali haya. Kama kijana mdogo mgeni wa kiume ameanza kuhudhuria kwenye huduma yetu, ni watoto gani kwenye kikundi watakuwa na uwezekano mkubwa wa kumfuata? Kama kijana wa kike ameandikishwa, atataka afuatane na nani? Je, aina hizo za ushawishi ni nzuri au ni mbaya?

Kitu cha kwanza kwa ajili ya huduma ya watoto ni mazingira ya Kikristo yenye hali chanya ya kiroho. Huduma ya watoto ni lazima ianze na kitu hiki cha kwanza. Kama huduma itakuwa tayari imepoteza mwelekeo huo, kwa vyovyote itabidi ianze upya, vinginevyo haitatimiza lengo sahihi.

## Kanuni ya Maisha ya Kuwasiliana

Maarifa ya Mungu huja katika mahusiano.

Wakati Mungu aliposema na Yakobo, alijitambulisha mwenyewe. Hakusema, "Mimi ni Mungu wa ulimwengu," au "Mimi ni Mungu niliyeumba ulimwengu;" ingawaje kauli yeyote katika hizo mbili ingeweza ikawa kweli. Mungu alisema, "Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka."[168] Mungu hujidhihirisha mwenyewe kupitia watu.

Ibrahimu alikuwa mtu wa imani na wengine walimwamini Mungu kwa sababu yake yeye. Mtumishi wake Eliezeri aliomba kwa "Mungu wa bwana wangu Ibrahimu."[169]

Kuna watu wanaotokea kumfahamu Mungu zaidi kwa sababu ni Bwana wao.

Wakati mwingine tunadhania kwamba huduma ya ufuasi ni kuwaambia tu watu klie wanachotakiwa kukijua na kile wanachotakiwa kukifanya. Sivyo ilivyo. Jambo la kwanza, unapaswa uwaoneshe maisha ambayo wanataka kuyafuata. Kama wanataka kuishi kama wewe unavyofanya, basi, watasikiliza maelekezo yako kuhusu jinsi watakavyofanya.

[168] Mwanzo 28:13
[169] Mwanzo 24:12

Ufuasi ni maisha ya kuwasiliana. Ni mtindo wa maisha, ulio na makusudio yake, na sababu za kutenda na maadili ya msingi ambavyo huhamishwa kutoka kwa mwangalizi hadi kwa mwanafunzi.

**Kanuni ya uhamisho wa maisha inatamka kwamba ufuasi unatokea wakati mwalimu anapopandikiza mtindo wake wa maisha, makusudio yake na maadili ya msingi kwa mwanafunzi.**

Rabi wa Kiyahudi wa karne ya kwanza walielewa ufuasi kama ni uhamisho wa maisha. Wakati kijana alipokuwa anataka kuwa mwanafunzi wa rabi, alikuwa anapaswa kumwomba rabi amkubali. Kama akikubaliwa, ataanza kujishirikisha katika maisha ya rabi. Atakuwa naye kwa muda mwingi, siyo tu kwa ajili ya kujifunza imani kwake, bali kujifunza njia yake ya maisha.

Yesu alijitofautisha na mila ya wakati ule kwa kuchagua watu ambao walikuwa hawajaomba kuwa watakuwa wanafunzi wake. Lakini, alifuata mila ya kufanya ufuasi kwa kushirikishana maisha pamoja kwa lengo la kuhamisha mtindo wa maisha.

Baada ya kifo cha Yesu na kufufuka, baadhi ya wanafunzi wake walikamatwa na kupelekwa kwenye baraza lile lile ambalo yeye alihukumiwa. Baraza la Sanhedrini lilifikiri kuwa labda matatizo yao yatakuwa yamekwisha kwa kuwa Yesu alishauawa. Walidhania kuwa kwa kutumia vitisho vidogo tu vilikuwa vinatosha kuwanyamazisha kabisa wafuasi wa Yesu. Kwa kuwapima wanafunzi wa Yesu, waliwaona kwamba hawakuwa watu wenye elimu ya juu, hakika walikuwa hawajaelimishwa kuliko mjumbe yeyote wa baraza la Sanhedrini. Lakini, Maandiko yanasema kwamba baraza la Sanhedrini wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu.[170] Yesu alishaweka mhuri kwenye maisha yao.

Je, walisema nini juu ya Yesu aliyekuwa ndani ya wale wanafunzi? Je, ilikuwa ni tabia zake au mtindo wake wa kuongea? Inawezekana; lakini kulikuwa na zaidi ya hayo. Waliona ujasiri uliotokana na ufahamu wa wito wa kimungu. Waliona kujitolea kusikoyumba kwa uhakika kwenye ukweli kwa gharama yeyote ile. Waliona heshima kwa ajili ya mamlaka lakini walikataa kukubaliana kuwa na maelewano na unafiki. Kwa hakika mioyo ya wale wanasiasa wakorofi na viongozi wanafiki wa kidini ilipigwa na mshangao kwa kutambua kuwa matatizo yao bado yalikuwa hayajaisha na hapo ulikuwa ni mwanzo tu. Yesu alikuwa amewaongeza kwa idadi na aliendeleza ushawishi wake kupitia uanafunzi.

Dr. Paul Brand alikuwa anawatazama wanafunzi wake vijana wa udaktari walipokuwa wanafanya mazoezi ya kuwapima na kuwachunguza wagonjwa katika hospitali moja nchini India. Wakati alipokuwa anamtazama mmojawapo wa hawa wanafunzi akimhudumia mgonjwa kwa unyeunyekevu, alishangazwa na hisia iliyokuwa inaonekana kwenye uso wa kijana huyu aliyekuwa kwenye mazoezi. Ile hisia ilifanana sawasawa na hii iliyokuwa inaonekana kwa Dr. Pilcher, daktari wa upasuaji aliyekuwa mwalimu wa Dr.

[170] Matendo 4:13

Brand huko Uingereza. Dr. Brand aliwaelezea wanafunzi wa mazoezi kwamba alibadilika kwa mshangao huo kwa sababu alijua kwamba Dr. Pilcher hajawahi kuwa India, na hakuweza kujua ni kwa vipi mwanafunzi huyo wa mazoezi aliweza kumuigiza yeye. Mwishowe, mmoja wa wanafunzi wa mazoezi akasema, "Hatumjui mtu yeyote kama Dr. Ficher, lakini Dr. Brand, hiyo ilikuwa ni uhusika wa sura yako aliyokuwa ameivaa."[171]

Ni kile unachofundisha wakati hukusudii kukifundisha ndicho kitakuwa na matokeo makubwa. Huwa unafudisha sana wakati hukusudii kufundisha chochote. Kama mtu mmoja alivyosema, "Unafundisha kidogo kwa kile unachosema, unafundisha zaidi kwa kile unachofanya, na unafundisha sana kwa jinsi ulivyo."

Kuwa na tahadhari sana kwa nguvu ya mfano wako ulivyo. Siku zote unafundisha. Zidi sana unafanya huduma ya uafusi kupitia mtindo wako wa maisha.

Unamwonesha mtu jinsi ya kuwajibika kwenye matatizo yake kwa njia ile ile ambayo wewe unawajibikia matatizo yako mwenyewe.

Upendo, heshima na uvumilivu ni mambo muhimu kwa ajili ya kumsaidia mtoto. Watu wengine wana uwezo zaidi wa kuwa na upendo, heshima, na uvumilivu kwa watoto kuliko watu wengine.

Unaonesha kwamba unamthamini mtu kama utampa ustahimilivu na umakini wote. Usiwe na papara au haraka wakati unapozungumza naye. Tafakari mnyumbuliko wa mwili wako unaelezea nini kama unataka kumwacha, unataka kwenda kwenye jukumu lako jingine, unafanya shughuli nyingine wakati yeye anaongea au umeelekeza umakini wako kwa mtu mwingine wakati uko naye.

Fanyia mazoezi tabia nzuri za kusikiliza. Ishara nzuri za kusikiliza ni mawasiiano ya macho, umakini unaoonekana dhahiri, kupuuzia mambo yanayotaka kuvuruga, na kuonesha mwitiko mzuri katika furaha ya anayezungumza au hisia zingine.

Kama kwa uhakika utakuwa ni lazima uharakishe na huwezi kutulia ili umsikilize, unaweza ukajieleza. Hilo halitawaudhi ikiwa kwa kawaida huwapa uangalifu wanaohitaji. Kama kwa ujumla unaona una majukumu mengi yatakayoweza kukukosesha nafasi kwa ajili yao, ukifikiria kwamba unahitaji kufanya jambo, unapaswa uache na ufikirie kazi yako ya uhakika ni ipi.

► Je, ni watoto gani walio sehemu ya maisha yako? Kuna njia gani unazoweza kuwaonesha kwamba wao ni muhimu? Je, unazo tabia ambazo unapaswa uzibadilishe?

Kupatikana kwetu kwa ajili ya Mungu ni muhimu zaidi kuliko uwezo wetu kimwili na kiakili. Mungu anataka kupatikana kwetu kuliko uwezo wetu kimwili na kiakili. Mungu atatoa uwezo wa kimwili na kiakili unaouhitajika kwa ajili ya kutimiza wito wake.

---

[171] Paul Brand na Philip Yancey, *In His Image*. (Grand Rapids: Zondervan, 1984), 18-19

Vijana wadogo wana tabia ya kutotulia katika mambo mengi. Kutoka siku moja kwenda siku inayofuata wanaweza wakabadilika kuonekana katika kiroho kwenda katika kuonekana waasi, Kutoka kwenye ukarimu kwenda kwenye uchoyo, au kutoka kukomaa kwenda kwenye utoto. Hiyo siyo kwa sababu ni wanafiki. Bado wako kwenye kuendelea kukua, na utu wao bado haujawa thabiti.

> "Wakati mtu mzima anapokuwa hamwonei tena huruma kijana mdogo, manufaa yake katika ulimwengu huu ni kama yamemalizika."
> - George MacDonald

Vijana wadogo bado hawajatulia, lakini wanakutaka wewe uwe thabiti katika matarajio yako. Kama katika nyakati zao mbaya unawaambia ninyi hamtafaa kwa jambo lolote, unashusha matarajio yao. Bado hawajijui wanaenda kuwa nani, na tathmini yako itaathiri kile wanachoenda kuwa.

Zungumzia zaidi kuhusu mpango maalumu wa Mungu uliopo kwa ajili yao. Waambie kwamba Mungu amewapa kila mmoja wao uwezo maalumu wa kimwili na kiakili. Elezea kuhusu kuridhika kwa kutafuta mapenzi ya Mungu.

Kijana mdogo mwenye karama ya uongozi anaweza kuwa na mawazo mengi lakini asifanye vizuri katika kukataa yaliyo mabaya. Kipengele cha kukua ni uwezo wa kimwili na kiakili wa kutofautisha kati ya mawazo mzuri na yale mabaya. Msadie ajifunze kuhusu hekima, lakini usimkatishe tamaa katika kuwa na mawazo ya ina mbalimbali.

Juu ya mambo yote, kumbuka kwamba Mungu anao mpango wa mwisho kwa kila mtu, na anafanya kazi katika kuuleta juu utumike. Omba kwa ajili ya ufahamu ili uweze kufanya kazi pamoja na mpango wa Mungu wa maendeleo kwa ajili ya mwanafunzi. Omba kwa ajili ya miujiza ya neema na uangalizi wa kimungu katika maisha ya mwanafunzi ambayo yatampeleka kwenye mwelekeo sahihi.

## Kuboresha Mbinu za Kufundisha.

► Je, kuna tabia gani katika mbinu nzuri ya kufundisha? Je, unapomwona mtu akifundisha, unajuaje kama ni mwalimu mzuri?

Mwalimu ndiye mwenye kuthibiti mbinu ya kufundishia. Kuna vipengele kadhaa vya mbinu za kufundishia ambavyo mwalimu anapaswa avipange kwa makini.

### (1) Kiwango cha Maelekezo

Watu ni kama majagi yenye shingo nyembamba. Kama utamimina kitu ndani kwa haraka sana, hakitaweza kwenda ndani chote. Kama utafundisha taarifa kwa haraka sana, hawataweza kujifunza. Mtu anapojifunza taarifa mpya, ni lazima aiunganishe na kile anachokijua. Ni lazima pia afikiri kwamba ni kwa jinsi gani taarifa hiyo itafanya kazi kwenye maisha yake. Kwa hiyo, kuna ukomo wa kasi ya mtu kujifunza kutokana na taarifa hizo.

Ni vyema kuweka jambo moja katika hali ambayo haitasahaulika kuliko kutaka kumaliza mambo mengi ambayo kwa vyovyote vile watasahau. Ni vyema wakajifunza jinsi ya

kutumia kipengele kimoja kwa usahihi kuliko kusikia vipengele vingi vya taarifa ambavyo hawaoni umuhimu wake.

### (2) Majadiliano ya Kikundi

Watu wengi wanahitaji kuwa na majadiliano na watu wengine wakati wanajifunza. Wanahitaji waweze kuuliza maswali na kurudia dhana katika maneno yao wenyewe. Kama mtindo wa mwalimu wa kufundishia hautaruhusu mjadala kutoka kwa wasikilizaji, hawataweza kujifunza mambo mengi

Unaweza ukatanguliza wazo la somo kwa njia ya swali, mfano "Kwa nini ni muhimu ku…?" au "Ni kitu gani muhimu sana unachojua kuhusu…?" Usipoteze muda mrefu kwenye majadiliano ya utangulizi, lakini tumia muda huo kuwafanya wawe na shauku ya kusikiliza.

Baada ya kuwasilisha baadhi ya taarifa, unaweza ukauliza swali ambalo litawafanya waweze kufafanua dhana kwa maneno yao wenyewe. Kwa mfano, "Kuna makosa gani aliyofanya mtu aliyeko kwenye taarifa…?" Uliza maswali ambayo yatakapojibiwa yataambatana na maelezo ya ufafanuzi, badala ya maswali ambayo yanajibiwa kwa ndiyo au hapana. Maswali yanabidi yawe marahisi katika kiwango cha kuwawezesha watoto wengi kupata majibu mazuri kutoka kwa watoto wenzao. Kwa kawaida kama majibu yao yataonekana yana makosa watapoteza hamu na au shauku yao.

- Usimpe mtoto shinikizo la kushirikisha jambo fulani la binafsi. Badala yake, jaribu kutengeneza mazingira ambayo atajisikia yuko huru kuwasilisha yeye mwenyewe.
- Usiruhusu wanafunzi wachache tu kuwa ndio wa kusema katika kila kitu. Unaweza ukaelekeza mambo mengine kwa wale ambao wanaonekana siyo wasemaji katika kikundi: "Je, unafikiri nini, Charles?" Unapaswa uwatie moyo na wengine kuwa washiriki: "Je, wengine mnafikirije?"
- Usiruhusu watu katika darasa kuwa na mijadala yao wenyewe huku wakisahau kuwa wao ni sehemu ya kikundi.
- Usiruhusu mtu yeyote kuingilia kati hata kama ni mtoto mdogo anaongea.
- Jaribu kuthibitisha kila wazo linalotolewa kwa namna fulani kabla ya kukosoa hilo wazo. Kama linahitaji masahihisho, jaribu kufanya hivyo kwa kulipanua zaidi.

### (3) Umuhimu

Wakati wote jiulize wewe mwenyewe swali hili. "Je, kwa nini jambo hili ni muhimu?' Kama wewe mwenyewe hujui, hata wao pia hawatajua. Je, kuna tofauti gani itakayofanyika ndani yao? Je, kuna mambo yoyote maalumu wanayopaswa kuyafanyia kazi kwenye maisha yao? Kama huwezi kufikiria lolote kati ya hayo, hata wao inawezekana wasiweze kufikiria jambo lolote.

Kama wataona kwamba mada hiyo ni muhimu kwao, watasikiliza kwa umakini mkubwa. Ili kuweza kulithibiti darasa, shughulika zaidi na kuifanya mada yako iwe ya kuvutia kuliko kushughulika zaidi na kudumisha nidhamu.

**(4) Umuhimu**

Onesha matokeo ya ukweli unaoufundisha. Je, kunakuwepo na matokeo gani wakati watu wanapoujua ukweli na kuufuata? Je, kunakuwepo na athari gani wakati watu wanapoukataa huu ukweli?

Watie moyo kwa mada zenye mvuto. Epuka kutumia muda mwingi kwenye mambo madogo madogo. Wasimulie hadithi nyingi kuhusu watu wengine ambao wamewahi kuishi sawa na ukweli unaoushirikisha. Hawataweza kuwa na kumbukumbu ya mihutasari yako ya masomo, lakini wataweza kukumbuka hadithi zako.

Waeleze kuhusu mashujaa. Wanataka wawaone watu ambao watawakubali na kuwaiga. Waelezee kuhusu mashahidi wa imani—siyo wale walioona miujiza mikubwa tu, lakini wale waliokamilisha kufanya matendo makubwa kwa kutumia nguvu za Mungu. Wasaidie waone kwamba jukumu la kanisa la kueneza injili na kufanya uanafunzi ni changamoto kubwa na kazi inayohitaji zaidi kukamilishwa duniani.

**(5) Vielelezo vya Kufundishia**

Kama kutakuwepo na uwezekano, tumia picha za rangi wakati unapokuwa unaelezea hadithi. Unapokuwa unafundisha dhana, andika maneno muhimu kwenye ubao. Watayakumbuka kwa wepesi zaidi kama wataona na kusikia.

**(6) Vitendo**

Watu hujifunza kwa kufanya kwa vitendo. Watoto wanaweza kujifunza kwa kutengeneza kitu fulani, au kwa kuigiza kutoka katika hadithi. Mwalimu hata anaweza kuwaelekeza kuigiza kutoka ndani ya Biblia kadri anavyokuwa anaielezea. Hatua hii inachukua muda, kwa hiyo huwezi kuwa na onyesho kwa ajili ya hadithi kila siku, lakini itakupasa uangalie njia ya kuweza kuwa na onyesho mara kwa mara.

► Baadhi ya watu katika kikundi wanaweza kuzungumzia kuhusu masomo au mahubiri ya hivi karibuni waliyowasilisha na wakaelezea jinsi ambavyo wangeweza wakavitumia vipengele hivi vinavyohusiana na mbinu vizuri zaidi. Baadhi wanaweza wakaelezea mambo ambayo tayari wanayafanya katika kutumia vipengele hivi.

## Mtindo wa Injili kwa Watoto: Kitabu kisichokuwa na Maneno.

Kila ukurasa wa Kitabu kisichokuwa na Maneno una rangi tofauti na unawakilisha sehemu fulani ya injili.

Ufuatao hapa chini ni muhtasari wa ujumbe unaokwenda na kila ukurasa. Wakati unapotumia Kitabu kisichokuwa na Maneno itakupasa uongezee ufafanuzi zaidi na umwache mtoto aingilie na kuuliza maswali.[172]

Kumbuka: Watu wengine huweka rangi ya dhahabu kwenye ukurasa wa kwanza, kisha kufuatiwa na nyeusi, na kuendelea na rangi nyingine kufuatana na utaratibu ulioonyeshwa hapa chini.

**Dhahabu:** Rangi ya Dhahabu huwakilisha mbingu, mahali ambapo Mungu anatuandalia sisi makao yetu. Maisha yetu hapa duniani yatakapokuwa yamemalizika, tutaishi na Mungu mbinuni mahali ambapo hakuna huzuni, maumivu au uovu.

**Nyeusi:** Rangi Nyeusi inatukumbusha kuhusu dhambi, na mambo mengi mabaya ambayo tumeyafanya. Biblia inasema kwamba kila mtu ametenda dhambi. Kwa ajili ya dhambi, tumekuwa kwenye matatizo na Mungu. (Katika pointi hii, utapaswa umwambie mtoto akiri kwamba yeye ni mwenye dhambi.)

**Nyekundu:** Habari njema ni kwamba Yesu, Mwana wa Mungu, alikufa kwa ajili yetu ili tuweze kupata msamaha wa dhambi zetu. Rangi Nyekundu inawakilisha damu ya Yesu. Yesu alikufa, lakini alifufuka kutoka katika wafu na kwa sasa anaandaa makao huko mbinguni kwa ajili yetu.

**Nyeupe:** Wakati Mungu anapokuwa ametusamehe dhambi zetu anatufanya tuwe wasafi kwenye mioyo yetu. Huzichukua dhambi zetu zote tulizozitenda. Unaweza kusali na kumwomba Mungu akusamehe dhambi zako. Mungu yuko tayari kukusamehe ikiwa utajuta dhambi zako.

**Kijani:** Wakati unapokuwa umeshasamehewa dhambi zako, wewe ni mtoto wa Mungu. Utakuwa unakua kwenye uhusiano wako na Mungu. Rangi ya Kijani inaamaanisha kukua. Utajifunza zaidi kuhusiana na Mungu na utajifunza jinsi anavyokutaka uishi. Unapaswa usome Biblia yako, uombe kila siku, na usikilize kutoka kwa watu wengine ambao wanajua jinsi ya kuishi na Mungu kwa ukaribu zaidi.

---

[172] Kwa taarifa kuhusu utasema nini wakati utakapokuwa unatumia kitabu kiitwacho Kitabu kisichokuwa na Maneno, tembelea tovuti hizi:
http://berean.org/bibleteacher/wb.html
http://www.abcjesuslovesme.com/ideas1/bible/bible-themes/1150-wordless-book.
Kwa taarifa kuhusu jinsi utakavyoandaa kitabu kiitwacho Kitabu kisichokuwa na Maneno, au chenye mambo ya kufanana, ona tovuti hii:
http://www.teenmissions.org/resources/wordless-book-bracelet/.

## Kazi za Kufanya

(1) Angalia tena nyenzo zote zilizoko kwenye somo hili chini ya kichwa cha habari “Kanuni ya Uhamisho wa Maisha.” Tafakari muingiliano wako na watoto, siyo tu kwenye mafundisho, bali wakati wowote unapokutana nao. Je, unahitaji nini ili ubadilike? Fanya mazungumzo na mtu anayekujua vizuri. Mwoneshe (kama ni baba au mama) nyenzo za masomo ulizo nazo na mfafanulie tathmini inayohusiana na wewe mwenyewe. Omba wakupe maoni yao. Utahitajika utoe taarifa kwamba uliifanya kazi hii, lakini unaweza kuchagua aidha kutoa au kutokutoa undani wa tathmini yako.

(2) Andaa somo au mahubiri kwa ajili ya watoto. Yaandae kwa uangalifu mkubwa ukitumia vipengele vya mitindo. Uwe tayari kutoa ufafanuzi ni kwa jinsi gani uliyaandaa.

(3) Tafuta njia yeyote ya kununua au kutengeneza Kitabu kisichokuwa na Maneno. Jifunze ushirikishaji na ushirikishe kwa angalao watu wasiopungua watatu. Andika sura moja inayoelezea uzoefu wako kwa kila mmoja.

# Somo la 15
# Mpango wa Kanisa

## Utangulizi

Eric anapenda kuzungumzia kuhusu miaka ya awali ya kanisa lake. "Tulianza kwa kukutanika kwenye bustani ya kupumzikia, tukimkaribisha kila mtu tuliyemwona. Wakati wa kipindi cha baridi, tulikutanikia kwenye basi mbovu la zamani. Hatukuwa na vyumba vya maliwato. Baadaye, tulihamia katika ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo kwa muda, kisha tukapangisha nafasi kwenye jengo moja la zamani la kanisa."

Kanisa la Eric lilikuwa linakua katika miaka hiyo. Watu waliokuwa wamejitoa kwa ajili ya kanisa hawakuwa wamevutiwa na jengo la kanisa. Walikuwa wamevutiwa na kundi la watu.

Kwenye somo hili, tunapozungumzia kuhusu mpango wa kanisa, hatuzungumzii kuhusu jengo la kanisa. Makanisa mengi makubwa wanayo maelezo kuhusiana na jinsi walivyoanza wakiwa katika mazingira magumu.

Baadhi ya makanisa yanasema kwamba hayawezi kuwa kivutio kwa watu kwa sababu majengo yao hayaridhishi kwa uzuri. Ukweli ni kwamba wanakosa kitu kingine ambacho ni muhimu sana kuliko hata jengo.

## Maana ya Mwaliko wa Kanisa

Wakristo kila mahali hupenda kuwaalika watu wengine wahudhurie kwenye makanisa yao. Wana mategemeo kwamba wageni watalipenda kanisa na watakuwa wanapenda kuendelea kuhudhuria pamoja nao. Wanategemea kwamba wageni watakubaliana na injili.

► Je, wakati unapomwalika mtu kuhudhuria kwenye kanisa lako, mwaliko huo unamaanisha nini? Unatoa nini?

Hatuwakaribishi kuhudhuria kwenye ibada zetu kwa ajili ya mazoezi ya kidini, kana kwamba hilo litatimiza hitaji au kukamilisha wajibu. Hatuamini kwamba kwa kushiriki mila za kidini kutaleta ufanisi wowote kwa mtu ambaye siyo wa imani.

Hatutegemei kwamba wanajua kumwabudu Mungu wakati ambapo bado hawajabadilishwa na au hawajaokoka.

Tunategemea kwamba watapenda upendo wa watu walioko na watataka kuwa pamoja nao tena.

Tunategemea kwamba watakubaliana na injili.

Baadhi ya makanisa wanajaribu kutengeneza programu zao ziweze kuwavutia watu ambao hawana shauku ya kiroho. Wanategemea kwamba kama watu wataifurahia programu yao, watakuwa wanaendelea kuhudhuria kwenye ibada zao. Tatizo ni kwamba kama burudani itakuwa imefanikiwa, inakuwa na mvuto kwa watu wengi ambao hawana shauku iliyo sahihi. Kusanyiko linakuwa la vikundi mchanganyiko ikiwa ni pamoja na watu ambao hawana shauku ya kumwabudu Mungu bali kuburudika na burudani iliyopo katika kanisa. Viongozi wa ibada na wanamuziki wanakuwa ni waburudishaji. Hatimaye, unakuza viongozi wa ibada ambao hawapendi ibada. Kuabudu kunakuwa kumeharibiwa.

► Tafakari swali hili tena. Wakati unapomwalika mtu kuhudhuria katika kanisa lako, unakuwa unatoa nini? Unatakiwa uwe unatoa nini?

Jaribu kufikiria kuhusu mabadiliko makubwa yanayotokea kwa mtu anapokuwa amebadilishwa au kuokoka. Huachana na dini yake ya mwanzo, jambo ambalo linaweza kumtenga yeye na familia yake au marafiki zake. Anatubu dhambi zake, ikimaanisha kwamba atatengana na mambo mengi aliyokuwa amefikiria kwamba yangemfanya awe mtu wa kufurahia. Anajisalimisha kabisa maisha yake kwenye uongozi na mapenzi ya Mungu.

Kwa sababu ya mabadiliko makubwa yanayotokea wakati wa kubadilishwa na au kuokoka, mtu kwa kawaida hakubali kubadilishwa na au kuokoka bila ya kufikiria kuhusu jamii yake atakayoiacha na ile atakayoingia. Kama mtu atavutiwa na ushuhuda wa Mkristo binafsi, anataka kuona jamii ya waaminio ambayo yule Mkristo anaiwakilisha. Atataka aone ni kwa jinsi gani imani inatenda kazi kwa uhakika. Anakuwa na hisia kwamba ujumbe anaousikia tayari umeshatengeneza jamii ya waaminio ambayo ataingia kuwa nayo kama atabadilishwa na au kuokoka. Anakuwa kama anayejiuliza, “Liko wapi kundi la watu wanaouamini ujumbe huu na kuishi kama unavyonena? Itakuwaje kwangu mimi kuwepo kwenye kundi hilo?”

Yesu alihubiri “injili ya ufalme” na mara kwa mara alizumgumzia kuhusu ufalme wa mbinguni. Alisema kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia (Luka 10:9). Watu wanaoingia kwenye ufalme wa Mungu wamekubaliana na uongozi wa Mungu, kuishi kwa mujibu wa sheria zake, na kushiriki maisha pamoja naye. Uaminifu wao kwa Mungu umewafanya wawe familia ya imani.

Kwa kuwa watu wanataka kuona familia ya imani iliyotokana na kuisikia injili, uinjilisti hauwezi kufanywa tu na watu binafsi wakiwashawishi watu wengine binafsi. Hiyo inamaanisha kwamba uwepo wa kanisa la mahali pamoja ni muhimu sana. Kanisa la mahali pamoja linatakiwa liwe la kuvutia kama familia ya imani.

> “Yesu alikuwa amejenga muundo wa kanisa ambalo kwa wanafunzi wake lingeleta changamoto na ushindi juu ya mamlaka zote za kifo na Motoni. Ilianza kidogo kama punje ya haraladi, lakini ikakua kwa kimo na nguvu...“
> - Robert Coleman, *The Master’s Plan*

► Je, ni kitu gani mtu atataka kuona kabla hajajiunga kwenye jamii ya imani?

Kanisa lina asili iliyoundwa na Mungu wajibu uliotolewa na Mungu. Kila kanisa la mahali pamoja linatakiwa lifanye vizuri itakavyowezekana kwenye viwango vya Mungu. Hatupaswi kuligeuza kanisa liwe kwa ajili ya shughuli nyingine kwa ajili ya kuvutia watu. Hatupaswi tujaribu kuliwasilisha kanisa kama kitu tofauti na jinsi lilivyo.

Kama kanisa litakamilisha kusudi ambalo Mungu amelitoa kwake, litawavutia watu sahihi ambao wataunda kikundi chenye kumaanisha.

## Tabia za Kanisa la Mahali Linalovutia

**(1) Washirika huonyesha kwamba uhusiano wao na Mungu ni wa uhalisia na unaotosheleza.** Watu wasiookoka hawana uhusiano wowote na Mungu. Mtu atakapoona ni kwa jinsi gani maisha ya kuishi pamoja na Mungu yalivyo, ndipo atakapoona hitaji la kuwa na uhusiano naye. Washirika huonyesha hali hii kwa kutoa ushuhuda wa kufurahia kumjua Mungu na kuishi maisha ya kujikabidhi kabisa kwa Mungu. Kama mshirika atakuwa bado anaishi kwenye dhambi wakati anapokuwa hayupo kwenye kanisa, huyo anaonesha kwamba hajaridhika na Mungu.

**(2) Kanisa huwasilisha mafundisho ya imani ya kweli na pia kama masharti kwa ajili ya kuwa na uhusiano na Mungu.** Tunafundisha mafundisho ya imani kwa sababu ni kweli, na siyo tu kwamba ni kweli. Fundisho la imani ni kitu ambacho tunahitaji kwa kuwa tunataka tukaishi pamoja na Mungu. Kama ambavyo ndoa ni uhusiano unaoambatana na ahadi za ndoa, uhusiano wetu na Mungu una ahadi zinazoambatana na kujitoa kabisa kwetu. Fundisho la imani linafafanua jinsi tunavyoishi kwenye uhusiano na Mungu.

**(3) Kanisa linadhihirisha furaha ya kumwabudu Mungu.** Furaha ya kuabudu katika ibada siyo sawa na furaha inayopatikana kwenye burudani. Watu ambao hawajui jinsi ya kumwabudu Mungu wa kweli hawana uwezo wa kuisikia furaha inayotokana na kumwabudu Mungu. Tumewekwa kwa ajili ya kuabudu; kwa hiyo, mtu ambaye hajaokoka anapoona ibada ya sifa inavyoleta furaha, yeye atakuwa na hitaji la kuipata.

**(4) Washirika wa kanisa huonesha kusudi la maisha kwa ajili ya mtazamo wa maisha ya milele.** Wakristo hawahitajiki kuwa na mashaka kama maisha yao yana umuhimu. Wkristo wanayo faraja na ujasiri katika nyakati ngumu za maisha. Watu ambao hawajaokoka wanajitahidi kutafuta kusudi la maisha, na hawajui jinsi ya kukabili kifo au uzima wa milele.

**(5) Kanisa huonesha kipaumbele cha mahusiano, badala ya malengo ya ubinafsi.** Kanisa halifanyi uinjilisti au kulea washirika wake kwa sababu za kujenga shirika lake. Watu wa dunia hudharau mahusino au hutumia mahusiano kwa ajili ya malengo ya ubinafsi.

**(6) Ujumbe wa kanisa unatosheleza mahitaji ya ndani kabisa ya kiroho.** Mtu mbaye hajaokoka huwa na kiu ya kiroho ambayo haiwezi ikatoshelezwa na kitu chochote

kinachotolewa na ulimwengu huu. Mahubiri na mafundisho na ushauri vinavyofanyika katika kanisa vinapaswa vishabihiane na au viendane na mahitaji halisi ya watu.

**(7) Kanisa ni mahali palipo na familia ya imani yenye upendo na inayowajali washirika wake.** Vikundi vya aina nyingine vinaweza vikasaidia mahitaji ya wanachama wake, lakini ni Wakristo peke yake wenye uwezo wa kuwa na ushirika wa kweli wa Kikristo.

► Je, ni kwa njia gani maalumu ambazo kanisa linaweza likadhihirisha tabia hizi? Je, ni njia gani ambazo kanisa linapaswa lianze kufanya ili liweze kuonyesha vipaumbele vilivyo sahihi?

## Kuliandaa Kanisa kwa ajili ya Uinjilisti

Kanisa linapaswa lihakikise kwamba programu zake na muundo wake unasaidia katika kutimiza lengo la umisheni kwa ajili ya huduma ya uinjilisti na ufuasi. Kila kitu ambacho kanisa linafanya kinapaswa kiende sambamba na kipaumbele hicho.

### Kuwakaribisha Wageni

Kanisa linapaswa lijiandae kuwakaribisha wageni na kuwasaidia wajisikie wako vizuri. Watu wengine hawana mazoea na taratibu za kanisa. Wanapolitembelea kanisa, hawajui ni nini cha kutarajia. Hawajui ni nini kinatarajiwa kutoka kwao. Kwa muda wa dakika chache za kuwasili kwao katika kanisa, aidha watafurahia kwa kuja kwao, au wakajisikia ni afadhali wasingekuja. Kanisa linapaswa liandae watu mahususi watakaokuwa tayari kuwakaribisha wageni kanisani.

Kanisa halipaswi kuwatenga watu kwa ajili ya umaskini wao. Uvaaji unaotarajiwa watu wavae katika kanisa haupaswi uwatenganishe watu maskini walioko katika kanisa.

Kanisa linapaswa liwe tayari kutoa huduma kwa watoto ambao huja bila wazazi wao. Watu wachaguliwe na wapewe mafunzo maalumu kwa ajili ya kuwahudumia watoto wanaohudhuria katika kanisa.

Mgeni anapaswa aalikwe kuhudhuria kwenye kusanyiko la kikundi kidogo au kusanyiko la seli za nyumbani ambako anaweza kujifunza zaidi na kuuliza maswali.

### Kuwafikia Watu wa Nje

Jukumu la kwanza la kanisa ni kulichunga kusanyiko la washirika ambao wamejitoa kabisa kwa ajili ya kanisa. Hata hivyo, kanisa siku zote linapaswa liwe linawafikia majirani na watu wengine walioko nje ya kanisa. Kanisa ni lazima liwe na shughuli za kufanya ambazo watahakikisha kwamba watu walioko nje ya kanisa wataona majukumu mbalimbali yanayofanywa na kanisa na hata kuweza kuisikia injili. Baadhi ya shughuli hizi zinaweza kuwa za kujitokeza. Inawapasa viongozi kupanga shughuli zingine vile vile. Washirika walio na uwezo wanapaswa waalikwe na kupewa mafunzo yanayohusiana na hizi shughuli za nje za kanisa.

Kanisa linapaswa litafute njia za kushughulikia mahitaji ya majirani wanaowazunguka. Kipaumbele siku zote kiwe ni kuonyesha upendo wa Mungu na kudhihirisha kanuni za kibiblia.

**Huduma ya Kikundi cha Seli**

Wakati mtu anapokuwa ameokoka hapaswi tu kukaribishwa kwenye huduma za ibada. Anapaswa aalikwe kwenye mpango wa haraka wa ufuasi. Jambo hili linaweza kuanza kwa kuwepo na ziara za binafsi zitakazofanywa na mchungaji. Mtu huyu pia anaweza kualikwa kwenye huduma za vikundi vya seli za nyumbani zinazokutana kila wiki.

Kwa kawaida kanisa lenye afya na ustawi huwa na aina ya vikundi vidogo mabimbali ambako maisha ya kiroho yanasimamiwa. Hivi vikundi vidogo vinaweza vikawa ni nyumba za kanisa, madarasa ya shule za Jumapili, au vikundi vya aina nyingine. Uwajibikaji wa kiroho na mabadiliko ya maisha kwa kawaida hutokea kwenye vikundi vidogo. Viongozi wa kanisa wanapaswa wahakikishe kwamba vikundi vidogo vinakuwepo ambavyo vitakamilisha malengo haya. Kama taratibu zilizopo na au miundo iliyopo ndani ya kanisa haviwezeshi kuwepo kwa maisha ya kiroho, mabailiko yatahitajika.

**Uanachama Unaoonekana**

Watu wanaotaka kuwa washirika wa kanisa wanataka hasa kujua kushiriki kikamilifu kutamaanisha nini. Baadhi ya makanisa wanadai kutokuwa na muundo wa uanachama, lakini kila kanisa lina jinsi ya kujua washiriki ni kina nani. Kila mtu huwa anahitaji kujua watu wanaoshiriki katika kanisa ni watu wa aina gani.

Kila mtu anapaswa kujua ni mambo gani yanayohitajika kwa ajili ya uanachama. Mahitaji na maelezo ya mchakato wa kuwa mwanachama wa kanisa inabidi yachapishwe.

Mtu aliyebadika na au kuokoka aliye tayari kujikabidhi katika kanisa anapaswa awe tayari mara moja kulisaidia kanisa. Hali hiyo haimaanshi kwamba atapaswa apewe aina fulani ya nafasi au majukumu ya uongozi. Ni muhimu kwake ajue kwamba yeye ni sehemu ya kanisa.

**Uwajibikaji wa Haraka kwa Watu Wapya Waliobadilika na au Kuokoka**

Ufuasi huanzia pale mtu anapokuwa amebadilika na au ameokoka. Mtu aliyebadilika na au kuokoka anakuwa na mahitaji kadhaa ya haraka. Kuendelea kwenye uhusiano na Mungu ambo ndio tu umeanza, anahitaji kujua jinsi ya kuomba na kusoma Biblia. Pia anahitaji jamii mpya ya marafiki wa sababu kwa vyovyote atawapoteza marafiki wake wengi wa zamani. Atahitaji apate mwongozo katika mambo mengi ya mtindo wa maisha.

Kanisa linapaswa lianzishe mara moja huduma ya ufuasi kwa mtu mpya aliyebadilika na au kuokoka. *Mara moja* haina maana ya Jumapili inayofuata. Inamaanisha kwamba mara tu anapokuwa anainua kichwa chake kutoka kwenye maombi kwa ajili ya kuokoka. Mtu mmoja ni lazima achukue wajibu wa mawasilino ya kila siku na huyu mtu mpya aliyeamua kubadilika na au kuokoka angalao kwenye wiki yote ya mwanzo. Atapaswa aweze

kukutana na Wakristo wengine katika kanisa la mahali pamoja. Atapaswa awe na nafasi za kujadili kuhusu mabadiliko yanayotokea kwake na aulize maswali.

Huyu mtu mpya aliyeamua kubadilika na au kuokoka atapaswa aalikwe na ajiunge kwenye kikundi kidogo ambacho anaweza akauliza maswali na kutiwa moyo. Ikiwezekana, atapaswa atambulishwe kwa washirika wengine kadhaa kwenye kikundi katika siku za mwanzo kabla ya kikao cha kwanza atakochohudhuria kwenye kikundi. Baadhi ya washiriki katika kikundi wanaweza wakampigia simu kabla ya kuanza kwa kikao kwa ajili ya kuendelea kumwonyesha urafiki pamoja naye na kumkaribisha ahudhurie kwenye kikao cha kikundi. Hali hii itaanza kumjengea hisia za kujisikia yuko na anahusika katika jamii.

Mtu mpya aliyeamua kubadilika na au kuokoka atapaswa kujiunga na kikundi kwenye kikao kitakachofuata. Masomo yatafanyika kwa mzunguko ili kwamba mshiriki katika kikundi aweze kuingizwa wakati wowote. Kwa njia hii mtu mpya aliyeamua kubadilika na au kuokoka anapata msaada wa kikundi mara moja. Washiriki huhitimu kozi kibinafsi wanapokuwa wamemaliza masomo yote.

### Kujali Mahitaji

Kanisa ni lazima liweze kujali mahitaji ya kifedha ya watu wa kusanyiko lake. Mahitaji mengi yatatimizwa na watu kusaidia watu wengine kwenye kusanyiko la kanisa bila ya kuhusisha kuongozwa na viongozi wa kanisa. Kama watu wengi katika kanisa hawaoni kujisikia kwa ajili ya kusaidia watu wengine, bado watakuwa hawajatengeneza kanisa lenye ukomavu.

Kanisa linatakiwa liwe na mashemasi ambao watakuwa wanahakikisha kwamba mahiaji yanatambulika. Kanisa katika kitabu cha Matendo kilichagua mashemasi wa kwanza kwa ajili ya kusudi hili.

Kujali mahitaji ni muhimu kwa ajili ya umisheni wa injili. Watu ni lazima wawe na umakini wa kuangalia kwamba kanisa ni familia ya waaminio ambao washiriki hujali kwa ajili ya mtu mwingine.

### Kazi ya Kufanya

Jaribu kufikiria kanisa linalotenda mambo yote tuliyozungumzia katika somo hili. Andika kuhusu mtu wa kufikirika ambaye hutembelea kanisa, akaamua kubadilika na au kuokoka, na akawa mshirka anayejitoa kwa kanisa. Elezea hali yote jinsi ilivyotokea.

# Somo la 16
# Wafuasi wa Kweli

## Kumfuata Yesu

► Je, inamaanisha nini kuwa mfuasi wa Yesu?

Baadhi ya watu hufikiri kwamba Mkristo ni mtu yeyote aliye mzuri. Wengie hufikiri kwamba kuwa Mkristo maana yake ni kuamini baadhi ya mambo fulani. Wengi wa watu hawa, imani hazileti tofauti yeyote ya maana kwenye maisha yao.

Watu wengine wako karibu na ukweli. Wanajua kwamba ni lazima kutakuwepo na kipindi cha kubadilika na au kuokoka, wakati mtu anapokuwa Mkristo. Wanaamini kwamba hali hii inatokea wakati mtu kwa kipindi fulani alipoamini kuwa alikuwa amesamehewa. Watu wengi wanaamini kwamba mtu aliyeokoka kwa ukweli ana uhakika wa mbingu hata kama akifanya jambo lolote baada ya kuokoka.

Ni ukweli dhahiri kwamba kuokoka ni lazima iwe jambo la kweli. Ni ukweli dhahiri kwamba msamaha unapatikana kwa neema kwa kukubaliana na imani. Ni ukweli dhahiri kwamba Mkristo anaishi kwa kumtii Mungu. Lakini hayo yote hayatoshi kumaanisha ndio kuwa mwanafunzi wa Yesu.

Tunaweza kuona ni nini kinachotokea wakati wa imani ikifanywa ndiyo kigezo pekee cha kuwa Mkristo—inatupeleka kwenye fundisho kwamba amri za Mungu siyo lazima kuzitii na au kufuatwa na Mkristo (antinomianism. Badala ya kuwa neema ya bure, inakuwa ni neema ya kubuniwa ambayo inajifanya kuhalalisha dhambi.

Makanisa ambayo yanatangaza neema ya kubuniwa yana watu wanaohudhuria katika ibada za kanisa lakini wanaishi kwenye dhambi za wazi kabisa. Wachungaji wao na viongozi wao wengine wanaishi maisha mazuri kuliko washirika wa makusanyiko yao lakini inawezekana pia wanaishi kwenye tabia za maovu. Wanasema siyo lazima kuishi kwenye utiifu wote kwa Mungu kwa sababu tumeokolewa kwa neema. Wamepoteza agizo lile Yesu alilolitoa kwa kanisa, ambalo ni kuwaweka watu kwenye utiifu wa maagizo yake Kristo. Kazi maalumu ya kanisa ni kuwageuza wenye dhambi wamrudie Mungu na kuwa watakatifu waabuduo Mungu, na kanisa halina sababu yeyote nzuri zaidi ya kulifanya lisiendelee kuwepo.

Hata makanisa ambayo yameshikilia msimamo wa umuhimu wa kumtii Mungu wana watu kadhaa ambao wako kwenye mrengo wa kimakosa. Wameyaweka maisha yao yakubaliane na matakwa ambayo wanaamini ni sahihi, lakini hawana ile roho ya kumfanania Kristo. Ni wakatili na wasiokuwa na msamaha. Hawawezi kutoa samahani yenye unyenyekevu na neema. Ni wepesi katika kuwahukumu watu wengine. Wana imani na baadhi ya watu wachache tu. Hawaonekani kuwa na mashaka na haki yao wenyewe. Wana majibu kwa

kila jambo, na hawana heshima kwa yeyote anayeonekana kutofautiana au kutokukubaliana nao. Hawana mpango wala bidii yeyote ya kuwatafuta waliopotea, bali wana mipango na bidii ya kutetea maoni yao wenyewe. Wamejitosheleza wenyewe, na hawana mpango wa kubadilika.

Je, watu kama hawa kweli wanamjua Yesu na kutaka wamfanane naye?

Kuwa Mkristo inamaanisha ni kuwa mwanafunzi wa Yesu.

Je, inamaanisha nini kuwa mwanafunzi? Je, ni kumtii Kristo? Kwa hakika, angalao kwa kiwango kikubwa. Katika Agizo Kuu la Yesu mahali alipowaambia waende kila mahali wakawafanye mataifa kuwa wanafunzi, alisema, "na kuwafundisha kuyashika yote."[173]

Kutii maagizo ya Yesu hayo yote hayatoshi kumaanisha ndio kuwa mwanafunzi.

Wanafunzi wa rabi wa Kiyahudi walishiriki maisha yanayofanana na wao, siyo tu katika kujifunza mafundisho yao, bali pia na mitindo yao ya maisha. Walijifunza tabia zao na vipaumbele vyao.

Wakati Yesu alipowaita wanafunzi, akisema, "Njoo unifuate,"[174] hayo ndiyo aliyokuwa amemaanisha. Yesu bado hata wakati huu anawaita wanafunzi kupitia kwenye injili.

Je, inatokeaje mtu kuwa mwanafunzi?

Kwanza, ni lazima uamini katika yeye—kama huwezi kuamini katika yeye, huna sababu ya kumfuata.

Unapaswa ubadili mwelekeo wako unakokwenda. Hakuna mtu yeyote anayeanza na kuwa mfuasi wa Yesu—tunaanza kwenda kwa njia zetu wenyewe. Unapaswa uamue kumfuata Yesu badala ya njia zako mwenyewe. Hiyo ina maana unaona kuna kitu kibaya kwa njia yako mwenyewe. Kumfuata Yesu kunaanza na toba – huwezi ukamfuata Yesu bila ya kuwa umejutia dhambi zako. Kama hujawa na majuto ya dhambi zako kwa kiwango cha kutosha kuachana nazo, bado utakuwa unaenda kwenye njia zako mwenyewe.

> "Yesu Kristo anasisitiza kuondoa kutoka katikati ya dunia chochote cha aina ya sanamu ambacho hapo awali kilimiliki, na yeye mwenyewe kuchukua mamlaka. Haya ni mabadiliko makubwa ya utii ambayo husababisha kubadilika na au kuokoka, au angalao mwanzo wake. Kisha mara moja Kristo amechukua nafasi yake sahihi, kila kitu kinaanza kuhama."
> - Lausanne Committee
> for World Evangelization,
> *The Willowbank Report*

Unatakiwa ujionee mwenyewe msamaha wake na uanze uhusiano na yeye. Unaanza kwa kumjua zaidi na utake kufanana yeye.

► Soma Mathayo 16:21-25.

---

[173] Mathayo 28:20
[174] Mathayo 4:19, Mathayo 9:9, Mathayo 16:24, Mathayo 19:21, Yohana 1:43

Katika mazungumzo haya na wanafunzi wake, Yesu alielezea kuhusu ujio wa kifo chake. Petro alishtushwa na maneno ya Yesu. Petro hakuona kama kuteseka na kufa ni sahihi kabisa kwa Yesu. Alianza kubishana na Yesu, akijaribu kumtia moyo kukataa wazo la kifo.

Yesu alimkemea Petro na kumwambia kwamba hakuwa anaelewa mambo ya Mungu. Yesu alimwambia kwamba mtu yeyote akitaka kuwa mwanafunzi wake, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, na amfuate. Hii ilimaanisha kukubali kifo kwa nafsi. Kukemewa huku kulikuwa kinyume na tabia za asili za mwanadamu za ubinafsi, kujitosheleza mwenyewe, na kujitetea mwenyewe—mambo ambayo huzuia ufuasi wa kweli.

► Je, kwa nini nafsi ya binadamu hukinzana na ufuasi?

Wanafunzi hawakuona mateso na kifo kama kilikuwa ni stahili yao. Walikuwa bado hawajaelewa kwa ukamilifu ilimaanisha nini kumfuata yeye. Haikugharimu chochote wewe kusamehewa, lakini itakugharimu kila kitu ili kumfuata Kristo. Kumfuata yeye kunasababisha moyo kuendelea kutafuta, kuwa mnyenyekevu, na mabadiliko.

► Fafanua kauli hii, "Itakugharimu kila kitu ili kumfuata Kristo."

Kuuchukua msalaba ni kukubaliana na aina ya kifo kwa ajili ya maisha ya milele pamoja na Mungu. Ni kifo cha nafsi, kifo cha uhuru wako mwenyewe. Siyo tu kukubali kwa nje, lakini inakwenda moja kwa moja hadi kwenye moyo. Ni unyenyekevu ambao Yesu ameelezea kama hitaji la kuingia kwenye ufalme wake.

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa mwanzo, walio wengi leo hawaelewi inamaanisha nini kuwa mwanafunzi. Makanisa yanatangaza neema kwa wale watu ambao hawajatubu. Hali hiyo haiwezi kuleta watu waokoke kwenye barabara iliyo sahihi au kuwaandaa kwa kile kinachokuja. Ni tofauti sana kulinganisha na hali halisi ya kuishi ya Kikristo kwamba siyo barabara inayofanana.

Dietrich Bonhoeffer alikuwa mchungaji wa Kijerumani ambaye aliuawa na Adolph Hitler. Aliandika mistari hii kwenye kitabu chake kiitwacho *The Cost of Discipleship*. *(Gharama ya ufuasi).*

> Neema yenye gharama ni hazina iliyofichika katika shamba; kwa ajili yake mwanadamu atakwenda na kuuza vyote alivyo navyo kwa furaha. Ni lulu ya thamani sana kununua ambayo mfanyabiashara atauza mali zake zote. Ni sheria ya upendo ya Kristo, ambayo kwa ajili yake mwanadamu ataling'oa jicho lake linalomsababisha kuyumba; ni wito wa Yesu Kristo ambao mwanafunzi huachana na nyavu zake na kumfuata yeye…imani ya aina hiyo ni ya gharama sana kwa sababu inatutaka tufuate.

Kumfuata yeye ni kufanana naye. Ni kufa kwa nafsi kwa sababu yeye mwenyewe aliisalimisha kabisa nafsi yake. Siyo tu jambo la kuacha kufanya mambo fulani mabaya, bali kuachana nayo kwa sababu Yesu pia angeacha. Tunajaribu kufanya yale ambayo Yesu angeweza kufanya katika usafi wake, huruma, wema na msamaha.

Hatufanyi tu kile ambacho ni sahihi wakati mioyo yetu inapingana nacho. Tunataka mioyo yetu ifanane na moyo wake. Hakuwahi kumchukia mtu yeyote. Wako baadhi ya watu waliochagua kuwa maadui zake, lakini yeye hakuwa adui wa mtu yeyote. Hata pale alipokuwa juu ya msalaba alisamehe.

Wafuasi wake wa kweli siyo watu wa chuki au wenye inda. Wanafanya yaliyo mema kwa wale wanaowatendea mabaya. Wanabariki badala ya kulaani. Hawana kiwango cha kusamehe kwao. Wameamua kuachana na haki zao za binafsi na badala yake kutumika.

Hakuna mahali pa kwenda ukiacha jambo hili la kujisalimisha binafsi. Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza—naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona.

► Je, tunawezaje kuwaita watu waokoke katika njia ambayo itawaandaa kwa ajili ya ufuasi?

## Malezi ya Kiroho

Kuna mchakato wa malezi ya kiroho[175] ambayo humfanya mtu aliyeamini kufika kwenye kiwango cha kukua kiroho.

Mtu aliyeamini anapaswa aendelee kukua katika maisha yake yote, lakini kuna kiwango cha kukua anachoweza kufikia kinachoweza kuitwa kiwango cha kiroho cha mtu mzima. Mtume Paulo alisema kwamba watu walioamini wanaweza kufika kwenye kiwango ambacho hawatakuwa tena watoto wachanga.[176]

Malezi ya kiroho kwa sehemu hupatikana kutokana na kujifunza. Hii ndiyo maana mtume Paulo alisema kwamba tabia ya uchanga iliwafanya wasiweze kuwa tayari kwa ajili ya mafundisho ya juu ya imani.[177] Alisema kwamba tabia ya ukomavu ni kwa ajili ya watu walioamini kujengwa katika mafundisho ya imani. Kwa kuwa kujifunza ni sehemu ya malezi ya kiroho, kufundisha ni kazi mojawapo ya huduma ya ufuasi.

Malezi ya kiroho hayakamilishwi tu kwa kujifunza.

Mtume alisema kwamba kukua kiroho ni kuwa katika umoja wa Kikristo, kuwa na maarifa kuhusiana na Mwana wa Mungu, na kufanana na Kristo .[178] Ukuaji huu ni zaidi ya maarifa na haupatikani kutokana na maarifa pekee.

► Soma 2 Petro 1:2-11.

Kifungu hiki ni mahususi kwa ajili ya maendeleo ya kiroho. Tambua mambo muhimu ya kifungu hiki.

---

[175] "Malezi ya kiroho ni mchakato wa neema ya kufananishwa kuwa kwenye sura ya Yesu Kristo kwa ajili ya watu wengine." Ufafanuzi huu umechkuliwa kutoka kwa M. Robert Mulholland Jr., *Invitation to a Journey* (Downers Grove: InterVarsity Press), 12.
[176] Waefeso 4:14
[177] 1 Wakorintho 3:1-2. Ona pia Waebrania 5:12-14.
[178] Waefeso 4:13

**Aya ya 3**: Mungu ametukirimia kila kitu muhimu kwa ajili yetu tuwe katika uweza wa kiungu na ametuita kwenye maadili ya Kikristo.

**Aya ya 4**: Mungu ametukirimia ahadi ya neema ya mabadiliko inayotuokoa na dhambi na kutupa sisi asili takatifu ya Mungu.

**Aya ya 5-7**: Hatupaswi kusimama na imani yenye kuokoa tu, bali tusonge mbele katika kukuza sifa za Mkristo.

**Aya ya 8**: Sifa hizi zitatufanya sisi tuwe na tunda la roho.

**Aya ya 9**: Mtu ambaye haendelezi sifa hizi haendelei katika ukombozi wa dhambi zake, na haoni kule anakokwenda.

**Aya ya 10-11**: Usipumzike kwenye uhakika wa wokovu bila ya kuwa umefanyia kazi kukuza sifa za Mkristo. Zitakujenga wewe katika wokovu wako na zitakuleta kwa ushindi mkubwa kwenye ufalme wa milele wa Mungu.

Sura ya pili ya waraka huu unazungumzia kuhusu watu waliokataa maendeleo ya koroho. Wanataka tu wawe na jina la Kikristo. Kwa kuwa wanakataa kuendelea katika kiwango cha juu cha kiroho, wanahalalisha dhambi. Wanatengeneza mafundisho ya uongo ya imani ili kuhalalisha na au kuunga mkono tabia zao. Mafundisho yao ya uongo yanasababisha waumini wapya waliookoka kuanguka tena kwenye nguvu ya dhambi na kurejea kuwa katika hali mbaya zaidi kana kwamba kamwe hawajawahi kukutana kabisa na neema inayookoa.[179]

Waraka unamalizia kwa kutoa onyo na au angalizo. Ni lazima tuepuke kurejea kwenye dhambi kutokana na mafundisho potofu ya imani, na badala yake, kujielekeza kwenye kukua katika neema.[180]

Yesu alisema katika Agizo Kuu kwamba kazi ya huduma ya ufuasi nikuwaleta watu kwenye utiifu kwake. Bila shaka, mtu anayejifunza ni lazima awe na utii wa kweli kwa yale anayojifunza; vinginevyo, atakuwa haendelei. Kusudi la maarifa ni kumwonyesha jinsi ya kumpendeza Mungu na kuongoza maendeleo ya tabia yake. Kama mtu ataendelea kujifunza lakini haendelei kuwa mtiifu, huyo siyo mfuasi. Kuna watu wengi ndani ya makanisa ambao wana maarifa mengi ya kidini, lakini hawawezi kudhihirisha maisha ya mwamini mkomavu.

► Soma Wafilipi 1:9-11.

Kanisa la Wafilipi lilikuwa ni kundi zuri la waamini, na barua ya Paulo kwa ajili yao ilikuwa na udhihirisho wa furaha.

---

[179] 2 Petro 2:18-22
[180] 2 Petro 3:17-18

Ndani ya aya hizi, Paulo anaelezea kukua kiroho kwa Wafilipi. Maelezo hayo ni muhimu kwa sababu yanaunganisha maarifa, ufahamu, upendo na tabia.

Paulo aliomba kwamba upendo wao uzidi kuongezeka, na kwamba upendo huo utadhihirishwa ndani ya ufahamu wao wa mema, ili kwamba waweze kuchagua mitazamo na mienendo ambayo ni mizuri zaidi. Maisha haya hayatakuwa ya kulaumika mbele za Mungu wakati Yesu atakaporudi. Maisha yao yatakuwa na wingi wa tunda la roho ambalo litampa Mungu utukufu.

► Kutokana na haya ambayo tumeshajifunza, mfuasi wa Yesu ni nani?

Mfuasi wa Yesu ni mtu aliyeamini anayeishi kwenye utiifu katika yale aliyojifunza, akitamani kwa bidii kuelewa zaidi mapenzi ya Mungu, na akitegemea nguvu za Mungu katika kukuza tabia na mwenendo wa Mkristo.

► Sasa kwa kuwa tunafahamu kuhusu malezi ya kiroho, Je, utamwelezeaje mtu ambaye anafanya ufuasi kwa watu wengine?

Anafundisha ukweli wa Biblia. Yeye ni mfano wa kuigwa wa utiifu wake kwa Yesu. Anawatia moyo watu wengine kujifunza, kutii, na kuruhusu kazi ya Mungu itendeke ndani yao.

## Uwezo wa Neema

Katika sehemu ya awali iliyopita tulijifunza 2 Petro 1:2-11. Katika kifungu hicho, tulijifunza kwamba Mungu alikuwa ameahidi neema ambayo inatukomboa sisi kutokana na nguvu na matamanio ya dhambi na inatupa sisi asili ya utakatifu. Maarifa hayo yanaongoza ukuaji wetu wa kiroho.

Baadhi ya watu wanaamini kwamba haiwezekani kwa mtu kuishi bila kutomtii Mungu. Wanaamini kwamba haiwezekani kwa mtu kuwa na moyo wa utakatifu. Mawazo haya huathiri uelewa au ufahamu wao kuhusiana na ufuasi.

Ufuasi unamaanisha kuwa unajfunza na kutii maagizo ya Kristo. Kama hatuwezi kuamini kwamba utii kamili ni jambo linalowezekana, ni kusema kwamba tunataka kutafuta njia nyingine ya kufanya tathmini ya hali ya kiroho.

John Wesley aliamini kwamba hakuna mtu mwenye uwezo wa kutekeleza amri za Mungu bila neema ya kumwezesha, lakini aliamini kwamba neema inayowezesha imetolewa kwa kila mtu. Wesley aliamini kwamba kila mwenye dhambi ana uwezo, siyo kwa asili bali kwa neema inayowezesha, kuweza kukubaliana na wito wa injili. Aliamini pia kwamba kila Mkristo amepewa neema ya kuishi kwa utiifu wote mbele za Mungu.

Kutoka katika theolojia ya Wesley kunajitokeza kanuni ya "kutafsiri Maandiko" (hermeneutics) ambayo inaweza kuitwa "Kanuni ya Ahadi." Wafuasi wa Wesley wanaamini kwamba chochote ambacho Mungu anaamuru, atawawezesha na watu wake kutekeleza.

Hii inamaanisha kwamba kila amri katika Maandiko inaweza kutazamwa kama ni ahadi ya neema.

## Kanuni ya Ahadi

Sura zifuatazo ni ufafanuzi wa Wesley kuhusiana na kanuni hii.[181]

> Pingamizi moja la kawaida ni kwamba hakuna ahadi ya namna hiyo [Ukamilifu wa kikristo] katika Neno la Mungu. Lakini kuna ahadi iliyo wazi kwamba tutampenda Bwana Mungu wetu kwa mioyo yetu yote. Tunasoma, "Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote."[182] Linalokaribia kuwa sawa na hilo ni neno la Bwana wetu, **ambalo bila kupunguka ni ahadi, ingawaje liko katika namna ya amri:** "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote."[183] Hakuna maneno yanayoweza kuwa na nguvu kuliko haya; hakuna ahadi inayoweza kuwa wazi zaidi ya hapa. Vivyo hivyo, "Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe" ni ahadi iliyo wazi kama ilivyo ambapo pia ni amri.
>
> Na ahadi hiyo ambayo haina kikomo katika umri wote wa injili, "Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, Na katika nia zao nitaziandika," **inageuza amri zote kuwa ahadi;** ukiweka pamoja na hii, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu." **Hii amri inakaribia kuwa sawa na ahadi, na inatupa sisi sababu za kutegemea kwamba atafanya kazi ndani yetu kwa kile anachotaka kutoka kwetu.**
>
> **Amri ya Mungu iliyotolewa na Mtakatifu Petro, "kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote," inaonyesha ahadi kwamba tutakuwa watakatifu**, ikiwa tuko tayari. Hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kukosekana kwa upande wa Mungu. Kama alivyotuita kwenye utakatifu, bila shaka yeyote yuko tayari, na ana uwezo, kuufanyia kazi utakatifu huu ndani yetu. **Kwa kuwa hawezi kuwafanyia mzaha viumbe wake wasiokuwa na uwezo, akituita kupokea kitu ambacho hajakikusadia kukitoa**. Hali ya kwamba ametuita sisi kwenye utakatifu hilo halipingiki; kwa hiyo, atatupa utakatifu kama hatutakosa kumtii kwa wito wake wa mbinguni.
>
> "Lakini, je, ametuahidi kutuokoa sisi kutoka katika dhambi wakati tukiwa katika hali ya kimwili?" Bila shaka ndivyo. Kwa kuwa **ahadi inahusika katika kila amri ya**

[181] John Wesley, "Christian Perfection," kutoka *A Timeless Faith: John Wesley for the 21st Century*. Imehaririwa na Stephen Gibson. (Nappanee: Evangel, 2006).
[182] Kumbukumbu la Torati 30:6
[183] Mathayo 22:37

**Mungu,** ikiwa ni pamoja na "Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote."

Inatupasa tuwe na matarajio ya neema ya Mungu inayohusiana na mtazamo wetu juu ya tabia ya Mungu. Tunategemea kwamba chochote Mungu atakachotuamuru atatuwezesha, kwa kuwa amri zake ni za uaminifu na kweli na zinaweza kutekelezwa pasipo njia nyingine yeyote.

Tunaweza tukayazingatia Maandiko yote kwa kumaanisha. Kamwe hatupaswi tuharibu maana halisi ya kauli za Biblia. Kanuni ya Ahadi ni ya heshima kwa Mungu, kwa kuwa inakuwa na mategemeo kwamba Mungu anazo nguvu na utayari wa kufanyia kazi ndani ya mwamini utakatifu ambao Mungu amemwitia. Maonyo, ahadi, na maombi ya kimaandiko havipaswi kupuuzwa. Theolojia nzuri huthibitika vizuri kwa jinsi inavyotumia Maandiko.

## Je, Kuishi Maisha Matakatifu Inawezekana?

> "Kama ufanisi wake ni sawa na haki yake, ahadi zake za neema ni lazima zieleweke kumaanisha ni zaidi ya mahitaji yake ya haki. Kama atapendelea kutoa kwa kiwango kile cha kupokea, ahadi zake ni lazima zimaanishe ni zaidi sana kama ilivyo lugha yake ya mahitaji."
> - Charles Finney,
> *Systematic Theology*

Ni kwa nini Mungu Mwenyezi asiitakase nafsi wakati bado ikiwa kwenye mwili? Kwani hawezi kukutakasa wewe wakati ukiwa katika nyumba hii, au ukiwa nje kwenye sehemu za wazi? Je, kuta za matofali au mawe zina uwezo wa kumzuia? Hata hizi kuta za nyama na damu hazina uwezo wakati wowote wa kumzuia asikutakase kabisa. Anaweza kirahisi sana kukuokoa kutoka katika dhambi zako zote ndani ya mwili wako na hata nje ya mwili. "Lakini hajatuahidi kwamba atatuokoa sisi na dhambi zetu wakati tukiwa katika hali ya kimwili?" Bila shaka alishafanya. Kwa kuwa **ahadi inahusika katika kila amri ya Mungu,** ikiwa ni pamoja na "Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote." Kwa ajili ya hii na amri nyingine yeyote iliyotolewa, siyo kwa ajili wafu, bali ni kwa ajili ya walio hai. Imelekezwa kwenye maneno yaliyonukuliwa hapa juu, kwamba tunapaswa tutembee "katika utakatifu mbele zake katika siku zote za maisha yetu."[184]

Watu wengi wanatoa ushuhuda kwamba wao ni Wakristo wa miaka mingi lakini kamwe hawajawahi kupata ushindi dhidi ya majaribu. Wanakua katika maarifa na ujuzi wa huduma lakini siyo katika mambo ya msingi na muhimu.

Biblia inafundisha kwa uwazi kabisa kwamba kiwango cha Mungu kwa mtu aliyeamini ni kwamba awe na ushindi dhidi ya dhambi na moyo wa utakatifu.[185] Kama mtu aliyeamini

---

[184] Ibid.
[185] Tito 2:11-12; Matendo 15:9; 1 Yohana 3:2-10, 1 Yohana 5:1-4

akitambua kwamba hayuko kama Mungu anavyotaka awe, atapaswa atafute mara moja kubadilishwa kwa kumaanisha na kwa kuwezeshwa na Roho wa Mungu.

Mtu aliyeko katika huduma ya ufuasi anapaswa aweke kipaumbele chake wazi. Ushindi dhidi ya dhambi ni jambo la kipaumbele cha kwanza. Kama mtu anaanguka katika dhambi, mhudumu wa ufuasi ni lazima amwongoze kwenye kutubu na ushindi kabla ya kuweza kufanya au kukamilisha jambo lingine lolote.

**Kazi ya Kufanya**

Andika aya chache kuhusiana na kila swali lililoko hapa:

- Mtu atarajie nini kama anataka kuwa mfuasi wa Yesu?
- Unawezaje kufafanua ukweli wa msingi ambao Petro alizungumzia kuhusu kukua kiroho?
- "Kanuni ya Ahadi" ni nini?

Urefu wa andiko lako angalau usipungue kurasa mbili.

# Somo la 17
# Kuelekea Kukua Kiroho

## Huduma ya Kufundisha ya Kanisa

Wakati wa kipindi cha mtu kuokoka mabadiliko mengi hutokea. Mtu aliyebadilika na au kuokoka anakuwa na matamanio mapya na vipaumbele vipya—mabadiliko hayo ni makubwa sana kiasi kwamba Biblia inamwelezea huyu mtu kama "uzao mpya."[186]

Lakini baadhi ya mambo huchukua muda kutokea. Mtu aliyebadilika na au kuokoka hawezi kuona kwa mara moja jinsi ya kutumia kanuni za Kikristo katika maeneo yote ya maisha yake. Atapaswa ajifunze hizo kanuni, na kisha aangalie jinsi ya kuzitumia.

Kunakuwepo pia na mchakato binafsi wa kukua kiroho. Mtu aliyebadilika na au kuokoka anakuwa ni "mtoto mchanga ndani ya Kristo."

► Soma 1 Wakorintho 3:1-2. Je, kwa mujibu wa aya hizi, mtu aliyeokoka anafanana sana na nini?

► Soma Waebrania 5:13-14. Je, maziwa yanayozungumziwa katika aya hizi ni ya namna gani? Je, chakula kigumu ni nini? Je, tabia ya mtu anayekua kiroho ikoje?

Mapema kwenye kozi hii, tuliangalia kuhusu Agizo Kuu la Yesu ambalo alilitoa kwa kanisa. Tulipitie tena kwa mara nyingine.

► Soma Mathayo 28:18-20. Kwenye aya hii, je, ni jukumu gani Yesu alilolitoa zaidi ya uinjilisti?

Kabla ya kutoa Agizo Kuu, Yesu alitamka kwamba amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kisha akalipa kanisa jukumu la kuwaleta watu watakaokuwa watiifu kwenye mamlaka yake.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa wasihubiri tu injili, bali wafundishe pia na mambo yote ambayo alikuwa amewaamuru. Uinjilisti ni sehemu moja tu katika haya majukumu. Kuwafundisha watu waliookoka kutii maagizo yote ya Yesu ni mchakato wa ufuasi. Ubaya wa kushindwa kufanya ufuasi ni sawa na ule ule kama wa kushindwa kufanya uinjilisti.

Huduma ya ufundishaji ya kanisa ni kwa ajili ya kuwaleta waliookoka kwenye kukua kiroho.

Kwenye Waefeso tunaelezwa kwamba Mungu huwaita watu kwa ajili ya makusudi maalumu ya huduma kwa lengo la kuwajengea uwezo watu waliokoka ili wasiendelee

[186] 2 Wakorintho 5:17

kuwa watoto wachanga.[187] Matokeo ya kufikia ukomavu wa kiroho wa utu uzima unatokana na uthabiti wa mafundisho ya imani.

Mchungaji ndiye mhusika mkuu wa huduma ya ufuasi. Paulo alimwambia Timotheo, "ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha."[188] Kimsingi hakuwa anarejelea kwa Timotheo kujifunza binafsi; alikuwa anazungumzia kuhusu huduma. Huduma ya Timotheo ilikuwa ni kuelekeza kwenye kusoma na kufafanua maandiko, kutoa mwelekeo wa kiroho, na kufundisha mafundisho ya imani ya Kikristo. Sifa mojawapo ya mchungaji ni kuwa na uwezo wa kufundisha.[189]

Kwa kuwa kujifunza ni sehemu mjawapo ya mageuzo ya kiroho, kufundisha ni sehemu ya huduma ya ufuasi. Waalimu ni muhimu sana katika kanisa, na kanisa ni lazima liwe na wajibu wa kuwaendeleza waalimu.

"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."[190] Maelekezo haya yalitolewa na Paulo kwa Timotheo, kutokea kwa mwinjilisti na mchungaji mzoefu kwenda kwa mtoa huduma mchanga. Paulo alikuwa na wasi wasi kama imani inaweza kuwa ya kuachizana kwa mahubiri peke yake. Watu binafsi watahitajika wapewe mafunzo kwa jitihada maalumu na wawe tayari kwa ajili ya kusaidia watu wengine. Kama mafunzo hayo hayataweza kukamilishwa kwa kuhubiriwa kwenye kusanyiko la washirika, "watu hawa waaminifu" watapaswa wahudumiwe kibinafsi au kwenye vikundi vidogo.

> "Lengo la awali la mpango wa Yesu lilikuwa ni kuwa na orodha ya watu ambao wangekuwa mashahidi wa maisha yake na ambao wangeubeba mzigo wa kazi yake baaada ya kuwa amerejea mbinguni kwa Baba."
> - Robert Coleman, *The Master's Plan*

Kuna mafundisho mengi yanayotakiwa kufundishwa. Je, mchungaji anao muda wa kuyafanya haya yote, hasa ikizingatiwa kwamba siyo kila mtu aliye na utayari wa kupokea maagizo yanayofanana kwa wakati mmoja? Lakini katika Waefeso 4:11 haijasemwa, "alimpa mchungaji" (mtu mmoja tu na jukumu moja tu). Badala yake, kuna majukumu mengi na watu kadhaa kwa ajili ya kuyafanya. Mungu anawaita waalimu, anawapa uwezo wa kufundisha, na anawawezesha kupitia katika kanisa kwa ajili ya huduma ya kufundisha.

## Jumuiya ya Kikristo na Uwajibikaji wa Kiroho

Kufanya huduma ya ufuasi wa kweli ni zaidi ya huduma ya kufundisha habari; inahusisha pamoja na kuboresha maadili, vipaumbele, mienendo na mtindo wa maisha. Mchakato huu unaweza kutokea peke yake kwenye jamii ya Kikristo yenye uwajibikaji wa kiroho.

[187] Waefeso 4:11-14
[188] 1 Timotheo 4:13
[189] 1 Timotheo 3:2
[190] 2 Timotheo 2:2

Tunaona kupitia Maandiko kwamba Mungu alikusudia watu wake waishi kwenye jumuiya, ukianzia na kauli ya Mungu kwa Adamu kwamba hutakuwa peke yako." [191]

Faida nyingi za jumuiya zimeelezwa katika Mhubiri 4:9-10:

> Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua.

Mungu alimwambia Musa kwamba mpango wake kwa ajili ya Israeli ni kuwa wawe ufalme wa makuhani, na taifa takatifu.[192] Urithi ulikuwa uende hadi chini kupitia familia, kunakoelezwa katika kile kinachoitwa "Amri Kuu."[193]

Roho Mtakatifu aliwavuvia waandishi wa Agano Jipya kutumia maneno hayo katika Agano Jipya ili kurejea kwenye kanisa.[194]

Mungu siku zote alikusudia kwa ajili ya watu wake walio katika uhusiano na yeye wawe pia kwenye uhusiano wa wenyewe kwa wenyewe. Uhusiano wetu na Mungu unatufanya tuwe kwenye jumuiya ya imani. Kama vile ambavyo uhusiano wetu na Mungu unatutaka uwe wa kujikabidhi kabisa, uhusiano wetu na watu wengine wa Mungu unatutaka pia tujikabidhi kabisa. Ni makosa kwa mtu kufikiria kwamba anaweza kuwa kwenye uhusiano sahihi na Mungu lakini akachagua kutokuwa kwenye uhusiano na watu wengine wa Mungu.

Paulo alitumia mfano wa mwili kwa kuelezea uhusiano kati ya washirika wa kanisa.[195] Hakuna mshirika anayeweza kutenda vizuri kama atakuwa anajaribu kujiweka mbali na ushirika huo. Washirika ni lazima washikamane kwa pamoja na kila mmoja kumjali mwenzake, au kutakuwa hakuna mtu kabisa. Endapo mshirika mmoja atajeruhika, washirika wengine wote wanateseka. Matendo ya mshirika mmoja yanagusa washirika wote. Paulo alizungumzia kuhusu hili alipokuwa akishughulika na hali ya mtu aliyekuwa katika uhusiano mbovu, ingawaje badala yake alitumia mfano wa mkate. Alisema, "Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima?"[196] Ni lazima tujione sisi wenyewe kwamba ni viungo kwa ajili ya jumuiya ya Kikristo.

Maagizo mengi ya Agano Jipya huwezi hayatekelezeki bila kujali jumuiya. Katika kutimiza amri za Mungu, Wakristo ni lazima tuishi kwa kujitoa kabisa sisi kwa sisi. Hii inamaanisha kwamba jumuiya ya Kikristo inasababisha uwajibikaji wa kiroho.

---

191 Mwanzo 2:18
192 Kutoka 19:6
193 Mathayo 22:36, Kumbukumbu la Torati 6:4-9
194 1 Petro 2:9
195 1 Wakorintho 12
196 1 Wakorintho 5:6

Tunaona katika Biblia maeneo mengi ambayo jumuiya ya Kikristo imeunganishwa katika uwajibikaji wa kiroho.

> Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi.[197]

Aya hii inawaambia watu walioamini na kuokoka kuwatii wale walioko kwenye nafasi za mamlaka ya kiroho. Amri hii pia inawapa majukumu makubwa viongozi wa kiroho. Jukumu lao siyo tu kuongoza kwa mamlaka, lakini kuziangalia roho zilizo chini ya mamlaka yao. Ili kufanya hayo, ni lazima wawe wamezoea na kuwafahamu watu wao kabisa kwa ajili ya kuwapa mwelekeo wa kiroho, na ni lazima wawe na uhusiano na watu wao ambako kutawezesha mwelekeo huo uwezekane.

Jumuiya ya Kikristo na uwajibikaji wa kiroho vinaelezwa pia katika kifungu hiki:

► Soma Waebrania 10:24-26. Je, ni kitu gani kilichoamriwa katika aya hii?

Hapa tunaamriwa tuwe macho na mahitaji ya Wakristo wengine na kuwatia moyo katika kutenda mambo yaliyo sahihi.

► Eleze uhusiano utakaokuwa muhimu miongoni mwa waamini kwa ajili yao kutekeleza jukumu hili.

Utiaji moyo wetu hautakuwa na ufanisi kama tutakuwa hatuna uhusiano mzuri na watu wengine. Tunapaswa tuwajue vizuri na tuonyeshe upendo na nia ya kuhusika nao. Vinginevyo, wanakwazwa kwa ushauri wa binafsi.

> Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo "leo;" ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi.[198]

Tumeitwa kuhakikisha kila mmoja anawajibika. Kushawishiana hapa ni lazima kuwe juu ya ratiba za vikao vya kanisa zima, kwani tumeamriwa kushawishi "kila siku." Hali hii inahitaji ushirika wa watu binafsi au mfumo wa vikundi vidogo. Ushirika wa aina hii hautahitaji tu kula pamoja au kutembeleana, ila utakuwa na kusudi la kiroho. Ili kutimiza kusudi hili, na kwa umuhimu huo, ni lazima kwa makusudi mazima kabisa tupange mazungumzo ya pamoja na vikao kwa ajili ya vikundi vidogo.

Njia ambayo kila mmoja anaweza kufadika na mwenzake imeelezwa katika Mithali 27:17:

> Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake.

---

[197] Waebrania 13:17

[198] Waebrania 3:12-13

Mtu hapaswi kuwa mkuu kwa mwingine kabla hajampa faida ya mwelekeo wa kiroho na kumwimarisha pamoja na kumtia moyo. Kwa kweli, mwelekeo wa kiroho unaotolewa kwa unyenyekevu una uwezekano mkubwa wa kukubalika.

> Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.[199]

Kuungama kwa makosa ya binafsi kwa kawaida hakutatokea kwenye makundi makubwa; kwa hiyo, amri hii haipokelewi kirahisi kwenye ibada za makanisa. Muktadha unaonesha sababu ya amri hiyo: kwamba watu wote ambao wamefanya makosa wanaweza wakarejeshwa tena.

> Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.[200]

Mara nyingi Mkristo hujihisi kwamba hakuna mtu anayejali katika yale anayopitia. Wakristo wenzake watajali kama watajua kwa uhakika kwamba amepatwa na mateso gani, lakini kwa kawaida hawamjui vizuri. Je, ni kwa jinsi gani tunaweza kubeba mizigo ya watu wengine ambao kwa kweli hatuwajui wao ni nani?

Kwenye siku za mwanzo za kuzaliwa kwa kanisa, ushirika wa karibu sana miongoni mwa watu waliokuwa wameamini ulikuwa ni jambo la kawaida.

> Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe.[201]

John Wesley alisema kwamba hakuna kitu cha kuitwa Ukristo wa binafsi.

► Je, unadhani Wesley alikuwa anamaanisha nini kwenye tamko lake hilo?

Uwajibikaji wa kiroho unatokea kwenye jumuiya iliyo na afya ya Kikrito.

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni kuanzisha uhusiano na mtu binafsi na au kikundi ambacho tutawajibika kwao kwa taarifa zetu za hali za kiroho, mafanikio yetu au kushindwa kwetu katika nidhamu za kiroho, na ahadi zetu kwa ajili ya maendeleo.

Bila ya uwepo wa uwajibikaji wa kiroho hatutaweza kutimiza amri zote Maandiko, na tutapuuzia maana ambayo Mungu ameikusudia kwa ajili ya kutupa sisi neema.

## Tabia za Kukomaa Kiroho

Je, inamaanisha nini kukomaa kiroho? Je, utamwelezeaje Mkristo aliyekomaa kiroho?

---

[199] Yakobo 5:16
[200] Wagalatia 6:2
[201] Matendo 2:46

Kwa kuwa kukomaa kiroho kunachukua muda, huelekea kuendana pamoja na umri.[202] Bila shaka watu huzeeka bila ya kukomaa kiroho kama ambavyo wangetakiwa wawe, na kuna vijana wadogo ambao wanadhihirisha ukomaaji usio wa kawaida.

Tabia nyingi za kukomaa kiroho hazipatikani zote kwa wakati fulani, lakini kunaongezeka hatua kwa hatua. Wakati mwingine kukomaa kiroho kunaweza kuongezeka kwa haraka kwa sababu ya uzoefu wa kiroho na au uzoefu wa maisha. Ingawaje mtu anatakiwa aendelee kukua kiroho katika maisha yake yote, kuna kiwango anachoweza kufikia ambacho kinaweza kikaitwa kukomaa kiroho.

Tabia za kukomaa kiroho zimeelezwa kwenye aya kadhaa za Maandiko.

► Wanafunzi kadhaa watapaswa kusoma aya hizi kwa ajili ya kikundi: Waefeso 4:11-14, Waebrania 5:12-6:1, 1 Wakorintho 3:1-2, and 1 Yohana 2:12-14.

Hapa chini pameorodheshwa tabia ambazo ni ishara au alama za kukomaa kiroho. Siyo orodha yote iliyoonyeshwa, na baadhi ya mambo katika orodha hii hayajatofautiana sana na mambo mengine.

Mkristo aliyekomaa kiroho hawezi akazielezea tabia hizi zote kwa ujumla, lakini bado anaendelea kukua. Anaweza asitambue baadhi ya makosa yake, lakini ataendelea kuitikia wito wa kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya moyo wake.

## Tabia Kumi za Kukomaa Kiroho

### (1) Kufanana Kristo katika nia, mtazamo na matendo

Kumfanania Kristo huja kutokana na shauku ya kumjua Kristo katika asili yake, kwa kupata uzoefu wa kiroho wa kifo chake na kufufuka kwake.[203] Inaweza kuwa ni pamoja na kushiriki mateso yake. Mtu anayempenda Kristo kwa kiwango hiki atabadilishwa afanane kama yeye.

Kumfanania Kristo ni kuhamasishwa kwa njia ya upendo na siyo kwa ubinafsi au kiburi. Mkrito anataka amfananie Kristo na inasikitisha wakati wowote anapojitambua kwamba hakuwa kama Kristo katika chochote alichokisema au alichokifanya.

### (2) Uhusiano mzuri na Mungu

Mtu anatakiwa akue akae kwenye uhusiano wa karibu na Mungu. Ishara au alama za uhusiano mzuri na Mungu ni pamoja na kufurahia uwepo wa Mungu, kulipenda Neno la Mungu, na wakati unaotumika katika maombi.

[202] Tito 2:1-5
[203] Wafilipi 3:10

**(3) Udhihirisho wa matunda ya Roho**

Roho Mtakatifu hutengeneza tunda katika maisha ya mwamini, ambayo ni pamoja na upendo, furaha, uvumilivu, na kiasi. Mwamini anakuwa thabiti zaidi katika wema na upole kama anavyomruhusu Roho Mtakatifu kufanya kazi katika silika yake.

**(4) Ushindi dhidi ya dhambi ya nje na ndani**

Mwamini hujifunza jinsi ya kumtegemea Mungu kwa ajili ya ushindi dhidi ya majaribu. Hujitoa kwa Bwana kwa ajili ya kutakaswa ili aweze kuwa na moyo ulio safi. Hukuza tabia na nidhamu ambavyo humsaidia yeye kuishi kwa uthabiti katika ushindi.

Akijikuta ameangukia kwenye jaribu, hukiri dhambi yake kwa Mungu na kuomba kwa ajili ya msamaha na kutiwa nguvu. Inampasa ashirikishe madhaifu yake kwa marafiki wake wa karibu wa Kikristo ambao wataomba kwa ajili yake.[204]

**(5) Nidhamu za kiroho huimarika**

Nidhamu za kiroho ni njia za kufanyia majaribio ya kufanya uhusiano wetu na Mungu uwe kipaumbele cha kwanza. Mtu ambaye hafanyi maombi, kusoma Biblia, na kuhudhuria ibada za kanisa kwa uendelevu siyo Mkristo aliyekomaa kiroho.

**(6) Tabia ya Kikristo iliyokuzwa**

Mkristo hujifunza jinsi ya kupangilia maisha yake kwenye kanuni za unyofu, uwajibikaji na kazi za uaminifu.

**(7) Kuishi maisha ya Kikristo kwa uendelevu**

Mwamini hujifunza kutumia kanuni za Kikristo katika maisha yake. Mkristo aliyekomaa Kikristo atapenda aonekane kama Mkristo kwa nyakati zote katika mwenendo na tabia zake. Anapojitambua kwamba kitu anachokisema au anachokifanya hakina uthabiti wa upendo ndani ya moyo wake, hutegemea nguvu za Mungu zimsaidie kufanya mabadiliko.

**(8) Mahusiano yenye afya.**

Mkristo aliyekomaa hukuza uhusiano wa ndani kabisa na Wakristo wengine. Hudumisha mahusiano kwa kuonyesha wema, uvumilivu, na msamaha. Ni mnyenyekevu na ni mwepesi kukiri afanyapo makosa. Kwa kuwa inawezekana kuelewa jambo vibaya, anaweza asiwe mvumilivu kama anavyopaswa awe, anaweza asikubaliane na kosa kwa haraka na anaweza asiwe na kauli sahihi kuhusiana na mtu mwingine.

**(9) Huduma binafsi**

Mwamini anapaswa atambue vipawa vyake vya kiroho alivyo navyo. Atapaswa atafute nafasi yake katika kanisa ili afanyike baraka kwa watu wengine. Mwamini anaweza

[204] Yakobo 5:16

akahudumu katika kanisa kwa kusaidia kufanya uinjilisti na kufanya huduma ya ufuasi katika maisha ya Kikristo.

**(10) Ustahimilivu katika nyakati ngumu**

Mwamini anapaswa ajifunze jinsi ya kumtii Mungu wakati mambo magumu yanapotokea. Anapaswa amtegemee Mungu anapokuwa kwenye mazingira magumu katika maisha yake. Mwamini aliyekomaa hapotezi imani wakati anapojikuta hajui ni kwa sababu gani jambo fulani gumu linamtokea.

## Hitimisho

Tabia za kukomaa kiroho hazitegemei kipaji cha asili.

Hazifanani na ujuzi wa huduma.

Siyo lazima ziambatane na uwezo wa uongozi. Ni jambo jema kama kiongozi atakuwa amekomaa kiroho, lakini wakati mwingine mtu huwa kiongozi kwa sababu ya uwezo wake alio nao, wakati yeye bado hajakomaa kiroho. Wakati mwingine unakuta mtu amekomaa kiroho, lakini hana ule uwezo wa uongozi.

Baadhi ya nafsi nyingine za watu huonekana kwa asili zaidi ni zenye uvumilivu na wema. Sifa za asili za mtu binafsi hazifanani na kukomaa kiroho. Mungu hufanya kazi ndani ya nafsi zetu na kusaidia kuleta uwiano kwenye tabia zetu. Kama tukimfanyia tathmini mtu fulani, hatuwezi kutofautisha kwa uhakika kati ya nafsi ya asili ya mtu na tabia za maendeleo ya kiroho.

Matatizo ya kiafya yanaweza pia yakaathiri kufanya maamuzi na jinsi anavyopokea mambao. Hivyo hatupaswi tuwe watu wa kufanya haraka katika kuwahukumu watu wengine.

## Kazi za Kufanya

(1) Jipime mwenyewe kupitia katika hizi tabia kumi za kukomaa kiroho. Kwa njia ya maombi tafakari ni zipi katika hizi ambazo umezikosa zaidi. Panga ni kwa jinsi gani utajiongeza katika hizo, Kupitia maombi, kujifunza, kupokea ushauri kutoka kwa watu wengine, na kutegemea msaada wa Mungu.

(2) Je, ni kwa njia gani za makusudi kanisa linaweza kutimiza jukumu lake la kufundisha na kuwajibika kiroho? Andika kurasa mbili ukielezea mpango kazi kwa ajili ya kanisa.

# Somo la 18
# Kitabu cha Mwongozo kwa Kikundi Kidogo

## Kumbukumbu kwa Kiongozi wa Darasa

*Somo hili halijawekwa kwa ajili ya kipindi cha darasa kama yalivyo masomo mengine. Hata hivyo unaweza ukalitumia kwa kufundishia, na kuna mada nyingi kwa ajili ya majadiliano. Itakuwa ni jambo la umuhimu kukutana angalau zaidi ya mara moja kwa ajili ya somo hili.*

*Darasa linapaswa lichukue muda mahususi kujadili kuhusu hatua zao za baadaye. Watapaswa wapannge kwa pamoja jinsi watakavyoweza kusaidia makanisa ya mahali pamoja kwenye majukumu ya uinjilisti na ufuasi.*

## Thamani ya Vikundi Vidogo kwenye ufuasi

Huduma ya vikundi vidogo inakuwa na mifumo ya aina nyingi katika dunia yote. Kuna aina nyingi ya vikundi vodogo, vilivyoandaliwa kwa malengo tofauti. Vikundi vidogo vinaweza kukutana kwa ajili ya kujifunza, uwajibikaji wa kiroho, huduma, maombi, au kwa ajili ya miradi maalumu.

Baadhi ya makanisa yamegawanyika kwenye vikundi ambavyo vinakutana majumbani. Hivi vikundi vidogo hufanya kazi zake kama kanisa ndogo Makanisa ya wakati wa Agano Jipya inaonekana yalifanya kazi kwa jinsi hii.

Katika kukua, makanisa yenye ufanisi yana mfumo wa aina fulani ya vikundi vidogo.

Katika sehemu hii, tutazungumzia kuhusu ufanisi wa vikundi vidogo kwa ajili ya huduma ya ufuasi.

## Mtindo wa Wesley

John Wesley (Uingereza, katika karne ya 18) alikuwa siyo wa kwanza kutengeneza mfumo wa vikundi vidogo ambavyo vilikuwa na ufanisi sana.

Wesley alikuza mfumo wa ufuasi akitumia vikundi vilivyokuwa na ukubwa unaotofautiana.[205] Mitindo ya Wesley haikuwa mifumo kamili iliyokuwa imekamilika pale mwanzoni, lakini iliendelezwa hatua kwa hatua kulingana na mahitaji. Wengi wa watu wa Wesley waliokuwa wameokoka walikuwa wanaomba kutiwa moyo, ushauri na maombi. Kwa kuwa walikuwa wengi sana, aliwapanga wawe wanakutana kila siku ya Alhamisi.

---

[205] Angalia "A Plain Account of the People Called Methodists," katika *The Works of John Wesley, Volume VIII* (Grand Rapids: Zondervan), 249-258.

Katika kila eneo ambalo Wesley na wahubiri wake walipeleka injili waliwapanga waliookoka kwenye vikundi ambavyo vilikutana mara kwa mara. Kwa kuwa makusanyiko yalikuwa makubwa, wengi walikuwa hawawezi kuelezea kuhusu mahitaji yao ya kiroho na walikuwa hawapati uangalizi waliouhitaji. Vikundi vidogo viliundwa vikaitwa madarasa, ambapo viongozi wao walitumika kama wachungaji ili kuwatia moyo na kuwaongoza washirika. Kila mshirika aliyeonekana anaendelea kutumika kwenye dhambi iliyo Dhahiri na hataki mabadiliko, aliondolewa kwenye ushirika na hakuruhusiwa kuja tena kwenye mikutano ya kikundi.

Vikundi vidogo kuliko uwezo wa madarasa vilianzishwa ili washirika waweze kushirikishana katika vita vyao vya kiroho na kumpa kila mmoja uwajibikaji wa kiroho. Katika vikundi hivi kiongozi anaelezea hali yake yeye mwenyewe ya kiroho, kisha anauliza washirika wengine maswali kuhusiana na hali zao za kiroho, dhambi, na majaribu. Kwenye vikundi hivi, washirika wake wote walikuwa wa jinsia moja.

Mafanikio ya Wesley yalisababisha mtu aliyekuwa maarufu sana George Whitefield kutoa taarifa hii: "Ndugu yangu Wesley alifanya kwa busara sana - roho ambazo zilikuwa zimeamshwa chini ya huduma yake ziliunganishwa katika darasa, na kwa ajili hiyo akafaulu kutunza tunda la kazi yake. Katika hili mimi nilipuuzia, na watu wangu wakawa tepetepe." Mtindo wa Wesley uliendelezwa na kanisa la Wamethodisti la Marekani kwenye miaka ya mwanzo, lakini kanuni zake za ufuasi pamoja na mafundisho yake ya imani yamepuuzwa na Umethodisti wa wakati huu.

## Kuelewa Kanisa lenye Msingi

Jengo la kanisa la kwanza lilijengwa takribani mwaka wa 250 B.K. Kwa karne mbili za mwanzo, kanisa lilijona lenyewe kama ni watu, siyo kama jengo au shirika. Kanisa limeundwa na vikundi vya Wakristo wanaoabudu kwa pamoja, wanaofanya uinjilisti, na wanaotii Biblia.

Vikundi vidogo vya watu ndiyo matofali yanayojenga kila kanisa lenye ufanisi. Programu ya ufuasi kwa ajili ya vikundi vidogo siyo taasisi mpya ambayo siku moja itakuwa imepitwa na wakati, Siyo mtindo mpya unaoweza kufanya kazi katika maeneo kadhaa na usifae kwenye maeneo mengine. Badala yake, vikundi vidogo ndio matofali ya msingi wa kanisa. Huduma kwenye vikundi vidogo inaweza ikafanywa kwa njia nyingi ili kukidhi changamoto ambazo kila kanisa linakutana nazo.

Kanisa halitaweza kukidhi malengo yake hadi pale watu wake watakapokuwa wameimarishwa na kufundishwa katika mfumo ulio wa kibinafsi zaidi kuliko ushirika wote kwa pamoja au wakati mwingi wa shule za Jumapili.

### Tahadhari

Vikundi vidogo vitakuwa tu vya kiroho kama watu wanaohusika kwenye vikundi hivyo watakuwa watu wa kiroho. Kama hawatakuwa wafuasi waliojitoa kabisa katika kipaumbele

cha kumpendeza Mungu, kuishi kwa uaminifu, na kukamilisha kazi ya umisheni ya kanisa, kuna njia nyingi ambazo kikundi kinaweza kupotoka na kwenda vibaya au visivyo.

## Hitaji la Kuwajibika Kiroho

Kuwa na uwajibikaji wa kiroho ni kuanzisha uhusiano na mtu au kikundi ambako hapo wewe unawajulisha hali yako ya kiroho, mafanikio yako ya kiroho, au kushindwa kwenye nidhamu za kiroho, na ahadi yako kwa ajili maendeleo. Watakuambia ni wapi wanapofikiri kwamba unaenda vibaya. Utawapa ahadi yako kwamba utatekeleza, na watakuuliza baadaye kama umetekeleza ahadi yako.

Msingi wa kibiblia wa uwajibikaji wa kiroho kwenye jumuiya yenye afya ya Kikristo umefafanuliwa kwa makini sana kwenye sehemu iliyotangulia. Pasipo uwajibikaji wa kiroho, hatutaweza kutimiza amri na maagizo yoye ya Maandiko; na, tutaipuuzia njia ambayo Mungu ameipanga kwa ajili ya kutupa sisi neema.

> Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.[206]

Mtu hatakiri madhaifu yake ya binafsi pasipokuwepo na uhusiano ambao utarahisisha jukumu hilo. Kama hatafanya ukiri wake kwa mtu ambaye atafanya maombi kwa ajili ya madhaifu yake, anapuuzia njia ya Mungu aliyoipanga kwa ajili ya kukutana na madhaifu hayo.

> Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.[207]

Kama hatumjui mtu vizuri, hatuwezi kujua ana mizigo gani mizito aliyo nayo. Hatuwezi kutimiza agizo hili la kimaandiko bila uhusiano ambao utawezesha hilo.

> Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri.[208]

Tunapaswa tujipime kila mmoja na mwenzake kwa ukaribu kwa nia yenye upendo ili tuweze kujua ni aina gani ya mambo ya kutia moyo na ya kurekebisha ambayo ni muhimu. Mambo ya kutia moyo yanaweza yakashindikana, na mambo ya kurekebisha yanaweza kukwama kama hatutakuwa na mahusiano na mtu mwingine.

Maswali yafuatayo yanaweza kusaidia mtu kujipima kama uwajibikaji wa kiroho upo au haupo katika maisha yake.

Je, nina mahusiano gani ambayo yanasababisha kuwe na uwezekano mtu kushikamana nami katika kubeba mizigo yangu mizito, ninakiri madhaifu yangu kwa mtu mwingine, ninasaidia mtu mwingine katika kubeba mizigo yake, na mtu mwingine anawajibika kwenye hali yangu ya sasa ya kiroho?

---

[206] Yakobo 5:16
[207] Wagalatia 6:2
[208] Waebrania 10:24

Je, kuna nyakati ambazo hakuna mtu yeyote ambaye naweza kumtegemea, nyakati ambazo nina furaha kwamba hakuna mtu anayejua hali yangu, na nyakati ambazo ninakwazika kutoa taarifa ya muda wangu wa maombi au muda wangu wa kujifunza Biblia?

Makanisa mengi hayatimizi wajibu wao wa uwajibikaji wa kiroho isipokuwa wawe wamepanga mfumo wa kufanya hivyo. Kwa wengi, huo ni mfumo wa vikundi vidogo.

## Sifa za Kiongozi wa Kikundi kidogo

Yesu alionyesha kipaumbele cha ufuasi. Tangu mwanzo wa huduma yake alichagua watu wachache ambao wangechukua jukumu la kuliongoza kanisa. Hakutumia muda wake mwingi katika kuhubiri kwa maelfu ya waatu waliokuwa wanamfuata; badala yake, mara kwa mara alikuwa anakuwa na muda wa kuwafundisha wale wanafunzi kumi na wawili. Aliiendeleza huduma yake kupitia kwa wale aliokuwa amewafundisha.

Mtu ambaye anafanya huduma ya ufuasi anapaswa awe na tabia hizi zinazofuata hapa chini. Hawezi akawa ni mzuri sana katika kila sifa, lakini itabidi ajaribu kuziboresha zote. Ikiwa atakosa sifa moja katika hizo, ufanisi wake utakuwa wa kiwango cha chini.

> "Ingawaje alifanya lile aliloliona linawezekana katika kusaidia watu wengi, kimsingi ilibidi ajitolee mwenyewe kwa watu wachache, kuliko umati wa watu, ili kwamba angalau walio wengi waweze kuokoka. Hii ilikuwa ni busara ya mkakati wake."
> - Robert Coleman,
> *The Master's Plan*

### (1) Aliyekomaa Kiroho

Anapaswa awe na sifa za kukomaa kiroho zilizoelezwa katika sehemu iliyotangulia. Kama siyo mtu aliyekomaa kiroho, hataweza kuonyesha mfano mzuri na hataweza kuwa na uzoefu atakaouhitaji.

### (2) Anayepatikana

Kama ratiba yake tayari unakuta imeshajaa na haijasimamiwa vizuri, hawezi kupatikana kwa ajili ya huduma ya vikundi vidogo. Ni lazima kupatikana kwake kuwe kipaumbele.

### (3) Anayeaminika

Ni lazima awe mtu anayetimiza ahadi zake. Ni lazima awe mtu anayetunza miadi anayofanya. Ni lazima awe mtu wa kuweza kuwafanya watu wengine waweze kuwajibika katika miadi yao.

### (4) Mwenye kujiamini

Ni lazima aamini kwamba ana uwezo wa kujifunza jinsi ya kuongoza kikundi. Kama atakuwa ana uwezo lakini hajiamini, anahitaji kwanza uongozi wa mtu mwenye uzoefu ambao utamsaidia kujenga ujasiri wake.

**(5) Uwezo wa kutatua migogoro**

Anahitajika awe na uwezo wa kuweka mtazamo sahihi au kamili wakati inapotokea watu kutokubaliana na hatimaye kusababisha matatizo. Anahitajika awe na uwezo wa kusaidia kutatua migogoro kati ya watu wengine.

**(6) Uwezo wa kufundisha**

Je, watu wanaelewa maelezo yake? Kiongozi anatakiwa asiwe mtu mwenye kuwachanganya watu.

**(7) Mwenye njaa ya Neno la Mungu**

Ni lazima awe mtu wa kufurahia Neno la Mungu, ili aweze pia kuwaalika na watu wengine wakalifurahie Neno. Ni lazima ahakikishe anaifanya Biblia kuwa kitu cha muhimu sana katika uhusiano wake na Mungu.

**(8) Mwenye kumtegemea Mungu**

Ni lazima afahamu kuwa matokeo ya kiroho yaweza kusababishwa kwa kazi ya Roho Mtakatifu tu. Anapaswa awe tayari kushirikiana na Roho Mtakatifu. Ni lazima ategemee upako kutoka kwa Mungu. Hapaswi kujiamini kuwa ufafanuzi wake utafanikiwa kwa sababu ya uwezo wake tu.

**(9) Aliye tayari kutumika**

Ni lazima awe mtu ambaye anajisikia kwamba anafanya jambo la thamani wakati anapokuwa anahudumia wenzake. Hapaswi kuwa mtu anayetakakutumikiwa. Hapaswi kutafuta huduma kwa kusudi la kudhihirisha vipaji vyake. Anatakiwa awajibikie katika mahitaji na awe tayari kujitolea.

**(10) Kukaa chini ya mamlaka ya kiroho**

Anapaswa awe anawajibika chini ya mamlaka ya kiongozi wa kiroho. Anatakiwa awe anafuata maelekezo ya viongozi wa kiroho.

**(11) Mwaminifu kwa kanisa**

Kiongozi wa kikundi anapaswa awe mshirika aliyejitoa kabisa kwa kanisa la mahali pamoja. Huduma ya ufuasi inapaswa kusababisha watu kukubaliana na kanisa na zaidi wawe watu waliojitoa kwa kanisa kabisa.

**(12) Ari ya mafanikio**

Kam atakuwa ana ari ya mafanikio, hatakata tamaa kwa haraka. Atakabiliana na mazingira ya huduma. Atatafuta taarifa za kumsaidia aweze kuwa na ufanisi zaidi. Atatumia maarifa wakati kunapotokea matatizo au fursa. Atakuwa na nguvu na shauku ya huduma.

**(13) Usahihi wa mafundisho ya imani**

Anapaswa awe na msingi mzuri wa kibiblia, na mafundisho ya imani ya kufanya uinjilisti.

**(14) Aliyefundishika kwa ajili ya huduma**

Siyo lazima mafundisho yafanyikie kwenye taasisi ya taaluma. Mafundisho huanzia kwa uchunguzi, jinsi mwamini anavyoiona huduma ikifanyika. Mafunzo huongezeka kwa ushiriki, wakati anapopewa majukumu chini ya maelekezo. Kusoma na kujifunza kwa kutumia nyenzo nzuri za mafundisho ni jambo muhimu sana.

## Kutengeneza Programu ya Ufuasi

Njia nzuri sana ya kufanya huduma ya ufuasi iwepo ni kwa kanisa la mahali pamoja kuelewa majukumu, kipaumbele cha ufuasi na kufanya kazi kwa umoja.

Kwa hiyo, maelekezo haya ni kwa ajili ya viongozi na washirika waliojitoa kabisa kwa kanisa.

Kama kanisa litatambua kwamba wanataka wafanye vizuri kwenye ufuasi, kwanza inabidi wajifunze maandiko na vipengele vilivyoko katika kozi hii ya ufuasi. Viongozi wanaweza kuwasilisha nyenzo za mafundisho haya. Washirika wote waliojitoa kabisa kwa kanisa kama inawezekana wanaweza wakashirikishwa, ili waweze kushiriki maono haya.

Sehemu ya pili ya maendeleo ni kuchunguza kile ambacho tayari kanisa linafanya. Makanisa mengi yana vikundi ambavyo tayari vinafanya kazi, hata kama bado hawakuwa na makusudi hayo ya kuzindua programu ya vikundi vidogo. Kwa mfano, kunaweza kuwepo na kikundi cha wanamuziki ndani ya kanisa ambacho hukutana mara kwa mara. Kunaweza kuwepo na kikundi cha uimbaji kinachofanya mazoezi mara kwa mara. Kunaweza kuwepo na kikundi cha mashemasi. Kunaweza kuwepo na vikundi kwa ajili ya masomo ya shule ya Jumapili, na waalimu wa shule ya Jumapili pia wanaweza wakaunda kikundi chao. Vijana katika kanisa wanaweza wakawa wanakutana mara kwa mara. Kamati mbalimbali za kanisa zinaweza kuwepo na kukutana kwa ajili ya kuangalia majukumu kadhaa ya kanisa. Kikundi kisicho rasmi kinaweza kufanya kazi kwenye mradi pamoja. Kunaweza kuwepo na familia ndani ya kanisa ambazo hukutana kwa pamoja mara kwa mara kwa ajili ya urafiki. Inawezekana kukawepo na mafundisho ya Biblia majumbani na vikao vya maombi.

Vikundi hivi vyote havijaanzishwa kwa ajili ya huduma ya ufuasi au uwajibikaji wa kiroho, lakini vinaweza kusaidia katika kutimiza malengo hayo. Kanisa lolote ambalo lina uhai wa kiroho lina vikundi kadhaa ambavyo vinasaidia katika uhai wa kanisa. Wakati kanisa linapoamua kujiongeza kwenye programu yake kwa ajili ya ufuasi, linapaswa lifanye tathmini ya vikundi vilivyopo na kutaka kujua ni nini kinachoendelea, kisha tafakuri ifanyike kuona ni kwa jinsi gani lengo linaweza kufikiwa kwa njia iliyo bora zaidi.

Vikundi vipya vinaweza vikahitajika. Inawezekana aina nyingine ya vikundi ikahitajika. Kunaweza kukawepo na vikundi vya kutoa mafunzo ya vitendo kwa ajili ya huduma.

Kunaweza kuwepo na vikundi ambavyo kimsingi ni kwa ajili ya mafundisho ya Biblia na maombi. Kunaweza kuwepo na vikundi vidogo kwa ajili ya uwajibikaji mzito wa kiroho.

Lengo la kikundi huamua nani awepo na kwa jinsi gani kikundi kitafanya majukumu yake. Kwa mfano, Kikundi kwa ajili ya uwajibikaji mzito wa kiroho kinapaswa kiwe na watu wasoizidi kumi. Endapo kikundi kitakuwa na watu wengi sana, uwajibikaji unapungua, ushirikishanaji unakuwa hauna nguvu, uangalizi mkubwa zaidi utahitajika, ushiriki mdogo ni jambo linalowezekana kutokea, na mahudhurio huenda yakawa mabaya sana. Undani wa ushiriki wa mtu utakuwa finyu kama wanaume na wanawake watachangamana pamoja.

Lengo la kikundi huamua kama nafasi kwa ajili ya washiriki wapya iwepo au isiwepo. Kama lengo ni kwa ajili ya uwajibikaji wa kiroho, haitakuwa jambo la busara kuongeza washiriki wapya baada ya kikundi kuwa kimeshakutana mara kadhaa. Watu wengi hawatataka kushirikisha hali zao za kiroho hadi pale watakapojiona wana usalama na watu wengine waliopo kwenye kikundi. Kama lengo la kikundi ni kukamilisha masomo ya mfululizo na au mfuatano, siyo jambo la busara kuongeza watu wengine wapya wakati wa mafunzo.

Kunaweza kuwa na kikundi cha watu wapya waliookoka.[209] Ni jambo muhimu kwamba watu hawa hawapaswi wakae nje kwa wiki kadhaa kabla hawajajiunga kwenye kikundi. Kwa hiyo, kikundi hiki kinahitaji mafunzo yanayozunguka ambayo yatatoa nafasi kwa watu wapya kujiunga wakati wowote. Viongozi watapaswa watambue kwamba baadhi ya watu wapya walioamua kuokoka wanaweza kuamua kutoendelea na mafunzo. Pamoja na ukweli kwamba watu wengine wataweza kuamua kuondoka kwenye kikundi, hiyo haimaniishi kwamba kikundi hakifanyi vizuri. Ingawaje watu wengine wanaweza wakaamua kuondoka, kikundi cha waamini wapya kinapaswa kiwe wazi kwa ajili ya watu wapya.

Kama kikundi ni kwa ajili ya kutoa huduma ya mafunzo au maendeleo zaidi ya kina ya kiroho, watu wa kikundi wanapaswa wawe walio na shauku ya kukua kiroho na wanaotaka kuwajibikia kwa moyo wote makusudio ya kikundi. Endapo baadhi ya washirika katika kikundi siyo wenye kuwajibika kikamlifu, kikundi hakitakuwa na uwezo wa kufanya vizuri na hakitafikia malengo yao.

Washiriki wengi ni lazima wapewe mafunzo ya awali kwa mwaliko wa binafsi. Usngojee watu watake au waombe wenyewe kujiunga.

Siyo kila mtu katika kanisa atakayeweza kujihusisha katika progaramu ya vikundi vidogo. Kama wewe ni kiongozi kwenye kanisa, usiwakimbize watu kwa kuwalaumu kwa kutoshiriki katika kikundi kidogo. Kuza huduma ya kikundi kwa kuelezea faida zake.

---

[209] Shepherds Global Classroom inatoa kitabu cha masomo 26 kwa ajili ya huduma ya uanafunzi kwa waamini wapya. Chanzo hiki cha bure kiitwacho, *Masomo ya Kukuza Uanafunzi*, kinapatikana kwa kupakua kwenye mtandao wa shepherdsglobal.org.

Kwenye kikao cha kwanza, hakikisha kila mmoja anaelewa umuhimu wa kikundi. Shirikisha maandiko na taarifa ambazo zinaonyesha umuhimu wa ufuasi.

Ili kusaidia mahudhurio, kikundi kinaweza kupangwa kukutana kwa majuma kadhaa. Elezea kwamba kikundi kina mpango wa kukamilisha mfululizo wa masomo maalumu, na uwaeleze mwisho wa huo mfululizo wa masomo utakuwa lini. Kwa njia hiyo, kila mwanachama anajua hasa anachojitolea. Sisitiza kuhusu hitaji la mahudhurio yaliyo mazuri. Muda wa mafunzo ukishamalizika, kikundi kinaweza kikaanza tena na wale watu ambao bado watahitaji kuendelea.

**Hali ya kufikiriwa**

Andrea amekuwa Mkristo kwa miaka kadhaa. Yeye ni mshirika wa kanisa na huwa anasaidia majukumu kwenye kanisa. Anachojali sana ni kwamba kanisa lake halina mpango wa kufanya huduma ya ufuasi. Anawaza kama kanisa lingeanzisha vikundi vidogo, lakini viongozi wa kanisa hawana mpango katika hilo.

► Je, Andrea afanye nini?

Itabidi Andrea aongee na viongozi wa kanisa na aombe kibali cha kuongoza kikundi kidogo. Hapaswi kulaumu huduma ya kanisa, lakini badala yake ataelezea faida zitakazopatikana kutokana na kikundi. Kama kikundi kitafanya vyema, kanisa litaanza kuelewa faida za aina ile ya huduma.

**Kuongoza kikundi chenye ufanisi**

Mwanzoni kabisa kikundi kinapoanza, kuna msisimko na matarajio, Washirika wengi wa kikundi hawajui ni nini hasa cha kutarajia, lakini wanakuwa na matumaini ya kupata msaada kutoka kwenye kikundi.

Maelekezo yafuatayo yatasaidia kikundi kuwa cha ufanisi na kutimiza makusudi yake. Kuna kanuni muhimu kwa ajili ya vikundi kuweza kufanya majukumu yao. Kama kiongozi atasaidia kikundi kufuata kanuni hizi, atakuwa amepunguza kuchanganyikiwa na kukata tamaa.

Kikao cha kwanza kitakuwa tofauti na vikao vingine kwa sababu kikundi kinajifunza jinsi vikao vitakavyokuwa. Hata hivyo, kikao cha kwanza kitaweka mfumo kwa ajili ya vikao vitakavyofuata. Kama mtu hatapata nafasi ya kuzungumza kwenye kikao cha kwanza, mtu huyo ategemee kuwa kimya katika vikao vingine vya baadaye. Kama mtu atatawala mazungumzo, kikundi kitategemea mtu huyo aendelee kumiliki vikao vingine vya baadaye. Kama kikao kimekuwa hakina utaratibu na mpangilio mzuri, watategemea hali hiyo hiyo kwenye viako vitakavyofuata. Kama kikao ni kama darasa lililo na ushiriki hai mchache, wategemee mfumo huo huo kwenye vikao vinavyofuata.

Baadhi ya wajumbe wanaweza wakajiondoa baada ya kufanyika kwa vikao vichache kwa sababu kikundi kimekuwa siyo tegemeo lililokuwa linatarajiwa. Ni muhimu kuongoza

kikundi kwa usahihi ili washiriki waliokuwa wanategemea mambo mazuri wasikatishwe na tamaa.

## Miongozo kwa ajili ya kufika kwenye Ufanisi

**(1) Kipange kikundi kiweze kukutana kila wiki, kama itawezekana. Wengine wanaweza wakahitaji msaada kwa ajili ya malezi ya watoto wao wachanga.**

**(2) Mtiririko wa vikao utakuwa kama ifauatavyo: (1) Muda wa kujifunza, kisha, (2) Kushirikishana mahitaji mbalimbali ya kuombea, kisha, (3) Maombi.**

Kama msingi mkuu wa kikundi ni kujifunza, muda wa kujifunza unaweza ukawa mrefu na sehemu nyingine zikawa fupi; lakini sehemu hizi tatu ni lazima zihusishwe. Kama kusudi la kikundi ni kwa ajili ya uwajibikaji wa kiroho, muda wa kujifunza utapaswa uwe mfupi, lakini watakuwa wanazo nyenzo nyingine za mafunzo ambazo wanajifunza.

Kama kikundi kina mambo binafsi ya kushirikishana na kujadiliana lakini hakuna vifaa vya masomo yeyote ya kujifunza, inawezekana kukawa na kutoelewana. Kikao kitatawaliwa na baadhi ya washiriki walio na haiba kuzidi wengine. Vifaa vya kujifunzia huwafanya watu wote washughulike zaidi na ukweli kuliko yale waliyo nayo kwenye mawazo yao.

**(3) Anza na kumaliza kikao katika muda uliopangwa.**

Kama utaanza na kumaliza vikao kwa kuchelewa, wale wanaojali muda wao wataanza na wao kuja kwa kuchelewa au kukwepa baadhi ya vikao.

**(4) Weka muda wa kusitisha kikundi.**

Washirika wa kikundi watahitaji kujua ni kwa muda gani wataendelea kuwepo kwenye kikundi. Kwa kawaida washirika wapya wasiruhusiwe kujiunga na kikundi baada ya kuwa kumefanyika vikao kadhaa, labda iwe kikunda kina mzunguko wa masomo kwa ajili ya waamini wapya. Kama kikundi kinajifunza mafunzo ya mzunguko ya mfululizo wingi wa masomo unaweza kuwa kipimo cha wiki ambazo wataweza kukutana. Kama wanakutana kwa ajili ya uwajibikaji wa kiroho, wanaweza wakajiwekea kiwango cha miezi sita. Wakifika mwisho, wataanda tena upya. Kwa wakati huo baadhi ya washirika katika kikundi wanaweza wakaondoka, na kikundi kinaweza kikafikiria tena aidha kuwaingiza au kutowaingiza washirika wapya kujiunga.

**(5) Wakati wa kujifunza, sisitiza kuhusu kusudi linalobadilisha maisha badala ya maarifa kama maarifa.**

Mshirika wa kikundi atajihisi kwamba kikundi kinafaa kama atapata kitu cha kipekee cha kutumia katika Maisha yake binafsi kutoka katika mafundisho.

**(6) Kufuatilia ahadi.**

Kama mtu ameshirikishana tatizo lake kisha akakubali kuchukua hatua, uliza kwenye kikao kinachofuata endapo kama amefanya kama alivyoahidi kwamba atafanya.

**(7) Kiongozi anapaswa kupatikana ili kukutana binafsi ili kutoa maelekezo ya kiroho.**

Washirika wengine mara nyingine wanaweza wakakaa pamoja kwa ajili ya kutiana moyo.

**(8) Chagua eneo zuri la kufanyia kikao.**

Mahali pa kufanyia kikao pasiwe mahali rasmi lakini pawe ni eneo lenye mazingira ya nyumbani. Kikao kifanyike katika mazingira ya mkao wa mviringo kwa kadri inavyowezekana kusudi kila mshirika wa kikao aweze kumwona mwenzake usoni. Hali hii itamtia moyo mshiriki. Kikao kifanyike mahali ambapo hapatakuwa na usumbufu au vikwazo.

**(9) Jenga tabia nzuri za kusikiliza.**

Ishara za kusikiliza vizuri ni kwa macho kukutana, kujieleza kwa hisia, kupuuzia usumbufu, na kuwa na mwitikio kwa ucheshi wa mnenaji na hisia zingine.

**(10) Hakikisha hakuna mshirika wa kikundi ambaye kila siku ananyamaza bila kuongea chochote.**

Elekeza swali kwa mtu ambaye siyo mwongeaji sana katika kikao ("Charles, unafikirije kuhusu suala hili?").

**(11) Usimlazimishe mshirika wa kikundi kushirikisha kitu chake binafsi.**

Badala yake, tengeneza mazingira ambayo atajisikia huru kuongea. Jenga ujasiri wa mshirika wa kikundi kwa kumtazama machoni na kumpongeza kwa kile atakachosema.

**(12) Jaribu kuuliza maswali watakayoweza kujibu ili kujenga ujasiri wao.**

Kama mtu atatoa jibu lisilo sahihi, jaribu kuthibitisha kitu kizuri kilichoko kwenye jibu lake kabla ya kufanyia tahakiki jibu lake.

**(13) Jaribu kuthibitisha kila ushauri unaotolewa kabla ya kuanza kusahihisha**

**(14) Kama kuna mtu wa kuzungumza sana na kutaka kujibu kila swali, tafuta namna ya kumthibiti**.

Njia mojawapo ya kuweza kufanya hivyo ni kuelekeza maswali kwa baadhi ya washirika wengine wa kikundi waliopo. Au unaweza kuuliza, "Je, ninyi wengine mliobakia mnasemaje?" Kwenye majadiliano, unaweza ukasema, "Tusikilize kutoka kwa mtu mwingine ambaye hajaongea kabisa kuhusu jambo hilo."

Kama bado mshirika huyo anaendelea kuongea sana, kiongozi anaweza kumwomba atoke naye nje ya eneo la kikao kwa mazungumzo. Anaweza akakuambia jambo kama hili, "Charles, wewe ni mtu unayefikiri kwa haraka na una uwezo wa kuingilia jambo lolote kwa haraka kwenye majadiliano, lakini ninajisikia kwamba wengine wetu hawataweza kushiriki

kama tutajibu kila kitu kwa haraka. Je, unaweza kunisaidia kumfanya kila mmoja aweze kuhusika?”

**(15) Usiruhusu washirka wengine wawili au watatu kuwa na vikao vyao vya chini chini huku wakipuuzia kikundi.**

Kama kuna mtu ambaye anataka aendelee na kubishania kuhusu jambo fulani, mwambie kwamba majadiliano yatakamilishwa baadaye nje ya kikao.

**(16) Usiruhusu mtu mwingine aingilie kati ili awavuruge wasemaji wengine.**

Nyoosha mkono wako, na mzuie kwa dhati yule mtu anayeingilia kati kuvuruga, na ruhusu msemaji wa kwanza aendelee kuzungumza hadi kumaliza. Vinginevyo, majadiliano wakati wote yatakuwa yanatawaliwa na watu wachache wasiokuwa na maadili. Watu ambao hawana uthabiti wa mambo, watajisikia kufadhaishwa kwamba wanashindwa kumalizia sentesi zao katika majadiliano hayo.

**(17) Sikiliza malalamiko.**

Lalamiko lolote linaweza kuonyesha tatizo ambalo linaweza kurekebishwa. Usipuuzie hali zinazojitokeza za kuonyesha kutoridhika. Kama mtu ataonyesha kutoridhika na kikao hicho cha kikundi, hataweza kuelewa kusudio, au inawezekana akawa na lalamiko sahihi na lenye sababu thabiti.

**(18) Endapo mshirika wa kikundi anaonyesha uadui, kuchafua, ubishi, anaweza kuwa hakubaliani na malengo ya kikundi.**

Kikundi kinaweza kisifikie kuwa pale kilipokuwa kimekusudiwa. Zungumza na mtu huyu pembeni umsaidie aweze kuliona kusudi la kikundi.

**(19) Kiongozi siyo lazima awe na jibu la kila tatizo.**

Dhima ya kiongozi siyo kuwa na jibu la kila tatizo bali ni kukiongoza kikundi kubeba mizigo yao katika maombi.

**(20) Kuwa mtu mwenye uwezo wa kubadilisha mipango na mvumilivu wakati ratiba inapovurugika.**

Kumbuka kwamba matukio mengi katika maisha yetu ni sehemu ya mpango wa Mungu wa maendeleo kwa ajili yetu. Tatizo linaleta uwepo wa fursa nyingine.

**(21) Kama mshirika wa kikao mara kwa mara atakuwa anataka akifanye kikao chote ni cha kushirikisha mahitaji yake, mpatie siku nyingine ya kumpa ushauri.**

Vinginevyo, washirika wengine katika kikundi watajihisi kwamba wanapokonywa kikao chao. Usitoe fursa kwa kikundi kupoteza kusudi lake, labda iwe washirika wote wa kikundi wamekubaliana kwa pamoja kwamba kusudi hilo linapaswa libadilishwe.

**(22) Usiruhusu majadiliano yawe ya kichochezi.**

Usitoe fursa kwa kikundi kuwa ni jukwaa la kutolea lawama dhidi ya kanisa la mahali pamoja na viongozi wa aina zote.

**(23) Kumbuka kwamba ufanisi wa kikundi unategemea sana nguvu za Mungu zinazofanya kazi kupitia katika kikundi hicho.**

Kikundi ni muundo tu wa kimaandiko ambao Mungu anautumia.

# Somo la 19
# Kuwaombea Wafuasi

## Kumbukumbu kwa Kiongozi wa Darasa

*Kwenye somo hili la mwisho, kikundi kitajifunza kuhusiana na jinsi maombi ya Paulo kwa ajili ya waamini yanavyotoa mwelekeo wa maombi na huduma zetu.*

*Kisha, somo linatambulisha mfululizo wa masomo kwa ajili ya huduma ya ufuasi. Darasa litapaswa liangalie baadhi ya masomo hayo wakati wanafunzi wakiwa wanajifunza somo hili, kisha wapange jinsi ya kutekeleza kazi ya kufanya ya mazoezi ya vitendo.*

*Kikundi kitawajibika kikutane zaidi ya mara moja ili kutekeleza kazi hii ya kufanya.*

*Wanafunzi ambao wameshafuzu masomo ya kozi ya Uinjilisti wa Kibilia na ufuasi itawabidi wafanye mazoeziya masomo haya kwa ajili ya watu wapya waliookoka. Kwanza, mtu mmoja itabidi aoneshe jinsi ya kufundisha somo kwa kufundisha somo moja kwenye kikundi. Kisha, kila mwanafunzi atapaswa kufanya zoezi la kufudisha angalau somo moja. Baada ya darasa kuona somo moja lililotolewa kama kielelezo, wanaweza wakagawanyika kwenye vikundi vingine vidogo kusudi watu wengi zaidi waweze kufanya mazoezi kwa wakati mmoja. Kwenye vikundi vya watu wanne, kila mwanafunzi anaweza kuongoza somo na akawaangalia wanafunzi wengine watatu jinsi kila mmoja anavyoongoza somo.*

## Kuomba Maombi ya Paulo kwa Waamini Wapya.

Maombi ya Paulo kwa waamini wapya yanaelezea zaidi kazi ya ufuasi. Maombi haya yanatuongoza sisi kuomba kwa ajili ya Wakristo wachanga kwa sababu tunapaswa tuombe mambo yale yale ya kufanana kwa ajili yao ambayo Paulo alikuwa anaomba. Maombi haya pia yanaongoza huduma zetu kwa sababu tunapaswa tushiriki kile Mungu anachokifanya kwa ajili ya huduma hizo.

Tuangalie maombi ya Paulo kwa ajili ya vikundi vitatu.

### Wathesalonike

► Soma 1 Wathesalonike 5:23-24.

Waraka wa kwanza kwa Wathesalonike unatoa mwito kwa ajili ya utakatifu. Kila mwamini anaitwa kuishi katika maisha ya utakatifu na usafi, na ahadi za Mungu ambazo zinaweezekana kwa njia ya imani. Tunapaswa kuomba na kufundisha kwa lengo la kumleta kila mwamini kwenye ushindi na usafi.

### Wafilipi

► Soma Wafilipi 1:9-11.

Aya hizi zinaelezea kuhusu mchakato endelevu katika maisha ya mwamini. Upendo wake unatakiwa uwe unaoendelea kukua mfululizo. Wakati hilo likifanyika, uwezo wake wa kutambua yaliyo mema unatakiwa nao uongezeke. Akiwa anaendelea kutambua, anayaweka maisha yake katika kutazama kilicho bora zaidi. Hali hii inatakiwa iwe inafanyika kwa kusudi la yeye kuwa msafi (mwenye moyo safi) na bila kuwa na kosa.

Watu ambao Paulo aliwaandikia katika aya hizi tayari walikuwa wameshakuwa Wakristo kwa muda kadhaa. Lakini, bado Paulo alikuwa akiomba kwamba wawe wakiongezeka katika upendo wao kwa Mungu, na, kwa upendo huo, waweze kuelewa vizuri zaidi mapenzi ya Mungu yaliyo kwa ajili yao.

Hapa kuna maswali ambayo mwamini mchanga anapaswa atafakari;

- Je, kuna mfano gani wa mabadiliko ambao nimeufanya katika maisha yangu wakati Mungu aliponionyesha kwamba tabia, silika au kitendo hakikuwa kitu kizuri sana?
- Je, kuna jambo lolote katika masha yangu ambalo nina mashaka kuhusiana nalo?
- Je, niko tayari kumruhusu Mungu anionyeshe katika maombi mabadiliko yeyote ambayo ninapaswa niyafanye?

**Wakolosai**

► Soma Wakolosai 1:9-12.

Aliomba kwamba waweze kupata maarifa ya mapenzi ya Mungu katika hekima yote na ufahamu wa rohoni. Mtu mpya aliyeokoka bado huwa hawezi kuelewa mambo yote kuhusu mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yake. Atakuwa anaona hatua kwa hatua kwamba baadhi ya mienendo, maneno na tabia katika maisha yake vinabadilika. Kwa kuwa anampenda Mungu, atakuwa mara kwa mara anapatanisha zaidi maisha yake kwenye mapenzi ya Mungu. Mtumishi wa huduma ya ufuasi atapaswa kuwa anaomba na kwa uangalifu akifundisha waamini wapya kuyatambua mapenzi ya Mungu.

Alisema kwamba waweze kufanya, kama matokeo ya ufahamu mzuri wa mapenzi ya Mungu, "waenende kama ulivyo wajibu wao kwa Bwana." Watakuwa ni wawakilishi wa Mungu wa kufaa zaidi. Maisha yao yatafanana zaidi na ujuzi wa kubadilishwa kwa neema. Anachotakiwa kukumbuka mhudumu wa uanafunzi ni kwamba hadi hapo mchakato huu utakapokuwa umeendelea kwa muda fulani, baadhi ya mambo yenye kukinzana yatajidhirisha kwenye maisha ya Mkristo mchanga.

Sehemu ya "kutembea kuliko na manufaa" hujumuisha pamoja na "kuwa mtu mwenye kuzaa matunda kwenye kila kazi njema." Hatupaswi kuwa na mshangao wakati tunapomwona mwamini mchanga bado hajaweza kuzaa matunda kwenye kila kazi njema. Atakuwa bado hajaweza kuwa tayari kuwajibika na kuwa makini katika kazi kama ambavyo ingetakiwa awe.

Aya hizi vilevile hutueleza kwamba tunaweza kuwa na, “uvumilivu na mateso ya muda mrefu kwa furaha.” Mtu ambaye anaweza kuwa na furaha ya kikristo anapokuwa anahudumia na kuvumilia atakuwa amepata kiwango kidogo cha ukuaji wa kiroho.

**Hitimisho kuhusu Maombi ya Paulo**

Maombi ya Paulo kwa Wakristo wachanga yanatuelezea zaidi kuhusu kazi a ufuasi. Tunapaswa tuwe na malengo sahihi kwa ajili maendeleo ya waamini. Tunapaswa tuwe na uwezo wa kutambua maendeleo, Hatupaswi kushangaa tunapoona mambo ya kukinzana, kutokuelewana, na kutowajibika ndani ya vijana wadogo wa Kikristo. Tunapaswa tusitegemee kuona sifa zote za Mkristo zitajitokeza ghafla.

Tunapaswa tutambue kwamba Paulo hakuwa anajihusisha sana na huduma zao za mafunzo au kuendeleza ujuzi wa huduma. Alihusika sana na maendeleo ya imani yao na tabia ya Mkristo. Hatupaswi kuendelea kuridhika na watu ambao wanaweza kufanya kazi za huduma lakini wanakosa kuwa na tabia ya Mkristo.

Mwalimu ni muhimu kwa sababu ya mfano wake, na kwa sababu ya thamani ya taarifa. Kujifunza kunasisitizwa katika aina mbili za maombi hapo juu. Ujuzi unahusika kwenye mchakato wa kiroho. Mwalimu ana mguso mkubwa kutokana na matumizi yake ya ukweli.

Tunapaswa tuombe maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo wachanga tunaowapatia hamasa. Tunapaswa tushirikiane na Roho Mtakatifu ili kuwezesha michakato yote kujitokeza ndani ya maisha yao.

Maombi yafuatayo hapa chini yanatokana na maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo wapya.

**Maombi kwa ajili ya Mkristo Mchanga**

Baba wa Mbinguni,

Ninaleta maombi yangu kwako kwa ajili ya ___________ ili uweze kumtakasa kabisa. Ninamwombea kwamba aweze kuwa mtakatifu katika matendo yake, tabia, na nia zake.

Msaidie ili upendo wake kwako uweze kukua, ili kwamba aweze kuelewa vyema mapenzi yako yaliyo makamilifu kwa ajili yake. Msaidie katika kutambua yaliyo mema na siku zote aweze kuyachagua, na kwamba maisha yake yazae matunda kwa ajili ya utukufu wako.

Msaidie aweze kuishi kila siku kama anavyopaswa Mkristo kuishi, akikupendeza wewe katika kila jambo na akijifunza zaidi njia zako. Mpe nguvu zitokazo kwako ili aweze kuishi kwa ushindi na aweze kustahimili majaribu kwa furaha. Mpe kila siku kukushukuru kwa neema unayompatia.

Naomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

# Viambatisho Vilivyopendekezwa

## Vitabu

Coleman, Robert. *The Master Plan of Evangelism*. Ada: Revell, 2010.

Coleman, Robert. *The Master Plan of Discipleship*. Ada: Revell, 1997.

Eims, Leroy. *The Lost Art of Disciple Making*. Grand Rapids: Zondervan, 1978.

Friedeman, Matthew. *The Master Plan of Teaching*. Wheaton: Victor Books, 1991.

Gorman, Julie. *Community That is Christian: A Handbook on Small Groups*. (2nd edition). Ada: Baker Books, 2002.

Neighbor, Ralph. *Where Do We Go from Here?* Touch Publications, 1991. (Available on Kindle, 2011.)

Snyder, Howard*. The Radical Wesley: Patterns for Church Renewal*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1980.

Snyder, Howard. *The Problem of Wineskins*. Franklin: Seedbed Publishers, 2017.

Wilkinson, Bruce. *The Seven Laws of the Learner*. New York: Multnomah, 1992.

## Vianzo vingine kutoka katika mitandao:

Mafunzo ya Uinjilisti, vipeperushi vya injili, na taarifa nyinginezo zinapatikana kutoka Ray Comfort na Kirk Cameron www.livingwaters.com.

Kwa taarifa kuhusiana na Uinjilisti wa nje kwa kutumia picha zilizochorwa, ona mitandao ya Open Air Campaigners kwenye www.oacgb.org.uk na www.oacusa.org.

*Masomo ya Kukuza Uanafunzi,* kutoka Shepherds Global Classroom – masomo 26 yanapatikana kwa ajili ya kuwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi kutoka www.shepherdsglobal.org.

Nyenzo nzuri sana za masomo kwa ajili ya huduma ya uanafunzi zinapatikana kutoka kwa Nathan Brown katika comeafterme.com.

# Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa

Jina la Mwanafunzi ______________________________________

| Somo | Kazi ya kufanya 1 | Kazi ya kufanya 2 | Kazi ya kufanya 3 |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | (mtihani) | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | (mtihani) |
| 11 | | | |
| 12 | | | |
| 13 | | | |
| 14 | | | |
| 15 | | | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).

# Maelezo ya Kozi za Shepherds Global Classroom

### Kuchambua Agano la Kale

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

### Kuchambua Agano Jipya

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

### Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inasoma maisha ya Yesu kama mfano kwa huduma na uongozi katika karne ya 21.

### Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na dhamira kama inavyoelezewa katika vitabu ya Warumi, kujadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa ya kutatanisha katika kanisa.

### Kanuni za Tasfiri ya Kibiblia

Kozi hii inafundisha kanuni na njia za kutafsiri Biblia vizuri ili kuongoza maisha yetu na mahusiano na Mungu.

### Imani za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea mafundisho ya Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, Mwanadamu, Kristo, Wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na Vitu vya Mwisho.

### Eskolojia

Kozi hii inafundisha vitabu vya kibiblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu zingine za maandiko ya kinabii na inasisitiza mafundisho muhimu kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa Mungu wa milele.

### Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

**Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa**

Kozi hii inaelezea ubunifu na mpango wa Mungu kwa kanisa na masomo ya kibiblia kama vile uanachama wa kanisa, ubatizo, ushirika, zaka, na uongozi wa kiroho.

**Historia ya Kanisa I**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyotimiza dhamira yake na kutunza mafundisho muhimu kuanzia kipindi cha kanisa la mwanzo mpaka Matengenezo.

**Historia ya Kanisa II**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyopanuka na lilivyopitia changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo mpaka nyakati za kisasa.

**Uundaji wa Kiroho**

Katika kozi hii wanafunzi wanajifunza kuwa na mitazamo ya yesu, kuwa na Mungu kama Yesu alivyokwa na baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kufanya nidhamu ya kiroho na binafsi ya yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) lililoundwa na Yesu.

**Huduma ya Uongozi**

Kozi hii inahimiza tabia ya Kikristo wakati inafundisha viongozi kuongoza mashirika kupitia mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushirikishana maono, kuweka malengo, kupanga mkakati, kuchukua hatua, na kupitia mafanikio.

**Kanuni za Mawasiliano**

Kozi hii inafundisha theolojia ya mawasiliano, njia za kuzungumza kwa ufanisi, na njia za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

**Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi**

Kozi hii inatoa kanuni za kibiblia ambazo huongoza mbinu za uinjilisti. Inaelezea aina za uinjilisti na kutoa masomo ya kutumia kufundisha wapya waliobadilishwa.

**Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani**

Kozi hii inafundisha misingi ya kisayansi, kihistoria, na kifalsafa kwa mtazamo wa ulimwengu wa Kikristo, na inaonyesha jinsi gani imani ya Kikristo ni thabiti katika hoja na hali halisi.

**Dini za Ulimwengu na Ibada**

Kozi hii huumpa muumini wa kiinjili uelewa wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya dini.

**Utangulizi wa Kuabudu Kikristo**

Kozi hii inaelezea jinsi gani kuabudu huathiri nyanja zote za maisha ya muumini na hutoa kanuni ambazo humuongoza mtu binafsi na mkutano wote mazoezi ya kuabudu.

**Kuishi Kikristo kwa Vitendo**

Kozi hii hutumia kanuni za kiroho kwa utumiaji wa fedha, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na maeneo mengine ya kuishi kwa vitendo.

**Ndoa ya Kikristo na Familia**

Kozi hii inatoa mtazamo wa Kikristo kuhusiana na maendeleo ya binadamu kupitia hatua mbalimbali za maisha na zinatumia kanuni za kimaandiko kwa ajili ya majukumu ya kifamilia na mahusiano.